Jumanne Machi 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580181

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## JPM asimamisha kazi wahandisi wa Tanroads, ampa onyo waziri

UKURASA 5




UKURASA 13

CORONA

# Mgonjwa wa kwanza aripotiwa Tanzania

**ALIINGIA** nchini kupitia KIA, Magufuli afuta mbio za Mwenge, Muhimbili yaanzisha mikakati ya udhibiti... Habari zaidi...*Endelea ukurasa wa 2,3,8*



Askari wa kampuni ya ulinzi ya Nanga, Agnes Noah (kulia), akiwanawisha mikono kwa maji yenye dawa, wananchi waliokuwa wanaingia na kutoka katika lango kuu la Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## BAA LA CORONA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hadi jana, watu 153,517 walikuwa wamepata maambukizo ya virusi vya corona duniani huku 5,737 wakifariki dunia kwa ugonjwa huo katika nchi 143. Tayari nchi 24 barani Afrika zimeripoti kuwa na watu wenye maambukizo ya virusi hivyo.

* **Epuka mikusanyiko ya watu isiyo lazima**
* **Nawa mikono kwa maji yanayotiririka kwa sabuni kila mara**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## KIKONGWE AFA KWA KUBAKWA AKIENDA KANISANI

UKURASA 7

# Chadema yatangaza kuanza mikutano Tanzania nzima

UKURASA 5



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** MIRAJI ATOA MATUMAINI KUREJEA TENA SIMBA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Mgonjwa wa kwanza aripotiwa Tanzania

**Na Waandishi Wetu**

TANZANIA imethibitisha kuwapo kwa mgonjwa wa kwanza wa corona, huku serikali ikiwataka wananchi kuchukua tahadhari kuhusu mlipuko wa virusi hivyo.

Imeelezwa na serikali kuwa mgonjwa huyo aliingia nchini juzi kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji.

Akitangaza taarifa hiyo jana mbele ya waandishi wa habari, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema mama huyo wa kitanzania alikuwa amesafiri kwenda Ubelgiji.

"Machi 15 (Jumapili), tulipokea msafiri Mtanzania mwanamke (46), ambaye aliwasili nchini na ndege ya Rwanda Air akitokea Ubelgiji. Msafiri huyu aliondoka nchini Machi 3 mwaka huu na kati ya Machi 5 na 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena nchini humo na baada ya hapo kurejea Tanzania," alisema.

"Msafiri huyu alipita KIA akafanyiwa ukaguzi na kuonekana kutokuwa na homa. Baadaye alianza kujisikia vibaya akiwa hotelini na kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mt. Meru ambako alichukuliwa sampuli na kupelekwa Maabara ya Taifa ya Afya iliyoko jijini Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi.

"Vipimo vya maabara vimethibitisha kuwa mtu huyu ana maambukizo ya ugonjwa wa corona (COVID-19) na anaendelea vizuri," alisema.

Waziri huyo aliwatoa hofu wananchi kwamba tayari serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa usisambae nchini ikiwamo kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na wadau wengine katika kuendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana nao.

Alisema tayari amepigiwa simu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ambaye amemwambia kwa kuanzia watapewa Sh. milioni 500 ili kusaidia kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema tayari wametenga maeneo kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa watakaobainika kuwa na maambukizo ya ugonjwa huo.

"Maeneo tuliyotenga kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa ni Dar es Salaam (Mloganzila), Kilimanjaro na Arusha (Mawenzi) na Mwanza (Buswelu)," alisema na kubainisha kuwa wameelekeza kila mkoa na halmashauri kutenga au kuchagua kituo cha kutolea huduma kwa wagonjwa.

"Niwatoe hofu wananchi kwamba hata hapo Mawenzi tulipotenga siyo ndani ya hospitali kabisa, ni nje, hata Mloganzila ni nje siyo hospitali kabisa," alisema.

Mwalimu alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitarajiwa kukutana kwenye kikao cha dharura na mawaziri 12 ili kutafuta njia mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo.

"Tunaamini kwamba kwa sababu mgonjwa ni yule wa kuja siyo wa kutoka ndani ya nchi, tutadhibiti," alisema na kubainisha kuwa amezungumza na mgonjwa huyo kwa zaidi ya dakika 15.

"Asilimia 70 ya wagonjwa wanakuwa na dalili ambazo siyo kali sana, ni watu ambao wanaweza kuongea, hata huyu mgonjwa wetu nimezungumza naye kwa simu kwa zaidi ya dakika 15 ameniambia alivyoingia nchini.

"Ukimsikiliza mgonjwa maelezo yake hata kabla ya vipimo, alipokuwa Ubelgiji, nyumba aliyofikia mume wa mwenyeji wake walikutwa na maambukizo ya ugonjwa huyo, kwa hiyo alivyokohoa, alianza kujishuku na ndiyo maana alivyofika uwanja wa ndege, hakuenda nyumbani kwake, alienda sehemu akajifungia," alisema.

Aliwataka wananchi kuepuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana, kugusa pua, mdomo na macho ikiwa ni hatua mojawapo muhimu ya kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo.

Awali jana asubuhi, Mwalimu alisema Tanzania ipo hatarini kupata ugonjwa huo kutokana na kupakana na nchi ambazo zimeshapata maambukizo.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), hadi juzi, tayari watu 5,737 walikuwa wameshapoteza maisha duniani kutokana na virusi hivyo.

Alisema WHO pia iliripoti watu 153,517 wanaugua ugonjwa huo na nchi 143 zilikuwa zimeshapata kesi za kuwa na wagonjwa zikiwamo 24 kati ya 54 za Afrika.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Mary Geofrey***



# JPM asitisha mbio za Mwenge

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amezisimamisha mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu, kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Aidha, ameelekeza kwamba fedha ambazo zilizotengwa kwa ajili ya mbio hizo, zitumike kwa ajili ya maandalizi ya kukabiliana na tishio hilo.

Akizungumza wa wananchi wa Kibamba jijini Dar es Salaam jana, Rais Magufuli ambaye alikuwa akielekea mkoani Morogoro, alisema mbio za Mwenge ambao ulitarajiwa kuwashwa hivi karibuni visiwani Zanzibar kwa ajili ya kuanza kukimbizwa nchini.

"Kwa mamlaka niliyonayo, Mwenge hautakimbizwa mpaka ugonjwa huu utakapokoma na kuhakikisha haupo, kwa sababu tukiukimbiza unakusanya watu wengi," alisema na kuendelea:

"Maana yake kila mkoa badala ya Mwenge kuwasha amani na matumaini unageuka kuwa Mwenge wa kuhatarisha maisha ya watu."

Rais Magufuli alisema amezungumza na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwamba hautawashwa mpaka wahakikishe ugonjwa huo umeisha.

"Fedha ambazo zilipangwa kwa ajili ya kukimbiza Mwenge, zipelekwe Wizara ya Afya kwa ajili ya maandalizi ya wagonjwa watakaopatikana na corona. Zikasaidie kuokoa mioyo ya Watanzania, Mwenge utakaa hivyo hivyo, sisi tunataka maisha ya Watanzania.

"Kama hatua za corona zikiisha kabisa tutaamua kukimbiza hata kwa siku tatu, kwa sasa hakuna kukimbizwa wala kuwasha Mwenge," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema ameshatoa maelekezo kwa Waziri Mkuu ili fedha za Mwenge zikatumike kuboresha na kupambana na corona.

"Nimeamua mbio za Mwenge mwaka huu kuzisimamisha kwa sababu pakitokea mtu mmoja ameushika Mwenge na ana virusi vya corona maana yake Tanzania nzima tutakuwa na corona na Mwenge pia huwa kunakuwa na mikusanyiko, maana yake tutapoteza maisha," alisema.

"Ninawaomba madhehebu mbalimbali, Waislamu na Wakristo mwendelee kumuomba Mungu atuepushe na janga hili, limeshaingia nchi ya jirani lazima tujiandae, lakini tusibweteke tuchukue tahadhari."

**WIKI YA MAJI YAFUTWA**

Wizara ya Maji, imefuta shughuli za wiki ya maji mwaka huu ili kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano cha wizara hiyo kwa vyombo vya habari jana, ilisema mikutano hiyo ambayo ilikuwa ifanyike imefutwa.

"Wizara ya Maji imefuta shughuli zote zilizokuwa zifanyike kueleka Siku ya Maji Duniani na hafla ya uzinduzi wa miradi ya maji," alisema.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID (ITB)**

**ESTABLISHMENT OF LOCAL FRAME AGREEMENTS FOR SUPPLY AND DELIVERY OF ASSORTED NON-FOOD ITEMS**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers and manufacturers to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply and delivery of any or all of the below listed Non-Food Items.

**2. Requirement:**

| TENDER REFERENCE NUMBER | TENDER ITEM DESCRIPTION |
|---|---|
| ITB/2020/SUP/006 | Plastic Jerry Cans |
| ITB/2020/SUP/008 | Sanitary Napkins (Re-Usable Pads) |
| ITB/2020/SUP/009 | Sleeping Mats |
| ITB/2020/SUP/010 | Kitchen Sets |
| ITB/2020/SUP/011 | Solar Lamps |
| ITB/2020/SUP/012 | Mosquito Nets |

**3. Eligibility:**

Manufacturers, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - **Dar es Salaam**

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49, **Kibondo**

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - **Kasulu, Kigoma**

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – **Mwanza**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| **Deadline for receiving requests for clarification** | **Monday 23rd March 2020 at 16.00 hours EAT** |
| **Deadline for submission of offers** | **Wednesday 08th April 2020 16.00 hours EAT** |

***UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.***

215664402


# KANISA LA TAG KUFANYA MAOMBI

**Na Peter Mkwavila, DODOMA.**

KANISA la Tanzania Assemblies of God (TAG) Buigiri Mission, linatarajia kufanya maombi ya siku 40 kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Sherehe wa siku ya Wanawake Watumishi wa Kikristo (WWK), Mchungaji Jackson Ndama alisema kuwa kanisa limechukua hatua hiyo kutokana na tishio la ugonjwa huo na watafunga na kuomba kwa siku 40.

"Tunaomba Mungu atuepushe na janga hili mbalo tayari tumesikia Mataifa mengine yamepoteza watu kutokana na Corona," alisema.

Alitoa wito kwa madhehebu mengine kufanya maombi kwa ajili ya ugonjwa huo ili kuwanusuru Watanzania na ugonjwa huo.

HABARI KITAIFA



Rais Dk. John Magufuli akiwa pamoja na mke wake, Mama Janeth Magufuli wakimsikiliza Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale (wa pili kushoto), wakati akielezea maendeleo ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri Mpango aeleza athari corona kiuchumi

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**


WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameelezea madhara ya kiuchumi kutokana na ugonjwa wa corona.

Kutokana na hali hiyo, amewaagiza wataalamu wa wizara hiyo kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kuangalia madhara ya corona yanayoweza kujitokeza katika uchumi wa nchi pamoja na namna ya kukabiliana nayo.

Akitoa agizo hilo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na watumishi wa wizara hiyo kuhusu umuhimu wa kujikinga na virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa hatari wa COVID-19.

"Nilikuwa naangalia taarifa ya Tume ya Uchumi ya Afrika 'Economic Commission of Africa' inayoelezea madhara ya ugonjwa wa COVID 19 unaosababishwa na virusi vya corona, kwa kweli inatisha, wanasema uchumi wa Afrika unaweza ukaanguka na kufikia asilimia 1.8, wastani huwa ni asilimia 3.2," alisema Dk. Mpango.

Dk. Mpango alisema ugonjwa huo ni hatari ni vyema taifa liandaliwe upande wa uchumi ili kujiweka sawa na kutafuta namna ya kuchukua hatua katika kukabiliana na madhara yanayoweza kutokea kiuchumi hususani kwenye biashara na utalii.



Aliwataka watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo kwa kuzingatia taratibu za afya katika maeneo ya kazi na kwenye familia zao.

"Kila mmoja ana wajibu binafsi, wajibu katika familia na wajibu kazini ili tuendelee kukaa salama. Sitapenda kupoteza mtumishi hata mmoja wala mtumishi kupoteza mwanafamilia wake kutokana na ugonjwa huu," alisema Dk. Mpango.

Aliwaasa watumishi kuchukua tahadhari kwa kuiga mfano wa Rais John Magufuli wa kuacha mazoea ya kushikana mikono wakati wa kusalimiana.

"Kiafrika unaonekana unaringa kweli usipompa mtu mkono, lakini kwa dharura tuliyonayo, muwafundishe na watoto wenu hakuna kupeana mikono," alisisitiza Dk. Mpango.

Alifafanua kuwa katika kupambana na ugonjwa huo, wizara imeweka kemikali maalumu ya kunawia mikono (sanitizer) inayoweza kuua vijijidudu kwenye maeneo mbalimbali ya majengo ya wizara hiyo na kuwataka watumishi wahakikishe wanaitumia wakati wanapoingia ofisini na kwa wenye uwezo wainunue kwa ajili ya matumizi ya familia zao.

Aliwataka watumishi hao kutoa elimu ya afya kwa familia zao pamoja na kuepuka mikusanyiko na safari zisizokuwa za lazima za ndani na nje ya nchi ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema ugonjwa huo ni kama vita na kwa kuwa umeshafika katika nchi jirani za Kenya na Rwanda, hata hivyo alisema, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Wizara ya Afya, Tanzania iko salama.

# Muhimbili yachukua hatua za udhibiti

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa kushirikiana na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JCKI) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas), imeanza kuchukua hatua mbalimbali za tahadhari ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya Covid 19 vinavyosababisha homa ya Corona ambao ushaingia nchini.

**"Uongozi wa taasisi hizi umekubaliana kwa kauli moja kuwa kuanzia sasa wataruhusiwa ndugu wawili tu kwa kila mgonjwa mmoja wakati wa asubuhi na jioni na kwamba mchana ni mtu mmoja tu atakayeruhusiwa kupeleka chakula kwa mgonjwa ili kupunguza msongamano mkubwa ulioko eneo la Muhimbili," alisema Aligaesha.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kwa niaba ya taasisi hizo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, alisema hatua hizo ni pamoja na kuwataka wafanyakazi, ndugu na jamaa wa wagonjwa wote wanaoingia eneo la Muhimbili kunawa mikono kwa kutumia maji yenye dawa yaliyowekwa katika maeneo mbalimbali ya taasisi hizo kabla na baada ya kuingia ndani ya hospitali, wodini na sehemu za kutolea huduma.

Taasisi hizo, alisema pia zimeunda kikosi kazi kinachoratibu hatua za tahadhari dhidi ya Corona ambacho kinatoa mafunzo kwa wafanyakazi wote wa taasisi hizo, wanafunzi na kutoa mafunzo kwa wakufunzi (ToT) watakaosaidia kuelimisha umma kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Uongozi wa taasisi hizi umekubaliana kwa kauli moja kuwa kuanzia sasa wataruhusiwa ndugu wawili tu kwa kila mgonjwa mmoja wakati wa asubuhi na jioni na kwamba mchana ni mtu mmoja tu atakayeruhusiwa kupeleka chakula kwa mgonjwa ili kupunguza msongamano mkubwa ulioko eneo la Muhimbili," alisema Aligaesha.

Aliwataka Watanzania kuunga mkono hatua hizo ili kuongeza tahadhari dhidi ya ugonjwa huo ambao ushaingia nchini.

Kutokana na tahadhari hizo zilizoanza kuchukuliwa hospitalini hapo, wananchi waliokuwa wamekwenda jana kutembelea wagonjwa wao, walianza kukutana na changamoto ya msongamano mkubwa wa kupata huduma ya kusafisha mikono.

Aidha, watu waliokuwa wanaenda kwa makundi kuwaona wagonjwa walilazimika kurudi nyumbani na kubaki ndugu mmoja.



# Chupa za chai zatumika kuuza pombe za viroba

## ▪ Madaktari bingwa waonya walevi
## ▪ Wizara, mamlaka zaanika mikakati



IGP, Sirro

**Na Mary Geofrey**

***SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilibainisha namna wauzaji wa pombe kali zisizothibishwa na Shirika la Viwango (TBS), wanavyotumia mbinu mbalimbali kutoa huduma kwa wateja wao pasi na kunaswa na vyombo vya dola. Endelea na sehemu ya mwisho kujua madhara ya utaratibu huo na mustakabali wake:***

---

Kwa upande wake, Daktari wa Macho wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, Dk. Catherine Makunja, aliiambia Nipashe kuwa hatari kwa watumiaji wakubwa wa viroba ni pamoja na mbinu za kuuzwa kwake zinazotia shaka juu ya ubora wa pombe hizo, usafi wa chupa na glasi zinazotumika na usindikaji wa pombe hizo ambao huwa ni wa kienyeji.

"Jambo hili ni sawa na mtu anatengeneza gongo na kuifungasha kwenye chupa au maji ya bombani ukayaweka kwenye chupa halafu ukawauzia watu. Hili jambo ni haramu na pia ni kinyume cha sheria," alisema.

Dk. Makunja alisema mtu anayekunywa pombe za aina hiyo, anakuwa katika hatari ya kupata matatizo ya presha ya macho ambayo mbali na unywaji wa pombe, husababishwa na mtu kuwa na umri mkubwa wa kuanzia miaka 40, magonjwa ya kurithi katika familia, kisukari, uvutaji sigara na matumizi holela ya dawa.

Alisema wanywaji pombe kupita kiasi hasa ambazo hazijapimwa na kuthibitishwa na mamlaka husika, wako hatarini zaidi kwa sababu madhara yaliyo kwenye pombe hizo ni mengi kuliko zile zilizothibitishwa.

"Kama nilivyoeleza, mtu anayekunywa pombe kupita kiasi, atakuwa hatarini kupata presha ya macho na hao wanaokunywa pombe kiholela ambazo hazijapimwa, ni hatari kwao na wanaweza kuwa na tatizo hili bila wao kufahamu," alisema.

Daktari Bingwa wa Figo wa MNH, Dk. Onesmo Kisanga, pia aliuhusisha unywaji wa pombe za aina hiyo na visababisho vikuu vya magonjwa ya figo, akivitaja vingine kuwa ni pamoja na uzito kupindukia, kisukari, matumizi makubwa ya sigara na kutokufanya mazoezi.

Alisema unywaji wa pombe unaathiri figo na kusababisha kushindwa kufanya kazi ya kuchukua taka vizuri na hatimaye kufa kabisa kwa sababu siyo rahisi kwa mgonjwa kutambua ana tatizo hilo haraka kama ni mnywaji wa pombe kupita kiasi.

"Magonjwa haya yakitambuliwa mapema, yanaweza kudhibitiwa kwa matibabu na kuepusha madhara kwenye figo. Ili kutambua magonjwa haya, ni vizuri watu wote wawe na tabia ya kupima afya zao mara kwa mara. Magonjwa haya pia huweza kukingwa na ufanyaji wa mazoezi," alisema.

Alibainisha kuwa asilimia 10 ya watu duniani wanasumbuliwa na magonjwa ya figo na kila mwaka, watu milioni 2.4 hufariki dunia kutokana na magonjwa ya figo, yanayoshika nafasi ya sita katika orodha magonjwa yanayochangia idadi kubwa ya vifo duniani.

Kwa Tanzania, Dk. Kisanga alinukuu takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2011 zinazobainisha kuwa Watanzania wapatao 4,300 hufariki kila mwaka kutokana na magonjwa ya figo.

**TBS, FCC**

Akizungumzia mbinu mpya zinazotumika kuuza pombe hizo, Mkuu wa Kitendo cha Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, alisema wanaofanya hivyo hawana tofauti na anayezalisha bidhaa bandia na kwa kuwa mazingira ya ufungashaji siyo rasmi, pombe hizo zinaleta madhara makubwa kwa watumiaji.

"Serikali kupitia vyombo vyake inaendelea kuwasaka wauzaji na wanaobainika, wanachukuliwa hatua kali," Andusamile alisema.

Ofisa huyo wa TBS alisema shirika limekuwa likifanya ukaguzi wa mara kwa mara kukabiliana na bidhaa zisizo na ubora zinazoingia sokoni.

Alikiri ukaguzi wao katika maduka na baa wamekuwa kukamata pombe kali ambazo ubora wake haujathibitishwa na mamlaka, hivyo kuwakamata wahusika kuziteketeza bidhaa.

Hata hivyo, Andusamile alisema vikwazo vinavyolikabili shirika katika jitihada zake za kukabiliana na biashara haramu kuwa ni pamoja na uhaba wa watumishi.

Alibainisha kuwa shirika kwa sasa lina watumishi 500, akisema hawatoshi kupita kwenye vichochoro vyote nchini na kubaini au kuwakamata wauzaji wa pombe zisizo na viwango, hivyo kuna haja wananchi kusaidia kutoa taarifa za wahalifu.

"Tunashirikiana na jamii, tunategemea kupata taarifa kama hizo kutoka kwao ndiyo sababu tumetoa namba ya simu ya kupiga bure ambayo ni 0800110827, watu wanapoona pombe za aina hiyo zinauzwa kiholela mitaani, watupe taarifa ili tuzifuatilie na kuchukua hatua," aliomba.

> **"Kama nilivyoeleza, mtu anayekunywa pombe kupita kiasi, atakuwa hatarini kupata presha ya macho na hao wanaokunywa pombe kiholela ambazo hazijapimwa, ni hatari kwao na wanaweza kuwa na tatizo hili bila wao kufahamu," alisema.**

Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Tume ya Ushindani (FCC), Frank Mdimi, alisema tume hiyo inatekeleza Sheria ya Alama za Bidhaa kuwashughulikia wanaotumia bidhaa na nembo za kibiashara za watu wengine, kuuza bidhaa feki.

Alisema inapobainika kuwapo kwa kosa, adhabu hotolewa kwa mujibu wa sheria, akibainisha kuwa FCC ikimkamata mtu na akakutwa na hatia, kosa lake huwa ni la jinai na adhabu huwa ni kifungo cha kuanzia miaka minne hadi 15 gerezani au faini ya kuanzia Sh. milioni 10 hadi 50 au adhabu zote mbili.

**HATUA ZA POLISI**

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, aliambia Nipashe kuwa wamekuwa wakichukua hatua mbalimbali dhidi ya wanaojihusisha na biashara hiyo kwa kuwakamata na kuwafikisha mahakamani.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (kuanzia mwaka 2017 hadi 2019), jeshi hilo lilikuwa na kesi 18,933 za biashara ya pombe haramu aina ya gongo, zilizohusisha watuhumiwa wanaume 24,554 na wanawake 10,574.

Alisema kati yao, wapo ambao sasa wanatumikia vifungo gerezani na wengine walitozwa faini baada ya kupatikana na hatia ya kujihusisha na biashara hiyo.

Alisema utengenezaji wa gongo na pombe kali zisizothibitishwa na mamlaka za nchi, ni kosa kisheria na Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua dhidi ya watu wanaojihusisha na uhalifu huo.

"Tumekuwa tukishirikiana na viongozi wa serikali za mitaa na wananchi kupitia kamati za ulinzi na usalama za maeneo yao kuwapata wahalifu na kupata njia za kuzuia utengenezaji wa pombe haramu," alisema.

**KAULI YA WIZARA**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Gerald Chami, alisema suala la unywaji wa pombe kali na uuzwaji wake wa kiholela ni tatizo katika jamii kwa kuwa limekuwa likisababisha madhara makubwa kiafya.

Alisema nchi sasa inakabiliwa na magonjwa ya figo, ini na saratani, ambayo moja ya visababisho vyake ni unywaji wa pombe kupita kiasi na pombe kali zisizo na ubora.

Chami alisema wizara yao kwa kushirikiana na mamlaka za kisheria, imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya pombe hizo na kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka sheria na miongozo iliyowekwa.

"Elimu inahitajika zaidi, tuendelee kuelimisha jamii kujali afya zao na kutumia pombe kwa wastani na kuachana na matumizi ya pombe kali ambazo ubora wake unatia shaka, hasa wakati huu ambao kuna mlipuko wa ugonjwa wa corona katika nchi mbalimbali duniani, ni muhimu Watanzania wakaacha upotoshaji.

"Kuna watu wanadanganyana ukinywa pombe unajizuia kupata corona, tuache kudanganyana, pombe zina madhara na siyo tiba ya corona," alionya.

# Chadema yatangaza kuanza mikutano Tanzania nzima

Na Enock Charles

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza kuanza mikutano ya hadhara kuanzia Aprili 4, mwaka huu kwa ajili ya kudai tume huru ya uchaguzi.

Akizungumza na wana habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, alisema lengo pia ni kufanya maandalizi ya uchaguzi mkuu mwaka huu.

Aidha, aliwatangazia viongozi wote wa Chadema katika mikoa na wilaya kuanza kufanya mikutano hiyo licha ya kupigwa marufuku na serikali tangu mwaka 2016 na kwamba hawatahitaji kibali kufanya mikutano hio kwa kile alichodai ni haki yao ya kikatiba.

"Kuanzia Aprili 4, mwaka huu hatutasubiri kibali cha mtu yeyote tutaanza mikutano nchi nzima na kwa kauli hii na watangazia viongozi wote wa Chadema tuanze kufanya mikutano ya hadhara tukidai vitu viwili tume huru ya uchaguzi na maandalizi ya uchaguzi," alisema Mbowe.

Alisema hatua yake ya kwenda Mwanza katika maadhimisho ya Uhuru wa Tanzania Bara, ambazo mgeni rasmi alikuwa Rais John Magufuli, lengo lake lilikuwa kufanyika kwa maridhiano ya kitaifa kati ya vyama vya siasa na wadau wengine wa siasa, na ndio sababu ya kumwandikia barua ya kuomba kukutana nae, lakini ameshangazwa na kutokujibiwa kwa barua yao hadi sasa.

Kwa mujibu wa Mbowe, kuomba maridhiano kati ya wadau wa siasa na Serikali sio dalili ya uoga bali ni kutaka amani katika nchi.

**ALAANI KIPIGO**

Aidha, Mwenyekiti huyo alilaani kitendo cha kupigwa na askari Magereza kwa wabunge wanawake wa Chadema ambao ni Mbunge wa Kawe na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya walipokwenda kumfuata magereza Ijumaa alipoachiwa, na kwamba kilichofanywa na askari Magereza ni kinyume cha sheria za nchi .

**AMTUMIA SALAMU DPP**

Aidha, aliitaka ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kufanya kazi kwa maslahi ya umma, na kwamba amekuwa ikitumika vibaya kuwatisha wabunge wa chama hicho, na kwamba akisimama upande mmoja na kufanya maamuzi ya upendeleo ni jambo baya.

Wiki iliyopita DPP, Biswalo Mganga, akizungumza na waandishi wa habari, alisema atamchukulia hatua Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, kwa kile alichosema ni kusambaza taarifa za uongo kuhusu mauaji ya watu 14 wilayani Manyoni mkoani Singida.

# JPM asimamisha wahandisi

Na Idda Mushi, MOROGORO

RAIS John Magufuli amewasimamisha kazi wahandisi 12 katika ofisi ya Wakala wa Barabara (Tanroads) mkoa wa Morogoro, akiwamo Kaimu Meneja aliyehamishiwa makao makuu kwa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wiki iliyopita.

Aidha, Rais ametoa onyo la mwisho kwa viongozi wa juu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, akiwamo Waziri wake Isack Kamwelwe, na Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Mhandisi Patrick Mfugale.

Mwingine aliyesimamishwa ni Mkurugenzi wa Matengenezo wa Wakala huo, Mhandisi Mohamed Ntunda, kutokana na madai ya uzembe uliosababisha kukatika kwa daraja la Kiegeya huku siku 14 zikimalizika bila kukamilika.

Rais alitangaza uamuzi huo baada ya kutembelea mara ya kwanza eneo linapojengwa daraja la Mkange Kiegeya lililokatika na kuzolewa na maji Machi 2, mwaka huu.

Alisema Mhandisi Ntunda asimamishwe kazi kutokana na kushindwa kufanya ukaguzi wa zaidi ya Sh. bilioni tatu alizoidhinisha ziende mkoani Morogoro kwa ajili ya ukaguzi na matengenezo ya barabara na madaraja.

Kabla ya kufikia uamuzi huo, aliwabana kwa maswali viongozi hao na kueleza wengi hawakutimiza wajibu wao akiwamo Kaimu Meneja wa Mkoa.

"Toka tarehe 2 hadi leo (jana) tarehe 16 daraja halipitiki ikizingatiwa njia hii ni muhimu kiuchumi, kitaifa na kimataifa, inaunganisha Tanzania na nchi zingine zikiwamo za DR Congo, Rwanda, sehemu ya Kenya na nchi zingine nyingi. Nimekuja hapa sijamweleza yeyote, Waziri nilikwambia nakuja? Mkuu wa Mkoa? Nia yangu ilikuwa nifike mwenyewe kuona adha wanayoipata wananchi. Kama wameshindwa kuvuka na mie nishindwe kupita, nikwame, muamue kama mngenibeba au mfanyeje ili niendelee na safari," alisema Magufuli.

Alisema kuna zaidi ya wahandisi 25,000 nchi nzima ambao wamesajiliwa na wako tayari wakati wowote kufanya kazi ingawa kwa sasa hawana kazi na kwamba kuondoka kwa wahandisi hao hakuwezi kusababisha athari yoyote kiutendaji.

Aidha, Rais Magufuli alimwagiza Waziri Kamwelwe kumwandikia barua ya kumfuta kazi meneja yeyote wa Tanroads mkoa ambaye katika mkoa wake kutakatika daraja na barabara kushindwa kupitika. Alisema serikali imekuwa ikitoa mamilioni ya fedha kwa kazi za ukaguzi na matengenezo ya muda mfupi na mrefu lakini wengine wanashindwa kutumia fedha hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alieleza hatua walizochukua tangu kukatika kwa daraja la Kiegeya na Rais akaitaka kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kutohangaika kwenda tena eneo la ujenzi badala yake wawaachie wataalamu na kuelekeza daraja na barabara hiyo ipitike vyema ndani ya siku saba kuanzia jana.

Awali, Rais Magufuli alitembea kandokando ya Mto Kiegeya kwa miguu na kubaini sehemu aliyosema ni rafiki kufungwa daraja kwa kutumia muda mfupi na gharama nafuu kutokana na kuwa kwa upana mdogo na mawe ya kutosha.

Aidha, alipingana na uamuzi uliotolewa na Waziri Mkuu wa kupeleka wanajeshi kuongeza nguvu katika eneo hilo kwa madai kuwa kazi hiyo ina uwezo wa kufanywa na watumishi wa Wizara ya Ujenzi.

"Mkitaka wanajeshi nitamwondoa waziri naye nimuweke mwanajeshi, nitamwondoa Katibu Mkuu nimweke mwanajeshi. Nitamwondoa Mtendaji Mkuu wa Tanroads nimweke mwanajeshi hadi mfagiaji, sishindwi," alisema.


**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

SIMU NA : 027-2530022
2530042
NUKUSHI NA
: 027/2530022
: 027/2530042

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG,
MANYARA.

*02/03/2020*

## TANGAZO LA KUKODISHA MASHINE YA KUSAGA NA KUSINDIKA NAFAKA

## ZABUNI NA. LGA/059/HQ/2019/2020/NC/10

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa mashine ya kusaga na kusindika nafaka.

Mashine ipo katika Soko la Kimataifa lililoko Kata ya Endagaw Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara.

Mashine ina uwezo wa kusaga na kusindika hadi tani kumi (10) kwa siku

**MASHARTI YA ZABUNI YA KUKODISHA MASHINE**

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Mhasibu wa Mapato Halmashauri ambayo haitarudishwa hata kama mwombaji wa Zabuni hatateuliwa. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni "Tender Document" na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe16/03/2020 hadi tarehe O3/04/2020.
2. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa mwaka moja tu.
3. Mwombai wa Zabuni anatakiwa ataje bei ya kukodisha mashine ya kusaga na kusindika kwa mwaka mmoja.
4. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kuwa na Leseni ya Biashara ya kusaga na kusindika nafaka na pia atatakiwa kulipia "Subsidiary Licence" kwa Halmashauri ya (W) ya Hanang', atatakiwa kulipa ushuru wa huduma (Service Levy) na awe na risiti ya mashine –"Electronic Fiscal Device" (EFD).
5. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atapaswa kutunza mashine na kuikabidhi kwa Halmashauri ikiwa katika hali nzuri.
6. Mwombaji wa Zabuni atahusika na uharibifu au hasara yoyote itakayojitokeza katika utumiaji na utunzaji wa mashine hiyo wakati ikiwa ndani ya muda wa mkataba.
7. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa mashine ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa.
8. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kulipa gharama zote za umeme na maji katika utumiaji wa mashine atakayokodishiwa.
9. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.

**Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:**
**KATIBU WA BODI YA ZABUNI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,**
**S.L.P 2,**
**KATESH – HANANG.**

Juu ya bahasha iandikwe **ZABUNI YA UKODISHAJI MASHINE YA KUSAGA NA KUSINDIKA NAFAKA**

10. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya **Ijumaa tarehe 03/04/2020 saa 5:00 asubuhi** kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.

- **Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.**

**BRYCESON P. KIBASSA**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG`**

NAKALA:
1. Ofisi ya Katibu Tawala Wilaya Hanang'
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni wananchi katika Kata zenu
3. Watendaji wa Vijiji - Wajulisheni wananchi katika Vijiji vyenu.
4. Mbao za Matangazo

115670602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kudhibiti mbinu mpya pombe viroba

KWA siku mbili mfululizo kuanzia jana, Nipashe tunachapisha ripoti maalum kuhusu mbinu mpya za kificho zilizobuniwa na wafanyabiashara kuuza pombe kali zisizokidhi viwango mijini, hasa jijini Dar es Salaam.

Ripoti hiyo ambayo ni matokeo ya uchunguzi wa miezi minne jijini Dar es Salaam, inabainisha kuwa wapigadebe, madereva, makondakta, wamebeba mizigo, waendesha maguta na wafanyabiashara ndogondogo, maarufu machinga, ndiyo wateja wakubwa wa pombe hizo.

Ndani ya mtazamo huo, kuna kuibuliwa kwa mbinu mpya za udanganyifu zinazofanywa na wafanyabiashara, pia wachuuzi wa viwanyaji hivyo haramu kuhakikisha walichokuwa wakifanya awali kinaendelea kuwapo, licha ya amri kali ya serikali inayotimua mwaka wa tatu sasa.

Kimsingi, serikali ilipiga marufuku biashara ya kuuza pombe kali kwenye mifuko midogo ya plastiki, maarufu viroba kuanzia Machi Mosi, 2017.

Uchunguzi wetu, hasa jijini Dar es Salaam, umebaini kupamba moto biashara ya vinywaji hivyo haramu, mbinu ya mlango wa pili unaotumiwa sasa ni namna ya ufanyikaji wake ni kificho kipya kinachoendeshwa kupitia ushirikiano wa aina yake kati ya wauzaji na wateja.

Ni nyendo zinazokinzana na agizo zito la marufuku lililotolewa na Mtendaji Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye aliweka bayana kwa watakaothubutu kukiuka, watakutana na mkono wa dola kwa kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Matabibu ambao ndiyo wanaohudumia waathirika wa vinywaji hivyo, wanaungana na Waziri Mkuu wakiwa na lao. Daktari Bingwa wa Macho katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Catherine Makunja, anadokeza walakini wa jumla katika ubora wa vilevi hivyo, usafi wa chupa na glasi zinazotumika, hata usindikaji wake, huku mnywaji akikaribisha kuugua presha ya macho.

Dk. Onesmo Kisanga, bingwa wa tiba ya figo - MNH, pia anavihusisha vilevi hivyo na chanzo cha kuugua figo, ambayo huwa haina mwisho mzuri kwa afya ya binadamu, ikiwamo kifo kama ilivyo kwa presha ya macho.

Kwa kuzingatia mtazamo huo, Nipashe tunaona mamlaka husika za serikali, kila moja kwa nafasi yake, kuchukua hatua stahiki kuzuia biashara hiyo haramu ili kuokoa afya ya wananchi.

Wapigadebe, madereva, makondakta, wamebeba mizigo, waendesha maguta na wafanyabiashara ndogondogo waliotajwa kuzama kwenye utumiaji wa vilevi hivyo ni kundi la vijana ambao ni nguvukazi ya taifa la leo na kesho.


Ni katika uzito huo, Nipashe tunaona mamlaka husika za serikali zinapaswa kuchukua hatua za haraka kukabiliana na wafanyabiashara na wachuuzi wa pombe hizo wenye nia ya kujipatia fedha kwa kuzalisha au kuuza bidhaa zisizokidhi viwango pasi na kujali madhara yake kwa afya za walaji.

Kuna madhara mengi na makubwa yanayoweza kutokea na kuwaathiri watumiaji wa bidhaa hizo, vikiwamo vifo. Hivyo ni matarajio yetu kuona hatua hizo zikianza kuchukuliwa na mamlaka zetu ili kuwabaini wote wanaojihusisha na mchezo huo mchafu.

Ni wakati mwafaka sasa wahusika hususani Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kuanzisha msako wa kuwabaini watu hao kisha kuwafikisha kwenye mkono wa sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Matumizi mitandao yawabadilishe vijana

KATIKA miaka ya hivi karibuni kasi ya matumizi ya teknolojia ya mitandao ya kijamii, imekuwa ni kubwa, lakini ikiwa imegawanyika katika sura mbili, ambazo ni nzuri na mbaya.

Nikianzia na nzuri, kukua kwa matumizi ya mitandao ya kijamii, watu wengi zaidi wanaweza kupata habari na elimu juu ya mambo mbalimbali kirahisi tofauti na enzi hizo.

Kimsingi ongezeko la watumiaji wa mitandao ya kijamii ni jambo zuri kwa maendeleo ya nchi, kwani inasaidia katika upashanaji habari na taarifa muhimu za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Lakini pamoja na faida hizo na nyingine nyingi, jamii imeshuhudia uholela wa matumizi ya mitandao jambo ambalo limeathiri baadhi ya vijana kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao hiyo.

Ni vyema ikaeleweka kuwa mitandao hiyo si tu sehemu ya mawasiliano, bali pia kimaendeleo katika jamii nyingi, hasa kwa vijana, ambao inasemekana wengi ni ndiyo watumia wakubwa.

Hivyo wanatakiwa kuitumia inavyotakiwa, kwani imekuwa ikidaiwa kuwa kuwa wapo baadhi ya vijana wanaoutumia vibaya na kujikuta katika mazingira ya hatari bila wao kujua au wakiwa wanajua.

Mitandao ya kijamii inadaiwa kuchochea vitendo vya ngono miongoni mwa vijana na kuwasababisha kuwa katika hatari ya kuambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwamo hata Ukimwi.

Hii inaelezwa kuwa inatokana na matumizi mabaya, na kwamba iwapo vijana wataitumia mitandao hiyo vizuri, wanaweza kupata manufaa makubwa kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye.

Vijana wanakumbushwa kuwa kuna faida nyingi kutumia mitandao ya kijamii inavyotakiwa, kwa vile ina fursa nyingi ikiwamo kupata nafasi za kujiendeleza kielimu.

Huu ni wito kwa vijana unaotolewa na Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP, Lilian Liundi, wakati akizungumza na wasichana kutoka vyuo mbalimbali vya vijijini Dar es Salaam.

Aidha, anawaambia wanatakiwa kutumia vizuri mitandao ya kijamii ili waweze kujiendeleza kielimu, kupata ajira na hata kufanyabiashara kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye.

Anawakumbusha kuwa wao ni kizazi ambacho kinatakiwa kuwa makini katika matumizi ya mitandao hiyo kwa kutojiingiza kwenye mambo yasiyofaa, ambayo mwisho wa siku ni matatizo.

Kinachosemwa na mkurugenzi huyu ni ukweli kwani kumekuwapo na malalamiko kuhusu matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, ambayo imechangia kuwaharibu baadhi ya vijana.

Yaani ni kwamba umefika wakati mitandao ya kijamii iwe ni faida kwa vijana badala ya hasara, kwa sababu tu ya kutoelewa au kuzembea matumizi ya sahihi yanayotakiwa kuzingatiwa.

Siyo siri kwamba vijana wengi wakiwamo wanafunzi, ndiyo wanaotumia mitandao ya kijamii na inaweza kuwasaidia katika masuala mbalimbali yakiwamo ya elimu, lakini wakienda kinyume wajue kuwa watakwama.

Wakumbuke kuwa mitandao hiyo inaweza kuwasaidia wanafunzi kupata hata ufadhili wa kielimu katika nchi mbalimbali na pia kuunganisha watu wa rika mbalimbali katika kujadili masuala muhimu.

Kimsingi mitandao ya kijamii ni muhimu kwa vijana kwa kuwasaidia kujadili masuala ya maendeleo na ndiyo maana mkurugenzi wa TGNP anasisitiza umuhimu wa kuitumia vizuri ili iwanufaishe.

Vilevile mitandao ya kijamii inawajengea uwezo vijana, inawasaidia kuibua vipawa na vipaji vyao na kuvitumia katika kujiingizia vipato, hivyo umuhimu wa matumizi sahihi ni mkubwa.

Inaelezwa kuwa mitandao yote ya kijamii hutoa maelekezo na makatazo muhimu kwa mtumiaji juu ya mambo ya kuzingatia wakati wa kujiunga lakini baadhi ya watumiaji huwa wanayapuuza.

Badala ya kuitumia kwa mambo ya elimu na maendeleo, wao huitumia kwa mambo yasiyo na dira wala muelekeo na hiyo ndiyo imemuibua Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP na kutoa somo kwa vijana.

Anakumbusha kuwa mitandao hii ya kijamii kama mawasiliano ni maendeleo na kwamba matumizi ya mitandao siyo mabaya ila watumiaji ndiyo wanafanya vitu vibaya na kuharibu lengo la mitandao hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Anusurika kifo kwa tuhuma za kuiba jeneza

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

MKAZI wa Mtaa wa Mpanda Hoteli, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Benad Bazilio, amenusurika kifo baada ya kupata kipigo kutoka kwa wananchi hadi kushindwa kutembea baada ya kukamatwa akidaiwa kuiba machela ya chuma inayotumiwa na waumini wa Kanisa Katoliki kubebea maiti za watoto ambayo alitaka kuiuza kwa Sh. 8,000.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Christina Ibrahimu, alisema tukio hilo la aina yake limetokea jana majira ya saa tano asubuhi.

Alisema kuwa Medadi ambaye anafanya kazi za ulinzi katika maeneo ya watu binafsi alikuwa akiishi kwenye nyumba ya Mwenyekiti wa Kigango cha kanisa hilo.

Kwenye nyumba hiyo aliyopanga ndipo huwa yanahifadhiwa majeneza mawili yanayotumiwa na waumini wa kanisa kwa ajili ya kubebea mili ya waumini ambao hawana uwezo wa kutengeneza sanduku kuwazikia wapendwa wao.

Alisema walipoamka asubuhi kwenye nyumba hiyo walibaini kuwa jeneza moja la chuma la kubebea miili ya watoto limeibiwa.

Taarifa zilifikishwa kwenye ofisi ya mtaa na jitihida za kulitafuta zilianza kwa ushirikiano wa viongozi wa serikali ya mtaa na wananchi.

Alisema wakati wakiwa wanaendelea na msako, Libelatus Nzelani alikutana na mtuhumiwa huyo akiwa amelibeba jeneza hilo.

Nzelani alimuuliza anapeleka wapi ndipo mtuhumiwa huyo alipomjibu kuwa kama analihitaji yuko tayari kumuuzia.

Alipomtaka amtajie bei, alimwambia ampatie Sh. 8,000 hatua iliyofanya Nzelani apige mayowe ya kuomba msaada wa kumkamata mwizi huyo.

Wananchi walifika kwenye eneo hilo na kuanza kumshushia kipigo hadi mtuhumiwa ndipo uongozi wa serikali ya mtaa ulipotoa taarifa kwa jeshi la polisi na kumchukua mtuhumiwa.

Mmoja wa wakazi wa mtaa huo, John Kameme, alisema kuwa hilo ni tukio la pili la watu au mtu kuiba jeneza kwenye kigango hicho. Inadhaniwa kuwa huenda wanaenda kuyatumia katika masuala ya kishirikina ama kuuza kama vyuma chakavu.

# Kikongwe miaka 70 abakwa hadi kufa akienda kanisani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MWANAMKE mwenye umri wa miaka 70 (jina linahifadhiwa), amefariki dunia, baada ya kubakwa na watu wasiojulikana wakati akielekea kanisani majira ya alfajiri.

Akizungumza jana kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema mama huyo alifanyiwa kitendo hicho cha kinyama saa 11:45 asubuhi wakati akielekea Kanisa Katoliki la Bikira Maria msaada wa Kristo lililopo mtaani hapo.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi kuwasaka watu waliomfanyia kitendo hicho.

"Tunashukuru wananchi kwa kutoa ushirikiano, hivyo Jeshi la Polisi linaendelea kusaka wahalifu waliotenda kosa hilo," alisema Muroto.

Akisimulia tukio hilo, Mwenyekiti wa eneo la Area 'A', Joshua Temu, alisema alipokea simu kuwa kuna mtu amelala kwenye majani kwenye eneo la wazi.

"Baada ya kupokea simu hiyo nilitoka nikaenda eneo alilolala mtu huyo na kukuta tayari amefariki, huku akiwa amevuliwa nguo za ndani zikiwa pembeni na Biblia yake," alisema.

Aliomba Jeshi la Polisi kufanya msako mkali kwenye eneo hilo ili kukomesha vitendo vya uhalifu ambavyo vimekithiri.

"Inasikitisha kuona vijana wanawaua wazee wa rika hili kwa kuwabaka badala ya kuacha waishi mpaka muda utakapowadia, tumechoshwa kusikia vitendo hivi," alisema.

**"Tunashukuru wananchi kwa kutoa ushirikiano, hivyo Jeshi la Polisi linaendelea kusaka wahalifu waliotenda kosa hilo," alisema Muroto.**

Naye, jirani wa mwanamke huyo, Innocent Lugusi, alisema wamesikitishwa na tukio hilo na kuliomba jeshi hilo kufanya utaratibu wa doria katika eneo hilo.

"Kumekuwa na matukio tofauti ya uhalifu hapa Area 'A' tunaomba Jeshi la Polisi kusaidiana na wananchi kuwasaka wahalifu," alisema Lugusi.

Alisema wakazi wa mtaa huo wanajipanga kuanzisha ulinzi shirikishi kwa ajili ya kujilinda katika eneo hilo.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Jatu PLC, Peter Isare (wa pili kushoto) pamoja na viongozi wengine wa kampuni hiyo, kwenye usiku wa Jatu Super Dinner iliyolenga kutambulisha uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi afa maji akifua nguo mtoni

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MWANAFUNZI wa darasa la tatu Shule ya Msingi Kianda Igonda, wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, Jenifer Kipeta (13) amekufa maji katika mto akiwa anafua sare za shule.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alisema tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita wakati mwanafunzi huyo alipokwenda kufua sare za shule kwa ajili ya kuzivaa jana siku ya Jumatatu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Kamanda, baada mwanafunzi huyo kufika mtoni na kuanza kufua nguo hizo, ghafla kulitokea maporomoko ya maji yaliyosababisha mafuriko makubwa yaliyomsomba mwanafunzi huyo.

Chanzo cha maporomoko hayo ni mvua kubwa iliyonyesha katika vijiji vya mbali na Kijiji cha Kaianda Igonda, ambayo yalisababisha madhara mbalimbali, ikiwamo kifo cha mwanafunzi huyo.

Kamanda Masejo alitoa wito kwa wazazi mkoani humo kuwalinda watoto wao katika nyakati hizi za mvua kwa kuwa ni hatari kwa usalama wa watoto hao.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA (MARUDIO)

**MAENDELEO BANK PLC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapa chini, walipe madeni wanayodaiwa. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zao kwa mnada wa hadhara.

Mnada utafanyika tarehe husika kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea.

| S/N | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA | KAMPUNI YA UDALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Getrude David Kalenga | Nyumba ya makazi yenye hati no.110040 kiwanja no.166,kitalu no.12 eneo la kibada Manispaa ya Temeke. | 04/04/2020. | Best group(T) Limited |
| 2 | Joseph Francis Nayinda | Nyumba ya Makazi yenye hati ya mahuziano iliyopo eneo la Kwembe Manispaa ya Ubungo | 09/04/2020. | Best group(T) Limited |
| 3 | Yusuph Hamis Kitumbo. | Gari aina ya YUTONG zenye namba za usajiri T 435 CVL na T 433 CVL | 04/04/2020.(sahihisho la Tangazo lililopita) | Best group(T) Limited |
| 4 | In the rise canteen/Milton Loth Shango. | Nyumba yenye hati no 70135,kiwanja no.53,kitalu no.9 iliyopo eneo la Bunju manispaa ya Kinondoni | 18/04/2020.(sahihisho la Tangazo lililopita) | Best group(T) Limited |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Nyumba/Mali za Mteja zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakaeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, Kutwaa Nyumba/ Kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku

*KWA MAWASILIANO ZAIDI:*

**MAENDELEO BANK PLC**
**HQ LUTHER HOUSE**
**P.O BOX 216**
**DAR ES SALAAM.**
**MOBILE 0688699289**

**BEST GROUP(T)LIMITED**
**P.O.BOX 1088 DAR ES SALAAM**
**MOBILE 0715363537/0766309913**

215670402

# Mlipuko virusi vya corona wabadili utendaji kazi SADC

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, amesema tishio la kidunia kama vile mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona umeilazimisha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutafuta mbinu mbadala za kiteknolojia kufanya kazi.

Amesema vikao vya SADC kufanikiwa kufanyika kwa njia ya mtandao kuna uwezekano wa mikutano ijayo ya jumuiya hiyo, kuendelea kufanyika kwa teknolojia hiyo endapo kutatokea aina ya janga kama hilo.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa maofisa waandamizi wa SADC kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Fedha, Viwanda ambao watakutana kwa siku mbili kujadiliana agenda nane zitakazowasilishwa kwa mawaziri.

Kanali Ibuge alisema: "Mafanikio ya jaribio hili yanayo nafasi ya kutufanya tuone uwezekano wa kuendelea kufanya mikutano yetu kwa namna hii. Hivyo sote wakati wa mkutano huu ndiyo tutajifunza namna ya kufanya mambo siku za usoni iwapo kutatokea aina hii ya majanga."

Alisema mkutano huo unaendeshwa kwa njia ya mtandao ikiwa ni mara ya kwanza kwa SADC kufanya mkutano mkubwa kwa mfumo huo, ambao ni uthibitisho kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ilivyobadilisha mfumo wa vikao.

"Naomba nitumie fursa hii kuwaomba na kuwasihi nchi wanachama kuendelea kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona na kushikamana kwa umoja wetu kupunguza kasi ya maambukizi na hatimaye kuuondoa kabisa katika sura ya dunia. Kwa pamoja tunaweza," alisema Kanali Ibuge.

Balozi Kanali Ibuge alisema kikao hicho kitajadili agenda umuhimu ambazo ni taarifa ya maandalizi ya Dira ya SADC ya mwaka 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo wa SADC wa mwaka 2020-2030, Maadhimisho ya miaka 40 ya SADC tangu kuanzishwa kwake mwaka 1980, utekelezaji wa maazimio ya vikao vilivyopita, hali ya michango na kifedha kwa ujumla ya SADC, kupokea taarifa ya ukaguzi wa shughuli mbalimbali za sekretarieti ya SADC.



Wahamiaji waliorudishwa kutoka Afrika Kusini kwa tuhuma za kuishi nchini humo bila vibali, wakiwa chini ya ulinzi wa askari kazu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Msako wa 'dadapoa' waanza

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MANISPAA ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imetangaza operesheni maalumu kwa ajili ya kuwasaka, kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria madada poa wanaofanya biashara haramu ya ngono katika mji wa Sumbawanga.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Jacob Mtalitinya, aliyasema alipokuwa akijibu maswali ya waandishi wa habari waliotaka kujua mikakati ya halmashauri hiyo katika kudhibiti kukua kwa kasi biashara ya ukahaba mjini humo.

Alisema kwa mujibu wa sheria, biashara hiyo ni haramu na ni kosa kisheria kuifanya biashara hiyo, hivyo anatoa wito kwa kinadada hao kuacha mara moja badala yake watafute biashara halali.

"Ninachopenda kusema ni kuwa biashara hiyo ni haramu na ninatangaza msako kwa wanaofanya biashara hiyo. Pia ni kinyume cha maadili ya wakazi wa mji wa Sumbawanga... kamwe hatutaifumbia macho, ni lazima tuhakikishe inakomeshwa kabisa," alisema.


TANGAZO KWA UMMA

MATUMIZI MABAYA NA YA UDANGANAYIFU YA JINA LA BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB)

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:

- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Hatutumii anuani za barua-pepe kama vile Gmail, Yahoo Mail n.k.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya barua-pepe: **security@afdb.org.**

215653002

HABARI KITAIFA

# NMB yamwaga misaada elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekabidhi misaada mbalimbali katika sekta za elimu na afya, Kaimu Mkurugenzi wake, Ruth Zaipuna, ameahidi kuendeleza utamaduni huo wa kusaidia utatuzi wa changamoto zinazozunguka jamii kwenye nyanja hizo.

Ijumaa iliyopita, NMB ilikabidhi vifaa tiba kwenye Hospitali ya Wilaya ya Katavi vyenye thamani ya Sh. milioni 8.5, pamoja na mabenchi 25 na viti 25 kwa shule mbalimbali mkoani humo, kama inavyofanya mkoani Ruvuma, ambako inakabidhi vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 15.

Vifaa vinavyotolewa Ijumaa mkoani Ruvuma ni mabati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 2.6 Shule ya Msingi Mlingotini, mabati sawa na hayo kwa Shule ya Msingi Nanjoka, vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 5 na madawati ya Sh. milioni 5 kwa Shule ya Sekondari ya Matemanga.

Akizungumza wakati akikabidhi misaada kama hiyo mkoani Simiyu, alisema utaratibu huo wa kurudisha faida iliyopatikana kwa jamii inayowazunguka kupitia uwajibikaji kwa jamii ni endelezo, lengo likiwa ni kusaidia jamii na kuunga mkono juhudi za serikali.

"Kila mwaka tunatoa asilimia 1 ya faida baada ya kodi na kwa mwaka huu 2020, zaidi ya Sh. bilioni 1 imetengwa ili kusaidia nyanja hizo. Kwa mkoa wa Simiyu pekee, tangu mwaka 2019 tu, tumetoa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 200, iliyosaidia sekta za afya na elimu.

Pia NMB ilitembelea wananchi wa Tarafa ya Mbweri na kukabidhi vifaa vya msaada katika Kituo cha Afya Mbweri, vyenye thamani ya Sh. milioni 5, vikiwamo vitanda vitano vya kulaza wagonjwa, kitanda kimoja cha kujifungulia pamoja na mashuka 60.

Aidha, wajawazito kutoka Kijiji cha Chalowe, Wilaya ya Wanging'ombe mkoa wa Njombe, waliishukuru NMB kwa vifaa vya kisasa vya kujifungulia vilivyotolewa na benki hiyo ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, iliyoadhimishwa Machi 8.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Dk. Lupembe Francis, alipokea msaada huo na kumkabidhi vifaa vya uzazi, Mganga Mfawidhi wa Kijiji cha Chalowe, Niwela Sai, ili kuwasaidia kinamama wajawazito waliokosa usalama kutoka kijijini hapo.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongela, alisema msaada huo umetolewa kwa muda sahihi kuwasaidia kinamama na watoto wanaozaliwa salama tofauti na hatua ilivyokuwa wanaposafirishwa mbali.

Chilongola alikabidhi msaada huo kwa sekondari za Igima na Wanging'ombe, ambazo zilipokea meza 100 na viti 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 15, ambavyo vimegawanywa 50 kwa 50, vikipokelewa kwa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Ally Kassinge na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Eden Lukoa. Kadhalika, benki hiyo NMB ilikabidhi msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa Kituo cha Afya cha Pugu Kajungeni, kilichopo Pugu jijini Dar es Salaam, huku ikikabidhi madawati 50 na viti 50 vyote vyenye thamani ya Sh. milioni 5, kwa Sekondari ya Dk. Olsen, iliyopo Mbulu, mkoani Manyara.

# Bunge lataka ulinzi Ubungo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imeitaka serikali kuhakikisha inaweka ulinzi madhubuti katika miundombinu ya mradi wa barabara za juu (interchange) katika makutano ya eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam ili idumu kwa kipindi kirefu.

Mradi huo wenye lengo la kupunguza msongamano wa magari katika njia za barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma, unagharimu Sh. bilioni 229 huku serikali ikichangia fedha za fidia kwa wananchi waliopisha mradi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Seleman Kakoso, alitoa agizo hilo kamati yake ilipotembelea ujenzi wa mradi huo na kuridhika na hatua ya kazi zilizofikiwa kwa sasa na kumtaka mkandarasi kutimiza malengo kwa mujibu wa mkataba.

"Tunaipongeza serikali, wizara na Tanroads kwa kazi nzuri na usimamizi kwani tumefarijika kuona miundombinu ambayo imejengwa ni mizuri na kazi iliyofikiwa ni nzuri sana, hivyo tuna mategemeo kwamba miundombinu hii itawanufaisha Watanzania," alisema.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, aliihakikishia kamati hiyo kuwa watasimamia utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu bora ya barabara kwa kila fedha inayopitishwa na Bunge kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla.

"Dhamira ya serikali ni kuongeza ubora wa huduma za miundombinu ikiwamo ya barabara na pia kupunguza msongamano katika majiji na hasa Dar es Salaam na sisi wizara tuwahakikishie kuwa tutaendelea kutekeleza miradi kama hii ya Ubungo na maeneo mbalimbali," alisema.

Aliongeza kuwa wananchi wanaopita katika barabara zinazokutana eneo hilo la Ubungo, wamekuwa wakipoteza muda mwingi katika foleni na serikali inapata hasara kubwa kutokana na uzalishaji kupungua, hivyo miundombinu hiyo itakuwa mkombozi kwa taifa.

Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Patrick Mfugale, aliiambia kamati hiyo kuwa barabara za juu katika makutano ya eneo la Ubungo zitadumu kwa miaka 120 na kupunguza msongamano wa magari kwa zaidi ya miaka 50 ijayo ndipo hali hiyo itajirudia tena.

Alisema mpaka sasa ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mapema mwishoni mwa wa Julai mwaka huu.

"Niwatoe hofu wajumbe kuwa mradi utakamilika mapema zaidi, mkandarasi yupo mbele ya muda na changamoto ya msongamano wa magari katika makutano haya itakuwa historia," alisema.



Ofisa uhifadhi msaidizi wa kitengo cha utalii wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane, jijini Mwanza, Alais Mamastia (kushoto), akitoa maelezo kwa wafanyakazi 28 wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Magu, kabla ya kuanza kutalii kwenye hifadhi hiyo, wikiendi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Wadau sekta ubunifu wailila serikali bajeti

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa teknolojia ya ubunifu Tanzania, wameiomba serikali kuongeza bajeti katika sekta hiyo ili kusaidia kupanua wigo wa kazi za kibunifu nchini.

Wakizungumza katika Wiki ya Ubunifu jijini Dar es Salaam, wadau hao walisema bado sekta hiyo imekuwa ikitegemea zaidi ufadhili kutoka katika mashirika ya nje.

Mtaalamu mbobezi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Ernest Salla, alisema kwa sasa sekta ya ubunifu Tanzania imekuwa tofauti na ilivyo kuwa katika miaka ya nyuma na kwamba ili kufanya vizuri zaidi, inatakiwa kushikwa mkono kwa kiwango kikubwa na nchi husika badala ya kuendelea kutegemea msaada kutoka kwa wahisani pekee.

"Kuna wimbi kubwa la vijana kwa sasa hivi ambalo limeona kwamba ubunifu ni fursa, kwa hiyo wengi wao wamevutiwa na wameingia kwa wingi katika sekta hii ya ubunifu, na hata mahitaji katika shughuli za kibunifu yameongezeka, kwa hiyo inabidi waungwe mkono," alisema Salla na kuongeza:

"Kutokana na kukua kwa sekta hii, kunahitajika serikali, sekta binafsi pamoja na wahisani kuungana kusaidia sekta hii badala ya kuachia upande mmoja... kwa sasa sekta hii inahitaji ushirikiano kutoka kwa wadau wote, tunatakiwa kuwa na programu za muda mfupi, kati na muda mrefu za kuipeleka mbele zaidi sekta hii."

Pia Salla alisema ipo haja ya kutenga maeneo maalum ya uwekezaji katika shughuli mbalimbali za ubunifu.

"Naona matokeo mazuri zaidi yanakuja katika sekta hii, vijana wanabuni vitu vizuri ambavyo hatujawahi kuvishuhudia katika siku za nyuma... wanakwenda na teknolojia na ndani ya miaka michache ijayo, Tanzania itakuwa inafanya vitu vikubwa kupitia sekta hii," alisema Salla.

## 'Serikali lazima ikubali kupokea mawazo mapya'

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, amesema serikali na taasisi zake ni lazima wakubali kupokea mawazo mapya ili kuongeza kasi kiutendaji na ikiwezekana kurekebisha sheria zinazowabana wenye fikra hizo mpya.

Manyanya aliyasema hayo juzi usiku katika hafla ya chakula cha jioni kilichoandaliwa na Kampuni ya Jatu PLC inayojishughulisha na miradi ya kilimo, viwanda na masoko baada ya kupata usajili wake wa kudumu Oktoba 20, 2016.

Kampuni hiyo inayoendeshwa na vijana wahitimu wa chuo kikuu, inasimamia miradi mbalimbali ya kilimo kwa kushirikiana na wanachama wake na miongoni mwa miradi iliyonayo ni wa ekari 968 wenye wanachama 112 wilayani Kiteto mkoani Manyara.

Katika hafla hiyo, Manyanya alisema badala ya serikali kujifungia na mambo ya asili, lazima ikubali kuyapokea mawazo mapya kama ya kampuni hiyo na kuyaboresha ili kufikia malengo.

"Hii ni moja ya kampuni iliyojikita kwenye mawazo mapya, zinaweza kuzaliwa kampuni nyingi, lazima vikwazo viondolewe, unakuta mtu anakwenda benki anatakiwa kwanza apeleke dhamana wakati hana, matokeo yake anakata tamaa na mwishowe anaona arudi kwenye ajira ambazo nazo hazitoshi," alisema.

Manyanya aliwatoa hofu Watanzania na kuwataka wathubutu kununua hisa za Jatu PLC ambayo ni kampuni ya wazawa, akisema kuwa kabla ya kukubali mwaliko wao, alijiridhisha kwanza na kubaini siyo wababaishaji.

Pia, aliwataka vijana hao ambao ndiyo waanzilishi wa kampuni hiyo, badala ya kujifungia na mawazo yao, wafungue milango ya kujifunza kupitia taasisi mbalimbali za serikali ili wasonge mbele.

"Nia yenu ni njema na mawazo ni mazuri, lakini kutokana na mambo hayo (kuwa taasisi ya umma) kukaa kisheria zaidi lazima muendane na mifumo ili msimame vizuri," alisema.

Naibu waziri huyo pia aliwataka wataalamu wasaidie kuboresha mawazo ya vijana hao na kuhakikisha vikwazo dhidi yao vinatafutiwa ufumbuzi.

Mkurugenzi Mkuu wa Jatu PLC, Peter Isare, alisema kampuni hiyo imelenga kujenga afya na kutokomeza umaskini nchini.

Alisema mradi wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara pekee unagharimu Sh. bilioni 7.5 na kwamba utakuwa na huduma zote muhimu ili kurahisisha shughuli hiyo.

Isare alisema wako katika hatua za mwisho kuwa miongoni mwa kampuni za kilimo zinazoingia na kuuza hisa zake katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Mohamed Simbano, alitaja miradi mingine waliyonayo kuwa ni mradi wa kilimo cha mpunga wilayani Kilombero. Pia wana miradi ya maharage mkoani Tanga, alizeti na mahindi wilayani Kiteto.

Alisema mkakati wao ni kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao yote wanayoyalisha na matarajio ni kuwa navyo kila eneo la mradi na mpaka sasa wana vituo vinne vinavyozalisha mazao.

# Jela miaka 30 kwa kosa kubaka mtoto

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemuhukumu mkulima wa Kijiji cha Ruvu, Kata ya Kilolambwani, wilayani Londi, Mussa Tharatha (52) kifungo cha miaka 30 jela, kuchapwa viboko na kulipa fidia kwa kosa la kumbaka mtoto wa miaka 16.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Elimo Massawe, baada ya Jamhuri kuthibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Hakimu Massawe alimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea, na akaiomba mahakama imwonee huruma kwa kumpa adhabu nafuu kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza na kuwa ana familia inayomtegemea, akiwamo mke, watoto, wazazi na wajukuu.

Pia, mshtakiwa Khalfani alidai alijikuta akishiriki tendo hilo bila ya kujitambua kutokana na ibirisi wa mapenzi kumfikia.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Masawe alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba iwapo ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa, ambaye alijibu kuwa, huku akiiomba mahakama hiyo kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye na tabia kama hiyo.

Hakimu Massawe akitoa hukumu ya kesi namba 80/2019, kupitia vifungu vya Sheria 130 (1) (2) (a) na 131 (1) kanuni ya adhabu sura ya 16/2002, alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili, lakini sheria imemfunga mikono, hivyo akamhukumu kwenda gerezani miaka 30.

Pia mahakama hiyo ilimpatia mshtakiwa huyo kuchapwa viboko sita wakati wa kuingia gerezani na atakapomaliza adhabu yake amlipe mlalamikaji fidia ya Sh. 200,000.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Mramba kuwa Novemba 4, 2019 mchana huko Kijiji cha Ruvu, Kata ya Kilolambwani, Tarafa ya Mchinga, mshtakiwa huku akitambua anachokifanya ni kosa, alimbaka mtoto huyo (jina limehifadhiwa).




Baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda cha TBL Mbeya wakifurahia wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHAWETU**

# Mfanyakazi anayedaiwa kufa kwa kichapo cha bosi azikwa

**Na Elisante John, SINGIDA**

MWILI wa Salome Zacharia (18), anayedaiwa kufariki dunia baada ya kupokea kipigo toka kwa waajiri wake mkoani Arusha, ulizikwa juzi katika kijiji cha Chikombo, Tarafa ya Itigi, wilayani Manyoni Mkoa wa Singida.

Wakizungumza kwenye mazishi hayo, baadhi ya waombolezaji waliwaomba wazazi na walezi, wajitahidi sana kujiridhisha kwanza na mazingira ya kazi, hususani makazi ya nyumba ambayo watoto wao wanakwenda kufanyakazi za ndani.

Wakati mazishi yakiendelea, mama yake Maria Athans, alikuwa akilia kwa simanzi kubwa, huku ndugu, jamaa na marafiki wakitumia wasaa huo kumfariji.

Waombolezaji nao walisema ni vema wazazi wawe wanajiridhisha na mazingira ya kazi, ikiwamo kuwatembelea mara kwa mara, badala ya kutofuatilia taarifa zao, hali inayochangia wapate manyanyaso.

"Ndugu zangu, watoto wetu tunawapeleka kwenda kufanya kazi za ndani, tujiridhishe na sehemu wanazokwenda, tujenge utamaduni wa kwenda kuwaona... tunaweza kudhani wanafanya kazi vizuri, kumbe ni afadhali angebaki tu hapa nyumbani ambako ni bora zaidi," alisema Haruna Chimanga, Diwani wa Kata ya Heka.

Naye Mchungaji wa Kanisa la Methodest, John Mjelwa, aliwaomba waombolezaji wa Kijiji cha Chikombo Tarafa ya Itigi alikozikwa Salome, waendelee kumtegemea Mungu katika maisha yao, ili waweze kushinda majaribu ikiwamo tukio kama hilo.

Mama wa Salome, Maria aliiomba serikali na wadau watakaojitokeza wamsaidie kumlea na kumsomesha mtoto mdogo mmoja aliyebakia.

Salome alifariki dunia mkoani Arusha, kutokana na kinachodaiwa alipata kipigo kikali kutoka kwa bosi wake mama mwenye nyumba, na kufariki njiani wakati akimpeleka hospitali.

## Wanafunzi waliosomea chini ya miti wajengewa shule

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WANAFUNZI 306 wa shule za awali, darasa la kwanza na la pili kwenye shule shikizi 'shule za muda' ya Mazinde Kata ya Loiborsoit, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wameondokana na adha baada ya kujengewa madarasa na Shirika la ECLAT Foundation.

Awali, kabla ya ujenzi wa madarasa hayo, wanafunzi wa shule hiyo walikuwa wakisomea chini ya miti.

Shirika hilo limejenga madarasa manne, matundu 16 ya vyoo na ofisi ya walimu.

Hata hivyo, wanafunzi wanatembea umbali zaidi ya kilomita 17, kwenda shule za msingi Loiborsoit A na Ruvu Remit.

Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima, akizungumza jana wakati akikabidhi shule hiyo, kwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema wamejenga shule baada ya kupokea maombi kutoka kwa uongozi wa kijiji hicho.

Toima alisema Shirika la ECLAT Foundation kwa kushirikiana na Taasisi ya Upendo ya Ujerumani wamejenga madarasa manne, matundu 16 ya vyoo na ofisi mbili za walimu.

"Katika ujenzi wa madarasa manne, wananchi walianza kujenga mawili, lakini hayakukamilika hivyo taasisi yetu iliyamalizia kwa gharama zilizobaki," alisema Toima.

Chaula, ameupongeza uongozi wa ECLAT Foundation, kwa kufanikisha ujenzi huo ambao utapunguza adha ya wanafunzi wa eneo hilo, kutembelea umbali mrefu wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Alitoa onyo kwa baadhi ya wanasiasa wa wilaya hiyo, wanaozusha maneno ya uongo dhidi ya shirika hilo kuwa wameingia makubaliano na halmashauri ya wilaya.

Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Silvanus Tairo, alisema shule hiyo, itasajiliwa hivi karibuni na jina la shule litakuwa ni Shule ya Msingi Mazinde.

Mwalimu wa shule hiyo, Kaika Elias, alisema alikuwa akifundisha peke yake wanafunzi 306, kwa kuwa mwalimu aliyekuwa akisaidiana naye alihama eneo hilo.

Mwanafunzi wa darasa la kwanza Samwel Alamayani, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwajengea madarasa hayo, kwa kuwa walikuwa wakisomea chini ya miti.

Alisema kwa kipindi chote walikuwa wakipigwa na upepo, vumbi na kunyeshewa na mvua.

Rachel Elia, mwanafunzi wa darasa la pili alisema baada ya shule hiyo, kujengwa hawatatembea umbali wa zaidi ya kilomita 32, kwenda shule za jirani kusoma kama ilivyokuwa awali.

# Watakiwa kuwajengea uwezo wanafunzi kujiajiri

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WAZAZI kwa kushirikiana na walimu wa shule za msingi na sekondari wametakiwa kuwaandaa na kuwajengea uwezo wanafunzi kujiajiri wakati watakapohitimu masomo yao.

Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari Winning Spirit, Simon Maxmillian, alisema hayo jana wakati akizungumza na wazazi na wanafunzi wakati wa mahafali ya tano ya kidato cha sita shuleni hapo, na jumla ya wanafunzi 44 walihitimu kidato cha sita.

Alisema shule hiyo na wazazi wana jukumu la kushirikiana kuwaandaa watoto, ili kukabiliana na tatizo la ajira na kuwajengea tabia ya kujiajiri wakiwa wapo shuleni.

Pia, alisema nchini kuna tatizo la ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo na shule za msingi na sekondari.

Alisema vijana wengi nchini wamejijengea dhana ya kuajiriwa na serikali baada ya kuhitimu masomo badala ya kujiajiri.

"Naomba wazazi tushirikiane kuwaandaa watoto wetu wakiwa bado shuleni kujiajiri kwa kufanya shughuli ndogo za kilimo na kuanzisha viwanda vidogo ambavyo mwisho wa siku vitawasaidia kujiajiri na kujikwamua kiuchumi," alisema Simon.

Hata hivyo, alisema shule hiyo imewaandaa wanafunzi hao, kujiajiri kwa kuwafundisha mbinu mbalimbali za kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari ya Renea, ambaye ni Ofisa Elimu Kata ya Sekei, Jiji la Arusha, Ruth Sabaya, aliwataka wanafunzi hao, kuwa na dhana ya kujiajiri kuliko kuajiriwa.

Aliwataka kuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii kwa kujishughulisha na kazi zitakazowapatia kipato.

Wakisoma risala kwa niaba ya wahitimu hao, Ansila Serafin na Justine Komba, walisema shule hiyo imewaandaa vizuri wanafunzi kujiajiri kwa kuwafundisha masomo ya ujasiriamali.

Walisema masomo hayo, watakwenda kufanya kwa vitendo kwa kuanzisha shughuli ndogo za kilimo na viwanda.

Hata hivyo, walisema shule yao inakabiliwa na tatizo la baadhi ya wazazi na walezi kushindwa kulipa ada kwa wakati na kusababisha baadhi ya wanafunzi kushuka kitaaluma na kushindwa kufikia malengo yao.

Mdau wa elimu jijini Arusha, Michael Shoo, akizungumza na wahitimu hao, aliwataka kuwa wabunifu kwa kuwa elimu ya kidato cha sita ni sawa na ya darasa la nne la zamani, hivyo kuwashauri kuwa wajasiriamali.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# NMB yawataka wajasiriamali kuchangamkia mikopo

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WAJASIRIAMALI katika sekta ya kilimo na biashara mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wametakiwa kuchangamkia fursa ya mikopo nafuu kwenye benki ya NMB ili kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Uhusiano wa Benki ya NMB, tawi la Mirerani, Damian Lukenza, aliyasema hayo jana, wakati wa kikao cha maendeleo cha Kata ya Endiamtu.

Lukenza alisema wajasiriamali wengi nchini, wamenufaika na mpango wa kilimo na biashara na kuwataka wakazi wa Mirerani kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema wananchi wakichukuwa mikopo itawasaidia kuendesha shughuli zao za kilimo na biashara na baada hapo watarejesha marejesho na watabakiwa na faida.

Alisema kwa kiwango kikubwa shughuli za kilimo na biashara kinawanyanyua wakulima wengi nchini.

"Kampuni nyingi zinaingia mkataba na wakulima wadogo ili kununua mazao yao ikiwamo mboga, matunda na maharage machanga, changamkieni fursa hiyo," alisema Lukenza.

Alisema Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mirerani, Allan Kombe, amefanikiwa kupiga hatua ya kimaendeleo kwa kutoa mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wa eneo hilo.

"Kwa upande wa uchimbaji wa madini ya Tanzanite tumeshindwa kutoa mikopo kutokana na mfumo wa uchimbaji ulivyo, lakini wafanyabiashara wengine wamenufaika kupata mkopo," alisema Lukenza.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tanesco, Justin Abraham, alisema viongozi wa benki hiyo, wanapaswa kuwashirikisha viongozi wa mitaa wakati wa kutoa mikopo hiyo ili kusitokee migogoro.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Endiamtu, Charles Msangya, ameipongeza benki hiyo wanavyotoa huduma kwa wananchi.





# Asisitiza vijana kujiajiri kwenye kilimo

**Na Godfrey Mushi, HAI**

KAMPUNI tanzu ya kilimo na ufugaji ya Agri-Connect Tanzania, imesisitiza kuwa ili vijana wajiajiri kwenye kilimo chenye tija, wanahitaji kuwezeshwa mitaji na mafunzo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Agness Link, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Machame iliyopo Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, alisema kuna haja ya serikali kuwekeza katika eneo hilo ili kumaliza tatizo.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa Afrika ndio inaongoza kwa kuwa na vijana wengi, huku ikitazamiwa kundi hilo kuongezeka.

"Mimi ninawashauri ninyi vijana mkipata nafasi baada ya masomo yenu hata mkimaliza chuo kikuu, nendeni kachangamkieni fursa zilizopo kwenye kilimo cha kisasa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kilimanjaro ili kiwasaidie kuwainua kiuchumi," alisema.

Alisema kwa sasa vijana wengi, wamejikita kwenye kilimo kisicho na tija, huku akiwataka kutumia muda mwingi kujifunza kilimo cha kisasa ambacho kinaendana na teknolojia pamoja na uzalishaji katika sekta hiyo.

Alisema Agri-Connect Tanzania wamelenga vijana wengi kujikita kwenye kilimo cha kisasa na chenye tija kitakachochangia katika kuinua kipato cha Mtanzania pamoja na ukuaji wa uchumi.

Kwa mujibu wa Link, Agri-Connect Tanzania ina mtazamo unaolenga kupunguza pengo la ukosefu wa ajira nchini kwa vijana, kupitia kinachoitwa minyororo ya thamani ya sekta ya kilimo na ufugaji.

**"Mimi ninawashauri ninyi vijana mkipata nafasi baada ya masomo yenu hata mkimaliza chuo kikuu, nendeni kachangamkieni fursa zilizopo kwenye kilimo cha kisasa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kilimanjaro ili kiwasaidie kuwainua kiuchumi," alisema.**

# Sekondari kuchuana insha maendeleo endelevu

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

SHULE 18 za sekondari za Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, kuanzia kesho zitaanza kuchuana kutafuta nguli wa insha inayoeleza maendeleo endelevu ya serikali ya Rais Dk. John Magufuli kwenye sekta mbalimbali.

Mashindano hayo yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), pamoja na mambo mengine yatahusisha pia elimu juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona ambayo itatolewa kwa kila shule.

Katibu wa Jumuiya hiyo Wilaya ya Siha, Bulugu Magege, akizungumza jana na Nipashe kuhusu shindano hilo, alisema mchuano huo unaanza rasmi Machi 18 na utafikia ukomo Machi 22, mwaka huu ili kupisha kamati inayoratibu kazi hiyo kutoa zawadi na majibu kwa umma.

"Napenda kusisitiza wakuu wote wa shule kuendelea kuwashawishi wanafunzi kuchangamkia fursa za mashindano pamoja na kuwaongezea uwezo wao kukuza ujuzi wa lugha, kwa sababu uandishi wa insha unaongeza maarifa kwa ujumla.

"Muhimu ambalo tunashauri wanafunzi na walimu kuzingatia ni kufuata taratibu zote za uandishi wa insha ili tuweze kupata insha nzuri, lakini kwenye suala la ugonjwa wa corona, pia wazingatie elimu ya wataalamu wa afya ya kujikinga na ugonjwa huu."

Bulugu alizitaja shule zinazoshiriki shindano hilo kuwa ni Suum Sekondari, Fuka, Oshara, Kishisha, Sanya Juu, Dahani, Kilingi, Kilasara na Karansi.

Nyingine ni sekondari za Magnificant, Magadini, Namwai, Matadi, Visitation, Nuru, Orkolili, Sikirari na Faraja Siha Sekondari.

Kwa mujibu wa katibu huyo, mshindi wa kwanza katika shindano hilo atazawadiwa kompyuta mpakato, mshindi wa pili atapata kompyuta ndogo ya mkononi ya Ipad, mshindi wa tatu atapewa zawadi ya begi la kisasa la vifaa vya shule, wakati washindi 10 wa kwanza watapewa medali.

Alisema uandishi wa insha, utawasaidia na kuwaongozea wanafunzi hao uwezo wao kukuza ujuzi wa lugha.

Aliwataka kusimamia kwa umakini mchakato wa mashindano hayo ili kuhakikisha ushiriki wa wanafunzi wengi.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Mbunge wa Babati Vijijini, mkoani Manyara, Vrajlal Jituson, akionyesha eneo linalopita mradi wa maji wa Minjingu-Darakuta, kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vitongoji 17 kuifanya Kilimanjaro ya kijani

**Na Godfrey Mushi, HAI**

VITONGOJI 17 vilivyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai mkoani Kilimanjaro, vimeanza 'kuusuka' upya mkakati wa kuufanya mji huo kuwa wa kijani, baada ya shule 21 za msingi na sekondari zilizopo eneo hilo kuanza utekelezaji wake.

Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo (TEO), Noel Nnko, amethibitisha kuwa ofisi yake, kwa maelekezo ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, inatekeleza mkakati wa kudumu wa kuondoa hali ya ukame katika mji huo.

"Zoezi hilo la upandaji miti linatarajia kuchukua muda wa mwaka mmoja kwa kupanda miti 100,000, na kwa awamu hii ya kwanza katika mji wa Hai tutapanda miti 10,000 ila tumeanza kutekeleza mkakati huu kwa kuigawa miti hiyo kwa shule 21 zilizopo kwenye vitongoji vyetu 17," alisema Nnko.

Kwa mujibu wa Nnko, nia ya mamlaka hiyo ni kubadili fikra za wananchi kuhusu mazingira, hasa wanaopita katika barabara kuu ya Moshi/Arusha, ambao baadhi yao hudhani mji huo hauwezi kubadili taswira yake kutokana na kuwa na miti michache.

Akizungumza wakati anazindua mkakati huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alisema:

"Mkakati wetu wa kutokomeza hali ya kijangwa ndiyo ambayo itaokoa hali iliyopo Hai kwa sasa. Mkakati huu wa 'Go Green' unalenga kuhakikisha tunabadilisha mtazamo wa watu wote wanaopita au kuujua mji wa Hai ulivyokuwa miaka ya nyuma na tunataka ufanane na miji mikubwa iliyopambwa kwa miti ya kijani kila kona. Zaidi ya watu 15,000 wanapita katika mji huo kwa siku."

Sintoo aligawa miche hiyo kufufua matumaini ya kuubadili mji huo kuwa wa kijani, baada ya kugawa miche ya miti 10,000 kwa wenyeviti wa vitongoji 17 na wakuu wa shule jana.

Pia Sintoo aliwaagiza watendaji wa kata na vijiji pamoja na Mkuu wa Idara ya Maliasili kuhakikisha wanasimamia upandaji na kutunza miti kwenye vitongoji vyote ili kufanikisha azma ya kuufanya mji wa Hai kuwa ya kijani.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 17, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**Mwanamke anaweza kuzaliwa bila kizazi**



Ukurasa 15

Ili kubana wabakaji, vifo mtoni, wachangishana kujenga shule



Ukurasa 17

## Ni hatari mabilioni ya vijana wakiwa viziwi




# 'Wazazi, walezi lawamani kulinda wanaoonyanyasa

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Polisi sasa kukagua magari kielektroniki



Polisi akikagua magari, jitihada zinafanywa na Shirika la Kuzalisha mali la Jeshi la Polisi, kuanzisha vituo vya ukaguzi kielektroniki. **PICHA: MTANDAO.**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uzalishaji mali ya mwaka 1974, madhumuni ya shirika hili ni kusimamia, kuendeleza na kufanya uwekezaji wenye tija kupitia miradi mbalim bali ya jeshi ili kulisaidia miradi ya kimkakati iwe na mchango chanya na manufaa kwa Jeshi la Polisi na taifa pia.

Malengo mahususi ya shirika hili ni kuhakikisha shughuli zote za kimkakati katika uwekezaji na uzalishaji mali zinafani kiwa kwa kiwango cha kuridhisha.

Lilianzishwa kwa madhumuni ya kutekeleza mambo kadhaa yakiwamo kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, kuboresha usimamizi wa rasilimali na uwajibikaji. Aidha, ni kuendeleza, kuimari sha na kuboresha mipango na uta ti na pia kuweka mazingira bora ya kazi na malazi.

## LIKO KIELEKTRONIKI

Moja ya mipango mkakati na ya muda mrefu ya shirika hilo ni pamoja na kuanzisha vituo vya ukaguzi wa magari vya kielektroniki au Electronic Vehicle Inspection Stations kwa nchi nzima ili kuendelea kupunguza ajali za barabarani zinazotokana na matatizo ya kiu fundi.

Halikadhalika pamoja na kukagua magari kielektroniki lina mpango wa kuanzisha namba za magari za kieletroniki hapa nchini ili kusaidia kudhibiti wizi na upotevu wa magari hayo na pia kutengeneza alama za barabarani kusaidia watumiaji wa barabara hizo.

Mipango mingine ni kuendeleza maeneo yote ya Jeshi la Polisi ambayo kwa muda mrefu hayajaendelezwa kimkakati.

Kuanzisha kituo cha michezo katika kambi ya Mtoni Kijichi Dar es Salaam kutakapokuwa na viwanja vyote vya michezo .

Shirika hili la uzalishaji mali ni matokeo ya maboresho ya polisi ambayo yanazingatia mihimili yote mitatu; kuboresha na kuanzi sha miundo mipya, weledi na kushirikisha.

Miundombinu ya Jeshi la Polisi itajengwa kupitia shirika hili kama ambavyo imeain ishwa katika Mpango Mkakati wake utakao ishia 2023 ukienda sambamba na mpango wa uchambuzi wa biashara.

Kwa upande wa kuishirikisha jamii, shirika litashirikiana nao katika maeneo ya uwekezaji hapa nchini ikijumuisha wadau kutoka nje ya nchi kwa manufaa ya Jeshi la Polisi.

Shirika limejipanga kuendesha mafunzo ya umahiri wa kutumia bunduki za kiraia na mafunzo yameshaanza kwa mkoa wa Dar es Salaam na baadae yatasambaa nchi nzima.

## MIKAKATI MINGINE

Mipango ya shirika la uzalishaji mali la jeshi la polisi ni pamoja na kukabiliana na hali ya kiushindani nchini, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi lina mipango ya muda mfupi kama ilivyo mirefu na miongoni mwa mipango hiyo tayari imeanza kutekelezwa na inaendelea vizuri.

Hii ni pamoja na kutoa mafunzo mbalim bali katika matumizi sahihi ya silaha za moto za kiraia. Mafunzo haya yanalenga makundi makuu matatu ambayo ni kampuni binafsi za ulinzi, kampuni za uwindaji, wamiliki binafsi wa silaha za moto za kiraia.

Aidha, pia ni kutoa ushauri elekezi katika maeneo ya ujenzi, usalama na ulinzi, tekinolojia ya habari na biashara ya kidijitali.

## HUDUMA

Huduma mbalimbali zinazotolewa na shirika hili la uzalishaji mali la jeshi la polisi ni pamoja na ujenzi na hii ni pamoja na ujenzi wa barabara, nyumba za kuishi, maghala, majengo ya burudani, majengo ya hoteli, mitandao ya mawasiliano na mitambo ya nishati ya jua.

Nyingine ni mafunzo ya umahiri wa matumizi ya silaha za kiraia na ukarabati wake. Hii inahusisha kampuni binafsi za ulinzi, matumizi na utengenezji au ukarabati wa silaha, mafunzo ya kujilinda na usalama wa mtu binafsi na mafunzo ya utaalam wa kutumia mbwa.

JIELIMISHE

# Mwanamke anaweza kuzaliwa bila kizazi

JULIAN Peters ana miaka 29, akiwa amezaliwa na ugonjwa unaojulikana kama (MRKH) Mayer Rokitansky K ster Hauser, huu ni ugonjwa unaoathiri wanawake na hasa kizazi cha mwa namke. Hali hii inamaanisha kuwa mtu anazaliwa bila mfuko wa kizazi.

Hali hii ninayoishi nayo ni achangamoto nyingi kwani kila siku ninakabiliana na hisia mseto, mbali na hayo jamii inayonizunguka pia wakati mwengine inataswira tofauti kuhusu hali hii , anasema Julian

Anasema kuwa maoni ya jamii yanatofautiana kuhusu hali yake kwani kuna wale ambao wanaamini kuwa hali anayoishi nayo sio ugonjwa bali ni jambo aliliojiletea mwenyewe, pengine kwa dhana kuwa aliavya mimba nyingi au pengine aliwahi shiriki maswala ya ushirikina.

Julian (pichani chini) anasema maoni hayo wakati mwengine yanakera lakini anavumilia na kuendelea na maisha yake,anasema aligundua kuhusu ugonjwa huu akiwa kidato cha tatu, wakati huo alikuwa na miaka 17, anakumbuka alikuwa alikwenda hospitalini ku pata ushauri wa daktari kwa sababu alikuwa anaumwa na miguu . Alipofika hospitalini daktari alianza kwa kumuuliza baadhi ya maswali

Daktari aliniuliza wakati wa mwisho wa kupata hedhi yangu ni lini? Jibu langu lilikuwa sikuwa nimepata hedhi zangu .

Kwa mujibu wa daktari Mutindi Kakuti wanawake wenye ugonjwa huu wanaweza kushiriki ngono endapo watafanyiwa upasuaji wa kurekebisha njia au sehemu za siri.

Baada ya daktari aliyekuwa anamtibu kufahamu kuwa kwa umri wake Juliana wa 17 hakuwa na hedhi, alitaka afanyiwe uchunguzi wa sehemu zake za uzazi, baada ya uchunguzi kufanywa ikiwa ni pamoja na kupigwa picha ya kizazi chake, hapo ndipo iligunduliwa kwamba alikuwa hana kizazi chote kama wanawake wengine na pia njia ya uke wake ilikuwa imeziba kutoka upande wa nje.

Japo alikuwa hana umri mkubwa sana hakuelewa mengi kuhusiana na hali hiyo, kwa hiyo alipoelezwa na dakatari kama binadamu hakua mini alichokuwa anaelezwa, Julian anasema.

Wakati huo nilikuwa shuleni na nilikuwa tayari nasomea baiolojia, nilifahamu jinsi mwili wa mwan amke unavyopaswa kufanana, kwa hiyo nililia sana kwa kutambua kuwa sehemu ya kizazi changu zilikuwa na kasoro ila sikuwa na lingine la kufanya

Madaktari wakati huo waliamua kuwa wangemfanyia upasuaji ili kufungua njia ya uke wake, japo katika suala la mfuko wa kizazi hawakuwa na la kufanywa zaidi ya kukubali kuishi maisha yake hivyo.

Juliana anasema kuwa Nilikubali kuhusu hali yangu nikiwa umri wa miaka 24, baada ya kuelezwa ukweli wa mambo, nilirejea shuleni tu na kuamua kusoma kweli kweli. Nilipomaliza shule ya sekondari nilianza kufanya uchunguzi wangu vitabuni, na nikaanza kuelewa changamoto nilizokuwa napitia kama muathiriwa wa ugonjwa huu

Mwanamke mmoja kati ya 4,000 duniani ana tatizo la kutokuwa na kizazi sawa na la Julian, anasema kuwa amekuwa na mahusiano ya kimapenzi, lakini hajajihusisha na shughuli ya ngono kwani kila daraja ambalo anavuka maishani mwake anahitaji kujitayarisha na kuwa makini zaidi lakini haijakuwa rahisi.

Upasuaji wa mwisho Julian anasema, ulihusisha kufanyiwa marekebisho kwenye uke wake sio kwa sababu ya kujifungua mtoto, lakini aweze kushiriki ngono.

Anasema kuwa bado hajaamua kuanza tendo lenyewe kwani matu maini yake ni kupata mtu ambaye atamkubali alivyo kwanza.

## CHANZO MKHR?

Daktari Mutindi Kakuti, anasema masuala ya uzazi nchini Kenya anasema hali hii hutokea wakati mtoto wa kike anapokuwa tum boni mwa mama yake, na wakati mwingine huibuka kuwa viungo vya mwili husussan vya uzazi vya mtoto hukosa kujiunda kama inavyofaa au kama ilivyokawaida. **BBC**



ELIMU

NA SHAABAN NJIA, KAHAMA

# Ili kubana wababakaji, vifo mtoni, wachangishana kujenga shule



Wanafunzi wa sekondari Ubagwe wakiimba nyimbo za kuwasifu wazazi kwa kujenga shule. Wanafunzi wa shule za msingi Ubagwe na Wadui wakiwa pembeni wanasikiliza. **PICHA: SHABAN NJIA**

HUENDA msemo wa elimu ni ufunguo wa maisha, ndiyo uliowafungua macho wakazi wa Kata ya Ubagwe wilayani Ushetu mkoani Shinyanga kuamua kuchangishana ili kujenga sekondari kwa ajili ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi.

Ukweli ni kwamba wilayani Ushetu wapo wanafunzi wanaoshindwa kufanya vema kwenye mitihani yao kutokana na sababu ya ugumu wa maisha nyumbani, kutembea umbali mrefu kutafuta elimu hali ambayo wakati mwingine huwakatisha tamaa ya kuendelea na masomo kutokana na kuchoka.

Licha ya kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wanaofanya vema kwenye mitihani yao ni wanafunzi wa kiume ukilinganisha na wanafunzi wa kike ambao hurubunika kwa vishawishi mbalimbali kwa kupewa lifti na madereva bobaboda kwenda shule na kujikuta kwenye uhusiano wa kimapenzi, changamoto inayotumbukiza kwenye mimba.

Kwa ujumla tatizo haliko Ushetu pekee ila changamoto za wanafunzi wa kike na wakiume kushindwa kufanya vyema masomo yao kutokana na umbali wa shule wanayosomea inawasibu hasa walio nje ya miji pengine hata kwa taifa zima.

Wasomi hawa ni wale wanaokaa kwenye kata ambazo hazina sekondari na wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi kila siku hutembea au kusafiri hadi kata za jirani.

### HALI HALISI

Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama ni moja ya maeneo ambayo yana changamoto ya ukosefu wa sekondari kwa baadhi ya kata hasa zilizopo pembezoni, hali ambayo inasababisha wengi kutembea umbali mrefu kutafuta elimu.

Kwanza hulazimika kutembea umbali wa kilometa 20 kwenye kata ya jirani ya Ulowa kutafuta elimu.

Wengi wa wanafunzi wa kata hiyo wanakatisha masomo hasa mabinti kwa kubakwa na kubebeshwa ujauzito na madereva bodaboda na baiskeli kwa kupewa lifti na wengi hujikuta kwenye ndoa baada ya wazazi na walezi wanaopenda wasome kuwapangishia nyumba lakini wakashindwa kuwalipia kodi na kuwahudumia.

Kwa kuliona hili kwenye kata ya Ubagwe, wazazi, walezi na wadau mbalimbali walichangishana kila kata Sh. 15,000 na kujenga Sekondari ya Ubagwe.

### WALIVYOLIPOKEA

Sabina Petro ni mmoja wa wakazi wa kata hiyo anayesema kuwa, kabla ya kujengwa sekondari ya kata wanafunzi walikuwa wakitembea kilometa 20 kutoka Ubagwe hadi Ulowa sekondari na wengine wakitembea kilometa nane kila siku kutoka Kijiji cha Mwadui kufikia shule hiyo. Anasema walichangishana fedha za ujenzi wa sekondari na kwa kila kaya

> Baadhi ya wanafunzi hao walikuwa wakitembea kilometa 20 kwenda kata ya Ulowa na wengine kilometa nane kutoka katika Kijiji cha Mwadui kilichoko kata ya Ubagwe.

Hata hivyo, anasema ili kufika shuleni Ulowa, wanafunzi hulazimika kuvuka mto mkubwa na wakati wa masika, wengi hawaendi shuleni kutokana na mto huo kujaa maji mara kwa mara.

"Binti yangu alisimama masomo kwanza umbali na pia kushindwa kuvuka mto mkubwa unaotutenganisha na kata ya Ulowa," anasema Sabina.

Rupia Surambaya, anasema walilazimika kufanya hivyo, kwa madereva pikipiki na waendesha baiskeli walitumia fursa ya umbali mrefu kuwahadaa wanafunzi wa kike kingono kwa madai ya kuwapa lifti za kuwafikisha shuleni.

### KUCHUKUA HATUA

Surambaya anasema kwa kuwa, changamoto hiyo ilikuwa kubwa walikaa vikao vya wazazi na walezi pamoja na diwani wa kata hiyo Hamisi Majogolo na kukubaliana kila kaya kuchangia 15,000 na kujenga vyumba viwili vya madarasa, jengo la utawala na nyumba moja ya waalimu ambayo nayo haijakamilika.

### JITIHADA ZA VIONGOZI

Diwani viti maalumu Ulowa, Ubagwe Gabriela Kimaro, kutoka kata ya Ulowa anasema, Sekondari ya Ulowa ina wanafunzi zaidi ya 2,000 na wengi wanatoka kata ya Ugawe na Kijiji cha Mwadaui.

Anasema kuwa, shule za msingi zilipo kata ya Ulowa na Ubagwe zina idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza ndiyo sababu ya halmashauri inaendelea kuzisajili shule Shikizi za Bukome, Mapamba pamoja Sekondari Ubagwe.

Diwani anasema kabla ya kujengwa kwa shule hiyo, malezi bora kwa wanafunzi wa kike yalikuwa yamepungua hasa wale waliokuwa wamepanga jirani na sekondari kujihusisha na vitendo vya ngono huku vijana nao wakishindwa kufika shuleni na kuishia njiani.

Diwani wa kata ya Ubagwe Hamisi Majogolo anasema kuwa, asilimia95 ya wakazi wa kata hiyo ni wakulima na wafugaji na hujitoa katika kuchangia shughuli za maendeleo inapofika wakati wa mavuno.

Hata hivyo anamuomba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matora, kutuma watalaumu na kulipima eneo lote la shule na kuliwekea alama ili wananchi wasilivamie na kuendesha shughuli za kilimo na kuzua migogoro.

Pia anawaomba wazazi na walezi kuendelea kuchangia michango mbalimbali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa shule hasa vyumba vya madarasa, nyumba ya walimu na ifikapo mwakani shule hiyo itapokea zaidi ya wanafunzi 250 watakaoanza kidato cha kwanza.

### UONGOZI WA UBAGWE.

Mwalimu Mkuu wa Sekondari ya Ubagwe, Lucas Magembe ana eleza kuwa, shule hiyo ilipangiwa wanafunzi 153 waliokuwa wakisoma katika sekondari ya Ulowa, wa kike 59 na wakiume 94. Anasema walioripoti ni 120 wa kiume wakiwa 71 na wakike 49.

"Baadhi ya wanafunzi hao walikuwa wakitembea kilometa 20 kwenda kata ya Ulowa na wengine kilometa nane kutoka katika Kijiji cha Mwadui kilichoko kata ya Ubagwe."

Magembe anasema Mkurugenzi wa Halmashauri alitoa milioni 29 ili kukamisha madarasa ambayo ndiyo yanatumika.

Anasema kwa sasa changamoto iliyopo ni ukosefu wa vyumba vya madarasa ya kwani shule nzima ina jumla ya madarasa mawili na kila darasa moja linabeba wanafunzi 60 na walimu wanalala kwenye nyumba za wageni.

Pia anasema kuwa, mwakani wanatarajia kupokea zaidi ya wanafunzi 250 idadi ambayo ni kubwa ukilinganisha na vyumba vya madarasa vilivyopo na kuwaomba wazazi kukamilisha miundombinu ya shule hiyo ikiwamo ujenzi wa matundu sita ya vyoo vya wasichana.

### SAUTI YA MBUNGE

Elias Kwandikwa ni Naibu Waziri wa Ujenzi na pia Mbunge wa jimbo la Ushetu, anapongeza wazazi, walezi na wadau wa maendeleo ya kata kwa kujenga shule ya sekondari ya kata.

"Hakuna jambo tunaweza kulifanya na kufanikiwa kama hatuna ushirikiano uliotukuka."

Anasema maeneo mengi walipojenga shule za sekondari na msingi kwa ajili ya kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu hakuna nyumba za walimu na kuwataka waananchi kujenga nyumba za walimu ili walimu waishi karibu na shule hizo.

ELIMU

NA MAGRETH MAGOSSO, KIGOMA

# ‘Wazazi, walezi lawamani kulinda wanaonyanyasa

• Huwahamisha watoto wanaonajisiwa

MUHALI au kuonea aibu nikimsema aliyenidhuru kijinsia atanitizamaje. Atanionaje au atanifikiriaje kwenye jamii yetu ni jambo linalokwamisha juhudi za kupambana na ukatili wa kijinsia karibu Tanzania nzima. Kinachojiri ni kufichiana siri, kulinda wahalifu na kupuuza ni mambo yanayoelezwa kuwa hurudisha nyuma maendeleo ya kutokomeza ukatili huo, kwenye mikoa mingi na Kigoma ambao unatajwa kuwa ni miongoni mwa vinara.

Kwa kulitambua hilo, serikali kwa ushirikiano na mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa (UN) wameanzisha Mradi wa Kigoma Pamoja Programu unaowezesha dawati la polisi jinsia na watoto kwa miaka mine, uliozinduliwa rasmi Septemba mwaka 2017,wilayani Kasulu kwa lengo la kutatua changamoto ya ukatili wa kijinsia kwa wananchi.

Hatua hiyo inatokana na sehemu kubwa ya wanawake na watoto kuathirika na matukio ya ukatili wa kijinsia nchini, hususani wilaya nne mkoani Kigoma.

Mradi wa Kigoma Pamoja Programu (KJP), unakuja baada ya kubaini wingi wa kero hiyo kwa kutumia takwimu za mwaka 2015 zinazoonyesha kuwa kati ya kesi 17,059 zilizoripotiwa kituo cha polisi, za ukatili dhidi ya wanawake ni 5,802 zinazohusisha ubakwaji na kesi 2,873 unajisi kwa watoto.




Polisi ni wadau wakubwa kwenye masuala ya kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia. Baadhi ya polisi na wanafunzi katika harakati za kupinga ukatili huo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Kwa mujibu wa washirika wa mradi huo takwimu hizo zimeisukuma serikali na mashirika 16 ya UN katika mradi wa KJP kuwawezesha wanawake na watoto kubaki salama.

Kinachofanywa ni kuwajengea uelewa kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia ni pamoja na kukosa kujiamini katika jamii, kupoteza utu wao huku wahalifu wakiendeleza mienendo mibovu ya kunajisi bila kuchukuliwa hatua.

Pamoja na mradi huo wa KJP kukabidhi majengo ya kisasa, kuboresha mazingira ya ofisi na kuwajengea uelewa maofisa wa dawati la polisi jinsia na watoto .

Hata hivyo, mambo ni tofauti kwa Wilaya ya Kasulu ambayo inakabiliwa na changamoto kubwa ya baadhi ya waathiriwa wa ukatili wa kijinsia kukwamisha kesi za ukatili wa kijinsia kortini.

**CHANGAMOTO**

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Dawati la Jinsia Polisi Wilaya ya Kasulu, Maimuna Abdul, anasema anakerwa na namna ya ukwamishaji wa kesi wakati wa uendeshaji mahakamani.

> “Nilipewa mimba nikiwa kidato cha nne, aliyenibaka alinifumba mdomo na familia kwa kutoa Sh 600,000, walimu waliniruhusu nifanye mtihani wa taifa 2014.




Anataja baadhi ya walezi na wazazi kuwa wanadiriki kuwahamisha mikoa watoto wao waliofanyiwa ubakwaji au ulawiti ili kupoteza ushahidi, ni kwa mujibu wa Abdul.

Anaeleza kuwa matendo hayo ni kuwalinda wahalifu lakini pia kukwamisha maendeleo ya watoto waathirika kitaaluma, afya na kisaikolojia kwa lengo la kuwatetea wahusika, jambo lisilokuwa na tija kwa familia na mtoto wao.

Anaeleza zaidi kuwa waathiriwa wa kesi mbalimbali za ukatili wa kijinsia ‘hususani wanaolawitiwa na wenza wao katika ndoa, ambao huharibu ushahidi wakati wa kusikiliza mashauri mahakamani.

“Yote haya yanazorotesha jitihada ya serikali na wadau wa maendeleo, kutokomeza vitendo vya ukatili katika jamii, mfano karibuni alikuja mwanamke akilia kwa madai ya kudhalilishwa kinyume cha maumbile na mwenza wake. Baada ya kupewa huduma ya matibabu hajarudi kwetu.” Anasema.

Anaeleza kuwa kwa uzoefu wake tangu wakabidhiwe dawati hilo Septemba 2017, kupitia mradi wa Kigoma Pamoja Program utoaji wa taarifa katika ofisi yake umeongezeka kutoka asilimia 35 kwa mwaka 2011 hadi 48 kwa mwaka 2019.

Hata hivyo, walengwa walio wengi wanalitumia vibaya dawati hilo, wanawake wanaonyanyaswa kingono kinyume cha maumbile na wenza wao, vipigo na ubakwaji ,huripoti tukio katika dawati hilo kwa ajili ya kupewa fomu ya PF3 kwa ajili ya tiba tu.

Lakini, kifungu cha 131 cha sheria ya kanuni ya adhabu ya Tanzania (CAP 16 2006) kinatoa kifungo cha maisha jela ,pamoja na kuchapwa viboko kwa mshitakiwa anayekutwa na hatia, lakini walalamikaji huingia mitini.

Abdul anasisitiza kuwa waathiriwa dhidi ya ukatili wa kijinsia wanapaswa kujitambua na kufahamu madhara ya kutupa haki zao kwa malipo kiduchu ya fedha kutoka kwa watuhumiwa kwa nia ya kudhibiti kesi kortini.

“Wao ndiyo waathirika siku za usoni. Wananchi wanatakiwa kulifahamu na kuwachukulia hatua za kisheria wahalifu huku akibainisha kuwa kutumia mikusanyiko ya watu kuelimisha madhara ya ukatili wa kijinsia ni hatua inayofuata,” anasema.

Aidha, anawakumbusha wanawake wasikubali kutumiwa vibaya na wenza wao kwa maslahi ya kulinda ndoa ambayo haina faida kwao mbali na kudhurika kiafya , badala yake anawataka kujishughulisha na biashara ndogondogo ambazo baadaye zitakua na kuwaondoa kwenye utegemezi wa kipato,unaopelekea baadhi ya wanandoa kutokuwa na amani katika uhusiano .

Anaeleza kuwa kinachosikitisha ni kwamba kesi zinazoripotiwa katika dawati hilo hushindwa kuwatia hatiani wahalifu wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa asilimia 80 huku asilimia 20 zinazofikishwa katika mahakama wahalifu huwatia hatiani.

Lakini, hata kufikia hukumu kunasuasua kutokana na baadhi yao kuharibu ushahidi kwa makusudi, wakati kesi zinapokuwa kortini , licha ya kwamba wapo wanaoujutia baada ya wahalifu kutoweka katika makubaliano na mipango waliyofanya ya kulindana.

Ofisa Ustawi wa Jamii Kasulu Godfrey Kapaya, anasema ushirika wa serikali na mashirika 16 ya mradi wa KJP kumeongeza utoaji wa taarifa kwa wakati.

“Changamoto inabakia kusaidia kuvuruga kesi, mfano mwanafunzi akipewa mimba hukubaliana kumtunza, lakini akijifungua hana msaada na mtuhumiwa anatoweka ndipo familia hutoa taarifa katika dawati la jinsia kutaka achukuliwe hatua kwa maslai ya kiuchumi na sio adhabu za kisheria zinazohusisha vifungo,”anaeleza Kapaya.

Aidha, jamii itambue madhara ya kuharibu ushahidi wa kesi za ukatili wa kijinsia ni pamoja na kusababisha hasara inayotokana na kutumia fedha nyingi kununua dawa na vifaa tiba kushughulikia walioumizwa na ukatili wa kingono.

Waathirika nao huondolewa utu wao, kutothaminika katika jamii na kuendelea kuwapo maadili mabovu kutokana na wabakaji na wanyanyasaji kuendeleza uovu.

**USHUHUDA WA WAATHIRIKA**

Akitoa ushuhuda Tatu Mussa, Mtendaji wa Kata ya Kimwobwe, anasema ukosefu elimu ya madhara ya ukatili wa kijinsia na utegemezi wa kipato huongeza unyanyasaji.

“Mtoto wa dada yangu alibakwa akiwa anatoka kuomba fedha ya chakula kazini kwa baba yake. Aliyemtenda hayo ni mfanyakazi mwenzie na baba yake. Kama wanawake wakijitambua na tukiimarika kiuchumi ukatili utakuwa historia “anafafanua shuhuda Mwajuma Kaweleka, mwanafamilia ambaye mtoto wao alibakwa huko Kigoma .

‘Nilipewa mimba nikiwa kidato cha nne, aliyenibaka alinifumba mdomo na familia kwa kutoa Sh 600,000, walimu waliniruhusu nifanye mtihani wa taifa wa mwaka 2014. Baada ya kujifungua, mwanamume huyo alinifukuza na mtoto akatafuta mwanamke mwingine,” anasema mwathirika.

> Mtoto wa dada yangu alibakwa akiwa anatoka kuomba fedha ya chakula kazini kwa baba yake. Aliyemtenda hayo ni mfanyakazi mwenzie na baba yake.

Mratibu Miradi ya UN Program ya Kigoma Pamoja, Evance Siangicha, mradhi huo unalenga kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (VAWC) ,kuwawezesha wasichana wa umri wa kupevuka kupata, kuwapatia wananchi,maji safi,usafi wa mazingira na usafi wa mwili.

Aidha, inahusika na nishati na mazingira endelevu (SEE) na kilimo ambayo inagharimu Dola milioni 55.

**CHANGAMOTO**

Akizungumzia changamoto ya ukatili wa kijinsia Katibu Tawala wa Kigoma Rashid Mchatta, anasema katika kila watoto 10 wanne wamefanyiwa ukatili.

Anasema Kigoma ni moja ya mikoa inayotajwa kuwa kinara katika ukatili wa kijinsia na kwamba kuanzia Januari hadi Juni mwaka 2019 watoto 53 walifanyiwa ukatili wa kingono.

Anasema kati yao 14 ni watoto wa kiume na 39 wasichana na kwa upande wa ukatili wa kimwili taarifa inaeleza idadi ya watoto 68 waliathiriwa wakiume wakiwa 32 na watoto wa kike 36 .

Anasema ukatili wa kiakili umefanywa kwa watoto 246 , kati yao 110 ni wanaume na wa kike ni 196.


Mchatta anasema wakati huohuo jumla ya watoto 117 walioajiriwa kwa ujira kiduchu ilihali wanafanyishwa kazi ngumu kwenye ukatili wa kiuchumi na kati ya hao 62 ni wa kiume na 55 watoto wa kike.

Mpango wa utekelezaji wa taifa wa kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ya mwaka( 2001-2015) unaoainisha umuhimu wa jamii kutambua athari ya ukatili wa kijinsia kuwa ni kuzorota kwa uchumi ikiwamo kukwamisha wanawake kushiriki ipasavyo katika shughuli za kiuchumi.

Aidha ni kuwaumiza watoto , kuzorotesha afya na maendeleo yao kuanzia kielimu, afya na kisaikolojia

RIPOTI

## Hatari mabilioni ya vijana wakiwa viziwi



Vijana wanapendelea kuweka ‘phone’ masikioni na kusikiliza muziki kwa sauti kubwa huumiza ngoma za masikio na huhatarisha uwezo wa kusikia. **PICHA: MTANDAO.**

VIJANA zaidi ya bilioni moja wa umri wa kati ya miaka 12 hadi 35 wanajiweka katika hatari ya kuwa viziwi, tena wasioweza kutibika kwa sababu ya kusikiliza sauti za juu za vitu kama muziki kwa kutumia simu za mikononi simu janja.

Taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaeleza baada ya kutoa mwongozo mpya wa kusaidia kushughulikia tatizo hilo.

Mapendekezo yaliyotolewa na mwongozo huo kupunguza tatizo la wengi kuwa viziwi kwa kusikiliza sauti za juu ni pamoja na utendaji kazi bora wa vifaa vya kusikilizia ambavyo vinaweza kudhibiti uwiano wa sauti ikiwa ni ya juu sana, muda ambao watu wanasikiliza muziki kutumia vifaa hivyo.

Mtaalam wa kiufundi wa WHO anayehusika na masuala ya kuzuia uziwi na kupoteza uwezo wa masikio kusikia, Dk. Shelly Chadha, anasema “vijana zaidi ya bilioni moja wako hatarini kupata uziwi kwa sababu tu ya kufanya kile wanachokifurahia zaidi mara kwa mara , ambacho ni kusikiliza muziki kupitia vipokea sauti vinavyobanwa kichwani (headphones)” anasema na kuongeza kuwa “kwa wakati huu hatuna kitu chochote kinachoshikika isipokuwa ni hisia zetu tu zikituambia ‘unachofanya ni sahihi, au je, hiki ni kitu ambacho kitatusababishia kupoteza uwezo wetu wa kusikia au uziwi katika miaka michache ijayo?”

Mradi wa pamoja wa WHO na Muungano wa kimataifa wa mawasiliano ITU ni jaribio la kutaka kukabiliana na tatizo la wateja wa simu na watu kwa ujumla kutokuwa na ufahamu kuhusu athari za kusikiliza kelele kubwa.

Haya yanatokea wakati kukiwa na takwimu zinazoonyesha kwamba, takriban asilimia 50 ya vijana wanasikiliza sauti katika viwango visivyo salama kupitia vifaa binafsi zikiwamo simu za kisasa ambazo matumizi yake yanaendelea kuongezeka duniani.

Kwa mujibu wa WHO tatizo la kupoteza uwezo wa kusikia ambalo halijashughulikiwa linaugharimu uchumi wa dunia Dola milioni 750 kila mwaka.

**MAPENDEKEZO**

Dk. Chadha anapendekeza kuwa “inabidi kufikiria kwamba suala hili ni kama kuendesha gari kwenye barabara kuu lakini bila kuwa na kidhibiti mwendo. Na tulichokipendekeza ni kwamba simu janja ziwe na vifaa vya kudhibiti sauti vinavyoelezea ni kiwango gani cha sauti unachokipata kwenye simu na kukujulisha endapo kimepindukia kiwango kinachohitajika.” **WHO**

JE, WAJUA?

# ‘Madudu’ yaliyosababisha TCU kufunga vyuo vikuu -2

• Mitaji yao, wahadhiri hali mbaya • Sayansi: Maabara, madarasa ‘uozo’



Moja ya majengo ya Chuo KIkuu cha Kampala (Tanzania). Chuo hicho kilisitishiwa udahili na TCU na baadaye kuruhusiwa baada ya kurekebisha dosari. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

***KATIKA sehemu ya kwanza wiki iliyopita, tuliangazia namna Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) inavyodhibiti ubora wa juu nchini na hatua inazochukua dhidi ya wasiokidhi viwango vya ubora.***

***Mwendelezo wa makala hii leo, unarejea hatua za kuvifuta baadhi ya vyuo na taasisi za elimu ya juu zilizochukuliwa na TCU kama anavyoeleza Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Profesa Charles Kihampa. Endelea...***

ANASEMA kuwa kwa kuzingatia muda uliotolewa na hali ya vyuo husika na dosari kubwa zilizobainika ikiwa ni pamoja na uhaba wa watumishi na fedha, baadhi ya vyuo kushindwa kujiendesha hata vikipewa muda zaidi, ilibidi kuvipitishia kalamu nyekundu.

Anasema kwa kulibaini hilo, TCU ililazimika kufuta usajili wa vyuo saba na kuelekeza wanafunzi wahamishiwe kwenye vyuo vingine vinavyokidhi viwango vya ubora.

Vilivyofutiwa usajili ni pamoja na Chuo Kikuu cha Eckenforde Tanga (ETU), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU), Chuo Kikuu cha Mlima Meru (MMU) na Chuo Kikuu cha Tumaini - Kituo cha Mbeya (TUMA - Mbeya Centre).

Vingine ni Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji - Kituo cha Tabora (TEKU - Tabora Centre), Chuo Kikuu cha Josiah Kibira (JoKUCo) na Chuo Kikuu cha Bagamoyo (UoB).

Anabainisha kuwa wanafunzi 2,607 wa fani za sayansi ya elimu, sanaa ya elimu, sanaa ya rasilimali watu, elimu maalum na udaktari wa binadamu, walihamishiwa katika vyuo vingine.

Anasema katika kipindi hicho cha miaka minne, kupitia makongamano na semina elekezi zilizoandaliwa na kuratibiwa na TCU kwa viongozi, wahadhiri na wafanyakazi, waendeshaji wa vyuo vikuu kwa lengo la kubadilishana uzoefu na tafsiri ya miongozo ya elimu ya vyuo vikuu duniani, vyuo vikuu vimeimarisha mifumo yake ya ubora na uendeshaji wa mafunzo.

> “Matokeo ya makongamano hayo ni pamoja na tathmini binafsi zilizofanywa na vyuo vyenyewe.Kufuatia tathmini hizo, baadhi ya vyuo vimeiomba tume kusitisha uendeshaji ili vijipange upya.



Katibu Mtendaji wa TCU, Profesa Charles Kihampa.

“Matokeo ya makongamano hayo ni pamoja na tathmini binafsi zilizofanywa na vyuo vyenyewe.Kufuatia tathmini hizo, baadhi ya vyuo vimeiomba tume kusitisha uendeshaji ili vijipange upya,” anasema.

Taasisi ambazo tume imesharidhia maombi yao na kufuta usajili wake ni pamoja na Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia - Kituo cha Arusha (JKUAT), Chuo Kikuu cha Mt. Yohana - Kituo cha Msalato (SJUT) na Chuo Kikuu cha Kenyatta - Kituo cha Arusha (KU).

“Vingine ni Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania - Kituo cha Mt. Marko (SJUT), Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Yakobo (AJUCo), Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Kadinali Rugambwa (CARUMUCo) na Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji - Kituo cha Dar es Salaam (TEKU),” anasema.

Profesa Kihampa anasema TCU pia ilisimamisha programu 33 za masomo kutoka katika vyuo mbalimbali kutokana na maombi ya vyuo husika baada ya kushiriki katika makongamano na mafunzo yaliyowafikia pia wafanyakazi 1,581 kutoka vyuo vikuu vinavyomilikiwa na serikali na taasisi binafsi.

Anasema TCU pia imerejesha kwa asilimia 100 jukumu la udahili kwa taasisi za elimu ya juu kama yalivyo matakwa ya sheria.

“Hili limewezekana kwa kutengenezwa mfumo wa pamoja wa kielektroniki kwa ajili ya kuratibu udahili wa shahada za kwanza kwa vyuo vyote vya elimu ya juu.

“Mfumo huu umeunganishwa moja kwa moja na mifumo ya vyuo vya elimu juu na umetoa mamlaka kamili kwa vyuo vya elimu ya juu kushiriki moja kwa moja katika udahili wa wanafunzi kupitia seneti zao kama yalivyo matakwa ya sheria,” anasema.

Anaongeza kuwa mfumo huo pia umeunganishwa na kanzidata za Baraza la Mitihani (Necta), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (Nacte), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB).

Anasema uunganishwaji huo umerahisisha upatikanaji wa taarifa za udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu na kuiwezesha TCU kuhakiki sifa za wanafunzi wanaodahiliwa na vyuo vya elimu ya juu kwa uhakika na ufanisi zaidi na pia umerahisisha upatikanaji wa taarifa za wanafunzi kwa taasisi za mikopo ya elimu ya juu.

Profesa Kihampa anasema kuogezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya TCU na taratibu za udahili katika vyuo vya elimu ya juu, kumepunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yaliyokuwa yanaibuka katika udahili wa elimu ya juu.

Anasema takwimu zinaonyesha idadi ya wadahiliwa wa shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 65,064 mwaka 2015/2016 hadi 87,813 kufikia mwaka 2019/2020, sawa na ongezeko la asilimia 35.

Anabainisha kuwa kwa takribani miaka 12 zimekuwapo wakala kwa wanafunzi wanaotaka kusoma elimu ya juu nje ya Tanzania na kwamba, pamoja na kuwa jukumu mojawapo la TCU ni kusajili wakala wa aina hiyo, utekelezaji wake haukuwahi kufanyika.

Anasema sababu mojawapo ikiwa ni kukosekana kwa miongozo ya namna bora ya kuzitambua na taratibu za uendeshaji.

“Ni katika kipindi hiki cha miaka minne, TCU imeandaa miongozo ya uanzishwaji na uendeshaji wa wakala za kudahili wanafunzi wanaotaka kusoma vyuo vilivyopo nje ya nchi.

“Baada ya kutengenezwa kwa mwongozo, TCU imesajili wakala tatu zilizokidhi viwango. Wengine watatu ambao waliomba kusajiliwa hawakukidhi sifa stahiki. Waliosajiliwa ni Global Education Link Ltd, DARWIN Education Agency Ltd na Yuhoma Educational Ltd.

“Wanatakiwa kuhuisha usajili wake kila baada ya miaka mitatu. Pia, Januari na Februari 2020, TCU imepokea maombi ya wengine saba na taratibu za usajili zinaendelea,” anasema.

UCHAMBUZI
NA SABATO KASIKA

# Ili kunusuru mabinti na 'utoro', diwani kujitosa taulo za kike



Diwani wa Kata ya Msigani, Agostino Mushi (kulia), akikabidhi baadhi ya katoni za taulo za kike kwa mwalimu Upendo Mwambona wa Shule ya Msingi Msigani anayeshughulikia nidhamu na malezi ya wanafunzi. **NA MPIGA PICHA WETU**

MOJA ya changamoto zinazowakabili wasichana katika shule za msingi na sekondari na kusababisha washindwe kuhudhuria masomo kikamilifu ni kukosa taulo au pedi ili kujisitiri wakati wa hedhi.

Hali hiyo ilisukuma wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo East Africa Radio na EATV, kuanzisha kampeni ya Namthamini, kwa lengo kuwapatia pedi mabinti hao ili wasikose masomo .

Wanafunzi wa shule za msingi za kata ya Msigani jijini Dar es Salaam, ni miongoni mwa wanaokumbwa na tatizo hilo, huku idadi kubwa ikikosa masomo kutokana na changamoto hiyo.

Mratibu wa Elimu ya Msingi wa Kata ya Msigani, Veronica Mallya, ndiye anayesema hayo wakati wa kupokea pedi kutoka kwa wahisani.

Anafafanua kuwa kata yake ina shule tano za msingi na wanafunzi wa kike 9,320, takribani mabinti 2,000 hukosa masomo kutokana na ukosefu wa taulo hizo.

Anazitaja shule zenye changamoto katika kata hizo ni Msigani, Temboni, Bwawani, Kisiwani na Malamba Mawili na kwamba zote zinakabiliwa na ukosefu wa taulo hizo.

"Kwa wastani idadi hiyo ya wanafunzi hukosa masomo kwa siku tatu hadi tano kwa mwezi wakati wa hedhi, hivyo hii ni changamoto ambayo inahitaji kupatiwa ufumbuzi ili waondokane nayo," anasema Mallya.

Akiwa katika hafla ya kupokea msaada wa taulo za kike kutoka kwa taasisi isiyo ya kiserikali ya Mpakani Tunaweza, Mallya anasema taulo hizo ni kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msigani.

Tukio hilo lilifanyika wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo ilifikia kilele chake Jumapili ya Machi 8 mwaka huu. Anasema, suala la hedhi salama linahusu afya, hiyo taulo hizo zilizotolewa kwa shule moja iwe ni chachu ya kuamsha wadau wengine kuchukua hatua za kuwasaidia wanafunzi wa kike kuondokana na changamoto hiyo.

"Ikiwezekana, hii iwe ni mwanzoni wa kampeni maalum kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule zote za Kata ya Msigani, Mpakani Tunaweza wametuonyesha njia kwa shule moja," anasema.

MANISPAA ZIHUSIKE

Diwani wa Kata ya Msigani, Agustino Mushi, anasema ameguswa na changamoto hiyo inayowakumba wanafunzi wa kike na kusema anataka aifanyie kazi kwa ajili ya kusaidia wanafunzi hao.

Mushi anasema moja ya mipango yake hiyo kuwa ni kuwasilisha pendekezo kwenye vikao vya madiwani wa Manispaa ya Ubungo, ili kuishawishi manispaa hiyo kutenga fedha kwa ajili ya kununulia taulo za kike.

> Shule ianzishe utaratibu huo, kwani kamati za shule zinaweza kukaa na kupendekeza namna ya kuchangia, ili kuhakikisha watoto wa kike hawakosi masomo wanapokuwa katika hedhi.

Fedha anazosema diwani huyo, ni miongoni mwa asilimia 10 ya fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya wanawake na vijana, ili zitumike kununulia taulo za kike kwa shule zote za manispaa ya Ubungo kuanzia msimu wa fedha wa mwaka 2020/2021.

"Ninaamini kwamba pendekezo langu likipita, linaweza kusaidia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa changamoto hii kwa watoto wa kike, ili waweze kuhudhuria masomo bila kukwamishwa na hedhi," anasema Mushi.

Diwani huyo anaongeza kuwa umefika wakati wa kuhakikisha watoto wa kike hawakai nyumbani kwa siku tatu hadi tano kwa sababu ya hedhi, badala yake wawe na taulo hizo, ili waendelee na masomo.

### KUWABAKIZA DARASANI

Mkurugenzi Mtendaji wa Mpakani Tunaweza, Asia Khalifa, anasema, ni bora kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kufanya jambo linawagusa mabinti kwa kuhamasisha jamii kuchangia upatikanaji wa taulo za kike.

"Ndiyo maana tumekuja na kaulimbiu ya ziada kwenye maadhimisho haya kwamba; 'wape watoto wa kike taulo za hedhi wabaki darasani," anasema Asia.

Anaeleza kuwa wadau saba wamechangia upatikanaji wa taulo hizo, na kwamba huo ni mwanzo, na kadri itakavyowezekana, wataendelea kuchangia na pia kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa kuwasaidia wanafunzi wa kike.

"Tunataka hedhi isiwe tatizo la kukwamisha wasichana kwenye masomo, tatizo hili linaweza kumalizika iwapo wazazi kila mmoja atatambua umuhimu wa hilo na hata jamii kwa ujumla wake," anasema.

Mkurugenzi mtendaji huyo anasema, taasisi yake imetoa taulo hizo, lakini pia ni kama kampeni ya kuhamasisha wazazi na jamii kuchukua hatua za kukabiliana na uhaba wa taulo za kike kwa wanafunzi.

Katika maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wanafunzi, walimu, wazazi na viongozi wa serikali, anasema, baadhi ya changamoto za kike ikivaliwa njuga na wadau wote, inaweza kuisha.

### WAZAZI

Mmoja wa wazazi waliohudhuria hafla hiyo ya kukabidhi taulo hizo, Rosemary John, anasema, umefika wakati wazazi na walezi kutobaki nyuma kwenye suala hilo la kuchangia upatikanaji wa taulo za kike.

Anasema, unaweza ukaanzishwa utaratibu maalum wa kuchangia fedha kwa ajili ya kununua taulo na kuzikabidhi shuleni, ili walimu wawe wanawagawia wanafunzi pale wanapokuwa kwenye hedhi.

"Shule ianzishe utaratibu huo, kwani kamati za shule zinaweza kukaa na kupendekeza namna ya kuchangia, ili kuhakikisha watoto wa kike hawakosi masomo wanapokuwa katika hedhi," anasema Rosemary.

Anasema, ukiwapo utaratibu wa kuchangia fedha kidogo, hata wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo wanaweza kuwa na kitu cha kutoa na hatimaye watoto wao kupata taulo hizo.

"Kwa kuwa taasisi hiyo imeonyesha njia, hebu na sisi wazazi tuwe na cha kufanya kwa ajili ya watoto wetu, maadhimisho haya yawe ni ya mkakati wa kuwaisaidia watoto wetu kuondokana na tatizo hili," anasema.

Rosemary anasema, inaumiza kuona wasichana wakikaa nyumbani kwa siku kadhaa bila kwenda shule, kwa sababu ya hedhi, kana kwamba hakuna njia nyingine ya kumsaidia ili ahudhurie masomo.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Elimu ni moja ya haki za mtoto, lakini wapo baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza mwaka huu lakini bado hawajaripoti shuleni. Wadau wanasemaje?



### SALIM MJUNGU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KILA mzazi na mlezi anatakiwa kuhakikisha mtoto wake aliyefaulu kwenda sekondari, anaripoti shuleni.

Rais alishaagiza elimu bure, hivyo wazazi au walezi hawana budi kuacha kutoa visingizio vyovyote vya kuwakamisha kupeleka watoto wao shule.

Wale ambao kwa makusudi hawataki kusomesha watoto wao watakambua kuwa wanawanyima watoto haki ya msingi. Ni wajibu wa mzazi au mlezi kumpa mtoto elimu.

Mtindo huu wa kutopeleka watoto shule inaendekezwa na baadhi ya wazazi na walezi, ambao mimi ninawaona kama hawafai kuitwa wazazi kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo kama wazazi.

Ni ajabu kuona au kusikia katika dunia ya leo kuna wazazi na walezi ambao watoto wao wamefaulu kwenda sekondari, lakini wao wanawaacha nyumbani au wanawaozesha ili kupata mali.

Mtindo huu unataka kuonekana kama wa kawaida, hivyo kuna haja ya kuanzisha utaratibu maalumu wa kuwepo watu wa kufuatilia kwa karibu, katika maeneo yao ili kujua kama kuna watoto waliofaulu halafu hawapelekwi sekondari, basi zichukuliwe hatua za kuhakikisha wanasoma na pia wazazi wao wachukuliwe hatua ambazo kwa namna moja ama nyingine zitakuwa ni mfano kwa wazazi wote wakiwamo wenye mpango wa kuzuia watoto wao kwenda sekondari ili waepuke kufanya hivyo ingawa inawezekana wapo baadhi ya watoto ambao ni watukutu hawataki kabisa kuisikia habari zozote kuhusu shule.



### NIZAR HAZARD (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

HIVI inakuaje mwanafunzi anasoma miaka yote saba halafu kwenda sekondari anakacha? Ninadhani kuna haja ya kufuatilia tatizo hili vizuri ili kujua chanzo chake, kwani inawezekana wazazi wakawa wanahusika katika uzembe huo au watoto wenyewe.

Ninasema hivyo, kwa sababu wapo baadhi ya watoto au wanafunzi, ambao suala la kusoma ni kama mtihani kwao.

Wanaweza kuwa wameanza darasa la kwanza hadi la saba kwa kusukumwa bila kuwa na chochote kichwani labda wakaibia kwa wenzao katika mitihani na kufaulu.

Lakini pia kuna wazazi ambao kusomesha watoto wao wanaona ni kazi ngumu na wanadhani ni bora wakawaacha.

Kimsingi elimu ni moja ya haki muhimu za mtoto awe wa kiume au wa kike, ingawa kuna baadhi ya jamii zinamuona mtoto wa kike kama hafai kupata elimu na badala yake kuwa kitegauchumi cha familia.

Kwa hiyo ni vyema wazazi kutenda mema kwa watoto ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu ambayo ndiyo urithi muhimu katika maisha yao.

Yaani wazazi waweke elimu kwa watoto ili baadaye waavune walichopanda, lakini kama tutaendelea na tabia hii ya kufaulu kisha tunakubali kukaa nao bila kwenda sekondari, tutakuwa hatuwatendei haki.



### MICHAEL MZUNGU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

WALE waliosoma enzi hizo, watakuwa wanajua jinsi ilivyokuwa vigumu kufaulu kwenda sekondari kutokana uhaba wa shule za sekondari na siyo kwamba wanafunzi hawakuwa na akili za darasani.

Yaani ni kwamba kufaulu kwenda sekondari ilikuwa kazi kubwa na unaweza kukuta shule nzima hakuna haat mwanafunzi mmoja aliyechaguliwa kwenda sekondari. Lakini leo shule za sekondari ni nyingi, halafu wanafunzi wanakuwa watoro, kwa nini? Kiwango cha kupenda elimu kimeshuka? Kuna haja ya kutafakari kwa umakini na kulitafutia tatizo hili ufumbuzi wa kudumu, kwani limekuwa likijirudia kila mwaka.

Wanafunzi wanachaguliwa kujiunga sekondari halafu muhula ukianza hawaonekani. Huwa wanakwenda wapi, kufanya nini, kwa sababu gani? Katika tatizo hili wazazi wako upande gani? Yaani kinachofanywa an wanafunzi wa sasa ni sawa na msemo usemao, penye miti hapana wajenzi. Shule zipo za kutosha, lakini wanafunzi hawataki kusoma, wanataka kuwa wa aina gani hapo baadaye?

Niwashauri wazazi pamoja na walezi kwamba umefika wakati wa kuhakikisha wanawapeleka watoto wao shule ili waendelee na elimu kuliko kuwaacha wanaishia njiani kwa sababu za aina yoyote ile, ambayo wao wanadhani ni sahihi kuwafanya watoto wao wasiendelee na elimu ya sekondari na kumbe ni kuwaharibia maisha yao ya baadaye.



### JUSTIN KAILEMBO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

MWAKA huu kumekuwa na vioja vingi kwenye elimu hasa baada ya matokeo ya mtihani wa darasa la saba wa mwaka jana, kutokana na baadhi ya wanafunzi kugoma kwenda kidato cha kwanza kwa madai kwamba hawaba akili.

Sasa hawa walifauluje kama hawana akili? Kuna baadhi ya wazazi kutoka mkoani mkoani Mara walitoa madai hayo mbele ya mkuu wa wilaya Musoma wakisema watoto wamewaambia kuwa hawana akili, hivyo hawawezi kwenda sekondari, kwamba walifanya vibaya katika mtihani wa darasa la saba ili asifaulu, lakini wanashangazwa na matokeo yanayoonyesha wamefaulu na kudai hawako tayari kusoma.

Wazazi wenye watoto wa aina hii ni bora waelimishwe kutambua umuhimu wa elimu ili wawasaidie watoto wao kwa kila njia waweze kusoma kuliko kuwaacha walivyo.

Elimu inamsaidia mtoto kufikia ndoto alizojiwekea kwa ajili ya maisha yake ya baadaye. Lakini anapoachwa afanye anavyotaka, maisha yake ya baadaye yanakosa mwelekeo.

Hivyo niunge mkono juhudi zinazofanywa na viongozi mbalimbali wa serikali katika mikoa na wilaya kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanakwenda sekondari.

Kimsingi elimu ndiyo kila kitu katika maisha, serikali haikukejenga sekondari za kata bure tu bali kwa ajili ya watoto wa Kitanzania, hivyo ni wajibu wa kila mzazi kuona umuhimu wa elimu kwa mtoto wake.



### HAPPY MURUGO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

HAIINGII akilini kuona mwanafunzi amesoma miaka yote saba halafu mwisho wa siku anashindwa kwenda sekondari bila kuwapo kwa sababu zinazoeleweka.

Ni kweli kuna taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari kwamba baadhi ya wanafunzi hadi leo hawajaripoti shuleni tangu shule zifunguliwe Januari mwaka huu na hakuna sababu za kueleweka. Kwa maoni yangu ni kwamba msako unaofanywa na serikali katika mikoa mbalimbali yenye tatizo hilo iendelee kwa nguvu zote na pia raia wema watoe ushirikiano kuweka wazi mambo ili kama wapo wazazi ambao wanachangia kuwapo kwa tatizo hilo, basi wachukuliwe hatua za kisheria, kwani inawezekana wengine wakawa wameolewa au kupewa jukumu la kuchunga ng'ombe na hasa wale wa vijijini na kusababisha wakose haki ya kupata elimu.

Serikali imejitahidi kutoa elimu bure, sasa kwa nini wanafunzi wasisome? Inashangaza kuona wamesoma vizuri kwa muda wa miaka saba kuanzia darasa la kwanza hadi la saba halafu baada ya hapo wanachaguliwa kwenda sekondari lakini hawaendi.

Kuna nini nyuma yake? Sina tatizo na wale ambao huenda wazazi wao wamewahamisha na kuwapeleka katika shule za binafsi, lakini wenzangu na mie ambao wameamua kukaa kimya huku watoto wao hawaendi shule, hao ni wa kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo.



# Wadau ushirika waja juu kisa wabadhirifu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI imeombwa kutunga sheria maalumu ya kulinda ustawi wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (Saccos), ikiwamo kuweka utaratibu wa kushughulikia wabadhirifu wa fedha za vyama hivyo kwa maelezo ustawi wa vyama hivyo kwa sasa unategemea uadilifu wa viongozi.

Aidha, wameomba sheria hiyo iweke viwango maalumu vya tozo ambavyo Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) kwa maelezo kuwa hakuna viwango maalumu na badala yake kila Saccos inakadiriwa kivyake.

Hayo yalisemwa na wadau wa Saccos jijini Mbeya mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya miaka 13 ya kuanzishwa kwa Chama cha Akiba na Mikopo cha Lulu Saccos.

Meneja wa Lulu Saccos, Emmy Ntale, alisema kuna tozo mbalimbali ambazo vyama hivyo vinatozwa na TRA pamoja na taasisi zingine na hivyo vyama vingi vinashindwa kustawi.

"Tunaiomba serikali itunge sheria hiyo ili kulinda vyama vyetu, kwa sasa ustawi wa vyama unahujumiwa sana na baadhi ya viongozi ambao sio waadilifu, lakini sheria ikitungwa viongozi hawa watakuwa wanaogopa kufanya hujuma," alisema Ntale.

Aidha, aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu wa kujiunga na Saccos na kuweka fedha zao mara kwa mara ili kuchochea maendeleo.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Erick Mvati, alisema idadi kubwa ya Saccos katika halmashauri hiyo, vimeshindwa kupata mafanikio kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema katika halmashauri hiyo kuna Saccos 78, lakini inayofanya vizuri ni moja pekee ambayo ni Lulu Saccos, na kwamba zingine zinachechemea na zingine zimekufa.

"Hizi Saccos zina msaada mkubwa kwenye maendeleo ya taifa, zinatoa misaada kwenye shughuli mbalimbali za kijamii, sasa tunatamani zote zilizopo hapa jijini zifikie hatua ilipofikia Lulu," alisema Mvati.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema sababu ya kudhoofika kwa vyama vingi vya ushirika ndani ya halmashauri yake ni viongozi kutokuwa waadilifu.

Alisema viongozi hao wanatafuna fedha za Saccos na kutapanya mali, hivyo alisisitiza serikali itaendelea kushughulika na wabadhirifu.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole (kushoto), akisalimiana na aliyekuwa Diwani wa Kata ya Iyunga jijini humo, Mchungaji Essau Kalinga, ambaye alihamia kwenye chama hicho akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Walimu Mbarali wataka kubadilishana mazingira

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

WALIMU wilayani Mbarali, wameiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwahamisha kwa kubadilishana mazingira kati ya wale wanaofanya kazi mijini na wa vijijini ili kuepuka uwapo wa matabaka kati yao.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Elimu wilayani humo ambayo yalifanyika katika Shule ya Sekondari Rujewa ambapo walidai kuwa baadhi ya walimu wanajulikana kama wa vijijini na wengine ni wa mijini.

Mmoja wa walimu hao, James Pascal, alisema baadhi ya walimu wanaofanya kazi vijijini huwa wakifika mjini wanajikuta wanatumia fedha nyingi kwa vitu ambavyo sio vya msingi kutokana na ugeni wa mazingira.

Alisema kutokana na hali hiyo wanajikuta wanajitengenezea madeni makubwa, ambayo wakati mwingine wanashindwa hata kumudu kuyalipa hivyo akaomba uwekwe utaratibu wa kubadilishana mazingira.

"Kuna baadhi ya walimu wanahamishwa kutoka kijiji kimoja kwenda kingine na mwingine anahamishwa kutoka mtaa hadi mtaa, sasa tofauti iliyopo ni kwamba yule mwalimu wa vijijini akija mjini anaanza kushangaa vitu na wakati mwingine ananunua hata ambavyo hakuviweka kwenye bajeti," alisema Pascal.

Alisema walimu wa vijijini hawana matumizi mengi wakiwa kwenye vituo vyao vya kazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema serikali kwa kushirikiana na wananchi inaendelea na uboreshaji wa mazingira ya elimu.

Alisema wameendelea kushirikiana na wananchi kujenga shule mpya nne za msingi na za sekondari sita pamoja na kuongeza vyumba vya madarasa kwenye shule zenye uhaba ili kuondokana na tatizo la uhaba wa vyumba.

Alisema wanaendelea na ujenzi wa mabweni kwenye shule mbili za sekondari ili kuzifanya ziwe za bweni kwa wavulana na wasichana ili kukabiliana na matatizo ya mimba shuleni.

Akifunga maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema pamoja na mafanikio hayo, wilaya hiyo ina uhaba wa shule za bweni.

# Miundombinu kwenye hifadhi kuboreshwa

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

SERIKALI imeanza kuboresha viwanja vya ndege, barabara na madaraja katika hifadhi za taifa zilizopo katika ukanda wa mikoa ya kusini mwa Tanzania kupitia mradi wa Regrow.

Lengo ni kukuza sekta ya utalii kwa haraka katika ukanda huo ambao una moja ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo ni kubwa zaidi nchini na Afrika Mashariki.

Mradi huo wa usimamizi wa rasilimali kwa ajili ya utalii na ukuaji wake unatekelezwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii katika hifadhi za Nyerere Kusini, Ruaha na utakuwa endelevu kwa hifadhi zingine za Kitulo na Katavi.

Hayo yalibainishwa jana na Kamishna Mwandamizi wa Hifadhi Kanda ya Kusini wa Tanapa, Dk. Chistopher Timbuka, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusiana na jitihada za kuendeleza sekta ya utalii katika ukanda wa kusini.

Dk. Timbuka alibainisha kuwa katika hifadhi pekee ya Ruaha kuna viwanja saba vya ndege, ambavyo vitaboreshwa kwa lengo la kuwawezesha watalii kutua katika moja ya maeneo ya hifadhi wanayotaka kutembelea kwa kuwa hifadhi hiyo ni miongoni mwa hifadhi kubwa nchini na katika Afrika Mashariki na Afrika.

Alisema ni jitihada za serikali za kukuza sekta ya utalii katika mikoa ya ukanda wa kusini zikiwamo za ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege, madaraja na barabara ili kuongeza kasi ya utalii kupitia mradi wa Regrow na jitihada zingine za serikali.

Alisema uunganishaji wa mtandao barabara katika mikoa ya kusini unaofanywa na serikali unaendelea kuchochea kasi ya utalii kutokana na maeneo mengi ya hifadhi kufikiwa na barabara zenye kiwango cha lami.

"Kuna hatua mbalimbali za ujenzi wa barabara zinazofanywa na serikali kwa mfano katika hifadhi ya taifa ya Katavi kuna ujenzi wa barabara kutoka Rukwa hadi Katavi, ujenzi wa barabara kutoka Katavi-Kigoma na ujenzi wa barabara kutoka Tabora-Katavi, zote zitafungua milango ya utalii," alisema Dk. Timbuka.

Pia alisema kunajitihada endelevu za ujenzi wa barabara unaofanywa na serikali kutoka Iringa hadi katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuwa hatua zote hizo zitasaidia kuchochea kwa kasi utalii mikoa ya kusini.

"Mtandao wa barabara kutoka Iringa-Mbeya-Rukwa-Katavi na ujenzi wa bandari ikiwamo ya Karema mwambao wa Ziwa Tanganyika na uwapo wa uwanja wa ndege wa Katavi umekuwa ni msaada mkubwa katika kuchochea utalii kwa mikoa ya kusini, na kuna watalii kutoka nchi jirani zikiwamo za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ambao wamekuwa wakifika kufanya utalii," alisema.

Alisema mbali na mikakati hiyo kuna jitihada za ujenzi wa hoteli yenye hadhi katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi mkoani Katavi kwa lengo la kuchochea utalii.

Pia alisema kuna mpango mkakati wa ujenzi wa malango ya kuingilia katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuwa mpaka sasa wapo katika jitihada za kumtafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya ujenzi wa malango hayo ndani ya mwaka huu.





# Taasisi zaagizwa kujiunga mtandao mfumo ununuzi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TAASISI za umma ambazo bado hazijaunganishwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao (TANePS), zimeagizwa kujiunga na kuanza kutumika kwenye ununuzi kabla ya kufungwa mwaka wa fedha 2019/20.

Hadi sasa taasisi 511 kati ya 540 zimewasilisha kwa njia hiyo mipango yake ya ununuzi kwa mwaka huo wa fedha.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Balozi Dk. Matern Lumbanga, alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka hiyo.

Aliwataka wafanyakazi hao kusimamia kikamilifu matumizi ya mfumo huo na kuhakikisha taasisi zote za umma zilizobaki zinaunganishwa na kuanza kuutumia kwenye matumizi yake.

"Ni imani yangu kuwa mfumo huu utakuwa mwarobaini wa matatizo ambayo yanalalamikiwa kwenye ununuzi wa umma kama vile michakato ya zabuni kutumia muda mrefu," alisema.

Alisema malalamiko mengine ni michakato kutumia pia gharama kubwa, kukosekana ushindani, uwazi na usawa kwenye zabuni na bei kubwa za bidhaa na huduma ikilinganishwa na bei halisi ya soko.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Mhandisi Leonard Kapongo, alisema mamlaka imepata mafanikio mbalimbali ambayo yametokana na usimamizi wa ununuzi wa umma nchini.

"Hadi sasa taasisi 511 kati ya 540 zimewasilisha kwa njia ya mtandao mipango yake ya ununuzi ya mwaka 2019/20, yenye zabuni mbalimbali 31,940 za Sh. trilioni 22.63," alisema.

Alisema hadi sasa watumishi 2,191 kutoka taasisi nunuzi zilizounganishwa na mfumo wamepata mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo huo.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo kushindwa kulipa stahili za watumishi kwa wakati, kutokuwa na ofisi.

Alisema hatua mbalimbali zimechukuliwa kutatua kero hizo na kwa upande wa ofisi katika bajeti ya mwaka ujao 2020/21 imepanga kuanza taratibu za kujenga ofisi zake za kudumu jijini Dodoma.

Alizitaka taasisi ambazo hazijashiriki mafunzo ya mfumo huo kufanya haraka iwezekanavyo kabla ya kuchukuliwa hatua.

Akizungumzia kikao hicho, alisema watapokea, kujadili na kupitisha bajeti iliyopendekezwa kwa mwaka ujao wa fedha 2020/21.



Ofisa Mdhibiti Ubora wa Benki ya NMB tawi la Kongwa mkoani Dodoma, Chausiku Mvungi, akitoa elimu kuhusu utunzaji fedha na kazi za benki hiyo kwa wananchi alipokaribishwa kutoa elimu hiyo wilayani humo mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu Mlawi atoa neno uchaguzi 2020

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

SERIKALI imeombwa kutominya uhuru wa siasa kwa chama chochote cha siasa katika mchakato wa uchaguzi mkuu mwaka 2020 ili uwe wa demokrasia.

Ombi hilo lilitolewa jana na Rais wa Chama cha Maaskofu, Wachungaji, Mitume, Manabii, Wainjilisti na Walimu wa Madhehebu ya Kikristo Tanzania (TPA), Askofu Muss Mlawi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu kongamano la chama hicho litakalofanyika Aprili 16-17, mwaka huu linalotarajiwa kufunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Askofu Mlawi ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Spiritual Pentecostal Tanzania (SPCT), alisema katika kuelekea uchaguzi serikali inatakiwa kuwa makini kwa kutokutumia nguvu kubwa kuvibana vyama vya siasa ili kuwe na demokrasia.

Alisema katika kongamano hilo wataliombea taifa na kuwaombea viongozi pamoja na uchaguzi huo.

"Tutaomba tukimsihi Mungu wetu kuendelea kulifanya Taifa la Tanzania kuwa na amani, umoja, upendo na mshikamano wa kweli katika kipindi cha kuelekea katika uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na Rais," alisema.

Hata hivyo, Askofu Mlawi alisema pamoja na serikali kufanya mambo mazuri ya kimaendeleo na kurejesha nidhamu kwa watumishi, inatakiwa kuwa makini katika kusimamia misingi ya demokrasia, utawala bora na siasa safi.

"Katika kuelekea uchaguzi mkuu serikali isitumie nguvu kubwa kukiminya chama chochote cha siasa kilichopo kwa mujibu wa sheria, demokrasia itumike na wananchi wachague kiongozi wanayemtaka kutoka chama chochote cha siasa na atangazwe kwa mujibu wa mamlaka ya Tume ya Uchaguzi," alisema.

Alisema TPA kinatambua kazi kubwa iliyofanywa na serikali kwenye kujenga barabara, reli, viwanja vya ndege na kutoa elimu bila malipo.

Katika hatua nyingine, Askofu Mlawi aliwaagiza viongozi wa dini nchini kutenga siku maalum ya kuliombea taifa pamoja na uchaguzi ujao.

# Wanafunzi waonywa mapenzi shuleni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WANAFUNZI nchini wametakiwa kuepuka mahusiano ya mapenzi na utumiaji wa dawa za kulevya ili kutimiza ndoto zao kielimu.

Wito huo ulitolewa juzi na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (MNEC), Mussa Mwakitinya, wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ihumwa jijini hapa alipoambatana na Taasisi ya Jasiri Asili kwa ajili ya kutoa elimu ya kujitambua kwa wanafunzi.

Alisema wanafunzi wanapaswa kutumia vyema fursa ya elimu bila malipo kwa kusoma kwa bidii bila kujihusisha na vitendo hivyo.

"Wadogo zangu mna nafasi kubwa kwenye hii dunia, asiwepo mtu yeyote wa kuvuruga ndoto zenu kwa kuwahadaa kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi kwa kuwa mtapata mimba za utotoni na mtashindwa kufikia ndoto zenu," alisisitiza.

Alisema watajiweka kwenye hatari ya kupata magonjwa kama vile virusi vya Ukimwi.

"Niwasihi muepuke vishawishi vyote na mkiona mnasumbuliwa sana toeni taarifa kwa wazazi, walimu na hata viongozi wa kiserikali wa mtaa," alisema.


Alisema ni aibu kuona serikali ikilipa mabilioni ya fedha kwenye elimu ili wanafunzi wasome, lakini wanashindwa kusoma.

"Deni lenu ni moja tu kwa Rais nalo ni kufaulu vizuri na kuondoa historia mbaya ya shule yenu, tangu ianzishwe mwaka 2007 imepata daraja la kwanza kwenye matokeo ya kidato cha nne mara mbili tu," alisema.

Mwanzilishi wa Taasisi ya Jasiri Asili, Diana Msacky, alisema malengo ya taasisi yao ni kutoa elimu ya kujitambua kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi lengo ni kuwakumbusha umuhimu wa wanafunzi kujilinda na vishawishi.

Diana alisema elimu hiyo pia wanaitoa kwa wanafunzi wa kiume ambao wanakumbana na kero mbalimbali na hivyo kushindwa kufikia ndoto zao.

"Hata wadogo zangu wa kiume msikubali kukaa kimya mtu anapowafanyia vitendo viovu vinavyoweza kuhatarisha afya zenu na ndoto zenu, toeni taarifa pindi inapotokea mtu anakufanyia vitendo hivyo ili mamlaka za kisheria ziweze kuchukua hatua," alisisitiza.



# Utafiti wabaini umeme jua kuzalisha megawati 40 Zenji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHIRIKA la Umeme la Zanzibar (ZECO), limesema utafiti wa nishati jadidifu umebaini umeme wa jua una uwezo wa kuzalisha megawati 40 za umeme visiwani humo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja Mkuu wa Shirika hilo, Hassan Mbarouk, alisema utafiti huo uliofanywa na Benki ya Dunia unaonyesha umeme wa jua ni sehemu ya nishati mbadala inayoweza kutumika kwa matumizi mbalimbali na kupunguza kutegemea zaidi uzalishaji wa umeme kutoka Tanesco.

Alisema utafiti mbalimbali umefanywa kwa ajili ya kutafuta nishati mbadala kwa matumizi ya umeme Zanzibar ikiwamo umeme wa jua na upepo.

"Utafiti mbalimbali umefanywa kwa ajili ya kupata nishati mbadala kwa sasa umeme wa mawimbi ya jua ndiyo muafaka utakaozalisha jumla ya megawati 40," alisema.


Hata hivyo alisema kutokana na marekebisho na matengenezo ya njia za kuzalisha umeme, Zanzibar inapata umeme megawati 140 ambao unatosheleza mahitaji ya umeme nchini.

Alizitaja kazi zinazofanyika kwa sasa ni kubadilisha nguzo zilizochakaa ambazo baadhi yake huanguka na kusababisha hasara pamoja na kuweka mita mpya za kisasa za umeme aina ya Luku.

Alisema kazi ya kubadilisha mita za zamani na kuweka za sasa zinatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Machi mwaka huu hatua ambayo italisaidia shirika kukusanya vizuri fedha zake.

"Shirika linafanya marekebisho makubwa ya kazi zake ikiwamo kubadilisha na kuweka mita za kisasa pamoja na nguzo za umeme na kuondoa zilizochakaa," alisema.

ZECO ipo katika maboresho makubwa ikiwamo kujenga uwezo wa ufanisi wa kazi kwa watendaji wake chini ya mradi unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Sweden (SIDA) pamoja na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA).



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia), akisalimiana na Balozi mdogo mpya wa India anayefanyia kazi zake Zanzibar, Bhagwant Singh, alipofika Ikulu, Mjini Zanzibar jana kujitambulisha. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## ZEC yakamilisha taarifa za wapigakura

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imekamilisha kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliokuwamo katika Daftari la Kudumu la WapigaKura kwa wilaya zote 11, Unguja na Pemba.

Akizungumza ofisini kwake, Ofisa Uandikishaji Wilaya ya Mjini, Safia Iddi Muhammed, alisema kukamilika kwa uandikishaji kunatokana na ushirikiano mzuri wa tume na wadau wa uchaguzi kwa kukubali kufuata sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yanayohusiana na kazi ya uandikishaji.

Alisema, ZEC kabla ya kuanza kazi ya uandikishaji iliwapatia mafunzo ya utendaji watendaji wa vituo vya uandikishaji wakiwamo makarani, masheha ambao ni wakala wa Tume na mawakala wa vyama vya siasa jambo ambalo limeifanya kazi hiyo kufanyika katika hali ya amani na utulivu.

Alisema uandikishaji ulifanyika katika hali ya amani na utulivu na wananchi wote waliofika katika vituo waliopatiwa haki yao ili kujiandaa na uchaguzi mkuu.

Alisema tume ilizipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza na hakukuwa na changamoto kubwa ya kukwamisha kazi hiyo.

Kwa upande wao mawakala wa vyama vya siasa walisema wameridhika na uendeshaji wa uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura kwa kuwa kazi hiyo inachukuwa muda mfupi wa wastani dakika moja mpaka mbili kwa mtu mmoja ambaye anahudumiwa kituoni.

Mawakala hao waliishukuru Tume kwa mpango wao huo wa kubadilisha mfumo wa uandikishaji ambao unaendesha kazi kwa haraka zaidi.

Uandikishaji wa wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliokuwamo katika Daftari la Kudumu la Wapigakura ulianza Januari mosi, mwaka huu kwa kuanza na Wilaya ya Michewni na kumalizika Machi 15, Wilaya ya Mjini.

# Z'bar yaridhishwa utekelezaji ilani CCM

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Mapinduzi Mkoa wa Kusini Unguja kimeridhishwa na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM katika miradi ya sekta ya elimu ikwamo ujenzi wa Chuo cha Ufundi Kibuteni ambao lengo utawawezesha vijana kujiajiri.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kusini Unguja, Ramadhan Ali, alisema hayo wakati alipofanya ziara kuangalia maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho Kibuteni, Makunduchi ambao unatekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Alisema ujenzi wa chuo hicho ni muhimu unaokwenda na malengo ya utekelezaji wa ilani ya CCM kuwawezesha vijana kupata ujuzi wa kazi za mikono na kujiajiri.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Kusini ikiwamo Makunduchi, Muyuni na Kizimkazi kujitokeza kwa wingi kutumia fursa za watoto wao kujiunga na chuo hicho kwa ajili ya kupata elimu ya ujuzi wa kazi za ufundi.

"Chama Cha Mapinduzi kimeridhishwa na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho katika ujenzi wa Chuo cha Amali Kibuteni na matarajio yetu makubwa kwamba chuo hicho kitakuwa mkombozi kwa vijana katika kupata ajira zinazotokana na kazi za mikono," alisema.

Alisema ameridhishwa na kazi zinazofanywa na Mwakilishi na Mbunge wa Jimbo la Makunduchi katika kuwaletea maendeleo ikiwamo sekta ya majisafi na salama na uimarishaji wa sekta ya elimu.

"Nimeridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman na mbunge wake ambao wote wanashirikiana kuona maendeleo yanafikiwa katika jimbo hilo," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Madina Mjaka, alisema ujenzi wa chuo hicho ulikuwa umalizike mwaka jana, lakini kutokana na kasoro zilizojitokeza ulichelewa kumalizika.

Alisema ujenzi huo umechelewa kumalizika kwa muda uliopangwa kutokana na tatizo la uhaba wa mchanga ambao unavikabili visiwa vya Unguja na Pemba.

"Ujenzi wa chuo ulikuwa umalizike mwaka jana, lakini uhaba wa mchanga ni moja ya kikwazo kikubwa na tulilazimika kuagiza mchanga kutoka Pemba wenye sifa ya ujenzi wa mradi huu," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman, alisema utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika Jimbo la Makunduchi umefikia asilimia 95 na kazi zilizobaki ni kufikisha umeme katika kijiji cha Muyuni Bandabaya.

# Wazazi lawamani mimba za utotoni

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

BAADHI ya wajumbe wa kikao cha kujadili mikakati itakayotumika kutokomeza mimba za utotoni na wanafunzi mkoani Rukwa wamewalaumu baadhi ya wazazi mkoani humo kuwa chanzo kikubwa cha watoto wao, kujiingiza katika vitendo vya mapenzi na kujikuta wakipata ujauzito kutokana na kutowapa mahitaji muhimu.

Baadhi ya wajumbe wamebainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wakichangia katika kikao cha siku moja kilichoandaliwa na Taasisi isiyo ya kiserikali ya Vijana Pambana Kujiletea Maendeleo Rukwa (Vipamaru) na kufanyika katika ukumbi wa mikutano wa Moravian Conference, uliopo mjini Sumbawanga.

Mmoja wa wajumbe hao, Israel Mwaisaka alisema, changamoto kubwa inayowakuta watoto wanaopata ujauzito wengi wao imebainika kuwa wazazi wao wamewatelekeza kwa kutowapa mahitaji ya muhimu kama chakula, mavazi pamoja na malazi mazuri.

Alisema kuwa kutokana na kukosa huduma hizo baadhi ya watoto hao wanalazimika kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na watu wazima na hivyo kujikuta wakipata ujauzito huku baadhi yao wakiwa ni wanafunzi na hivyo kupoteza ndoto zao za baadaye.

Naye Anna Malisa, mjumbe wa kikao hicho alisema kuwa baadhi ya kinamama hawatimizi wajibu wao katika malezi na kuwaacha watoto wakidhurura bila uangalizi hali inayosababisha baadhi ya vijana wa kiume hasa waendesha bajaji na bodaboda kutumia mwanya huo kwa kuwalaghai watoto wa kike na kuanza nao mahusiano ya kimapenzi.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Rukwa, Dionisia Njuyui, alisema, tatizo lingine ni watoto hao kupenda kufanya ngono, baadhi yao wamekuwa hawasikii mafundisho ya wazazi na hivyo kujiingiza katika mapenzi na kuishia kupata mimba.

Alisema pamoja na changamoto hiyo, bado serikali haikati tamaa ndiyo maana inaruhusu mijadala ya wazi ili kubaini njia ya kukabiliana na tatizo hilo na kuruhusu kuanzishwa kwa taasisi zinazotoa elimu ya kukabiliana na changamoto hiyo.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Vipamaru, Anania Mhalila, alisema taasisi hiyo imeamua kujikita kubaini sababu zinazosababu kuongezeka kwa mimba za utotoni mkoani Rukwa pamoja na mimba kwa wanafunzi katika kipindi cha miezi mitatu ijayo.



Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano Vodacom Tanzania, Rosalynn Mworia, akizungumza na wageni waalikwa kwenye kufunga maadhimisho ya wiki ya ubunifu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kituo chaombea msaada watoto wanaoishi mazingira hatarishi

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

KITUO cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi cha Shalom, kimewaomba wadau kusaidia kupata mahitaji muhimu ikiwamo chakula na kuwezesha ujenzi wa jengo la nyumba ya kuishi.

Akiongea na waandishi wa habari jana katika kituo hicho kilichopo Msangani Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Lilian Mbise, ambaye ni mlezi alisema, kwasasa watoto hao wanaishi katika nyumba ya kupanga.

Lilian alitoa ombi hilo wakati akipokea msaada kutoka kwa kikundi cha Pwani Generation mwanamke sahihi cha Kwamatias. Alisema, kituo hicho kilianzishwa mwaka 2016 kikiwa na watoto wawili na sasa wamefika 18.

Alisema, anashirikiana na Ustawi wa Jamii na Serikali za Mitaa kupata watoto hao ambao wengi ni yatima na baadhi yao walikuwa wanaishi na bibi zao.

Aliomba serikali imsaidie kutatua changamoto mbalimbali ili watoto hao waishi katika mazingira mazuri kama wengine.

"Kwa sasa tumepanga hapa ninapoishi na watoto, ninaomba wadau watakaoguswa wasisite kujitoa kusaidia watoto hawa ni wa wote, tuwasaidie wapate haki kama wengine, tunapowaona wanazurura mitaani tuwasaidie waishi vizuri," alisema.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Betty Msimbe, alisema wamekuwa na utaratibu wa kutoa misaada kwenye vituo vya kulelea watoto kila mwaka.

Alisema, wadau na mashirika wanatakiwa kujenga utaratibu wa kutembelea vituo vya kulelea na kuwasaidia chakula na nguo pamoja na vifaa vya shule ili watoto hao wasijione wana utofauti na wengine.

Kikundi hicho kilitoa msaada wa unga, sukari, mafuta na mchele ambavyo viligharimu zaidi ya shilingi milioni moja

**"Kwa sasa tumepanga hapa ninapoishi na watoto, ninaomba wadau watakaoguswa wasisite kujitoa kusaidia watoto hawa ni wa wote, tuwasaidie wapate haki kama wengine, tunapowaona wanazurura mitaani tuwasaidie waishi vizuri," alisema.**

# Kiama waliokopa fedha za makundi bila kurejesha

**Na Yasmine Protace**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, imejipanga kuanza kuwachukulia hatua wanavikundi waliochukua mikopo isiyo na riba na kushindwa kurejesha.

Zaidi ya shilingi bilioni tatu zilizochukuliwa, mpaka sasa zimerejeshwa Sh. milioni 700.

Hayo yakibainishwa na Diwani wa Kata ya Mabibo, Kassim Lema, katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo katika maadhimisho hayo Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) iliyaandaa maadhimisho hayo kwa kushirikiana na vituo vya Taarifa na Maarifa vya Wilaya ya Ubungo.

Katika maadhimisho hayo ambayo yaliyoangazia zaidi miaka 25 ya Mkutano wa Nne wa Dunia wa Beijing, ambapo baadhi ya washiriki waliopata nafasi ya kuuliza maswali kwa wageni waalikwa, walihoji juu ya wanawake kukosa mikopo ambayo imekuwa ikitangazwa kuwa itatolewa katika halmashauri na kuwazwezesha kinamama, vijana na wenye ulemavu.

Zuwena Juma, alisema wanawake hawapati mikopo japo wanasikia ipo, na kuhoji: "Sasa mwanamke ataweza vipi kijikwamua kiuchumi?"

"Tunaambiwa mikopo ipo katika halmashauri, ambayo inatolewa kwa makundi ya wanawake, vijana na walemavu, mbona hatujawahi kupata," alihoji zaidi.

Diwani Lema alisema mikopo kwa makundi hayo imeishatolewa, ila tatizo wanaochukua wanashindwa kurejesha na kusababisha makundi mengine yasipate kwa wakati.

"Katika Halmashauri ya Ubungo zaidi ya shilingi bilioni tatu zimetolewa kwa ajili ya kuwapatia mikopo kinamama, vijana na wenye ulemavu, lakini makundi hayo bado hayajarejeshea pesa," alisema.

Alifafanua kuwa kati ya o hizo zaidi ya shilingi bilioni tatu, zilizotolewa, wanawake walipata Sh. bilioni 1.6, vijana Sh. bilioni 1.5 na wenye ulemavu shilingi milioni 180, na kwamba kiasi chote cha pesa ni asilimia 10 ambayo inatolewa na halmashauri kwa makundi hayo kutoka vyanzo vya ndani vya mapato yake.

Aliongeza kuwa kamati zimeshakutana na kujadili hatua ambazo zitachukuliwa dhidi ya waliochukua mikopo na kushindwa kuirejesha.

## HABARI KIMATAIFA

# Wapigakura wakumbwa na hofu ya virusi vya corona

**PARIS,** Ufaransa

UFARANSA iko katika mchakato wa kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa, lakini wananchi wameingiwa na hofu ya kushiriki kutokana na hofu ya ugonjwa virusi vya Corona.

Wapiga kura watawachagua mameya wa mabaraza 35,000 ya miji, vijiji na Mji Mkuu wa Paris na karibu madiwani nusu milioni katika uchaguzi unaofanyika wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona na pia wakati ambapo wasiwasi umeongezeka nchini humo juu ya siasa za nchini humo.

Wakati huo huo, Ufaransa na Hispania zimetangaza hatua za dharura na kuzifunga huduma kadhaa ili kuzuia kuenea virusi vya ugonjwa wa Corona.

Ufaransa inatarajia kufunga maduka, migahawa na sehemu za burudani muda wowote na watu wapatao milioni 67 wanaoishi nchini humo wametakiwa wakae nyumbani kama hatua mojawapo ya kusaidia kupambana na virusi vya corona vinavyosambaa kwa haraka ambapo idadi ya watu walioambukizwa nchini humo imeongezeka mara mbili katika muda wa saa 72.

Waziri Mkuu wa Ufaransa, Edouard Philippe (pichani chini) alisema serikali haina jinsi nyingine isipokuwa kuchukua hatua ya namna hiyo baada ya idara ya afya ya umma kutangaza kuwa watu 91 wamekufa na karibu watu 4,500 wameambukizwa hadi kufikia sasa.

Nchini Ujerumani mamlaka ya Mji Mkuu, Berlin na ya Jiji la Cologne katika jimbo la North Rhine Westfalia zimetangaza kufungwa baa, vilabu vya starehe, majumba ya sinema na kumbi za matamasha wakati ambapo Ujerumani inaongeza juhudi za kupunguza kasi ya kuenea kwa virusi hivyo.

Kuanzia sasa hafla yoyote inayowahusisha watu 50 au zaidi katika mji wa Berlin imepigwa marufuku. **DW**



# Madaktari wanaotibu corona wagoma

**NAIROBI,** Kenya

WAUGUZI wanaofanya kazi katika wodi iliyotengwa kwa watu walioambukizwa virusi vya corona nchini Kenya wameanza mgomo baridi kulalamikia kile wanachodai kuwa ukosefu wa vifaa vya kujikinga na mafunzo ya kutosha.

Hospitali ya Mbagathi katika Mji Mkuu wa Nairobi, ni moja ya hospitali zilizo na wodi ya kutibu wagonjwa waliombukizwa virusi hivyo hatari.

Katibu Mkuu wa muungano wa wauguzi nchini Kenya, Seth Panyako alisema kwamba wauguzi watarejea kazini ikiwa watapewa mavazi maalumu na mafunzo ya jinsi ya kuwashughulikia wagonjwa.

"Wahudumu wa afya wako katika hatari ya kupata maambukizi katika mazingira yao ya kazi," alisema Panyako na kuongeza:

"Bila ya kuwa na vifaa maalumu, wanatarajiwa kujilinda vipi wakiwa kazini? na wanaporejea nyumbani kutangamana na familia zao?" alisema Panyako.

**Watu wengine wawili walioambukizwa virusi hivyo wamepelekwa katika hospitali ya kitaifa wa Kenyatta ambako mgonjwa wa kwanza aliyethibitishwa kuambukizwa anapewa matibabu.**

Hospitali ya Mbagathi imewazuia watu 22 ambao walitangamana na mgonjwa wa kwanza aliyeambukizwa virusi vya corona.

Watu wengine wawili walioambukizwa virusi hivyo wamepelekwa katika hospitali ya kitaifa wa Kenyatta ambako mgonjwa wa kwanza aliyethibitishwa kuambukizwa anapewa matibabu.

Kenya kwa sasa inakabiliwa na kibarua kigumu cha kuwatafuta wale waliotangamana na watu watatu waliothibitishwa kuambukizwa virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, Msemaji wa serikali, Cyrus Oguna alisema serikali itatoa maelezo zaidi shughuli hiyo imefika wapi.

"Kwa kweli kuna changamoto zipo na tunakubali mazingira yetu yataratibu wa kuweza kujua mtu anaishi wapi," alisema Oguna.

Hata hivyo, alitoa wito kwa watu ambao huenda wametangamana na wagonjwa watatu walioambukizwa virusi hivyo kufika katika kituo cha afya kilicho karibu nao.

Serikali ya kenya imewafahamisha raia kwamba hakuna haja ya kuwa na hofu licha ya kuthibitishwa kwa kisa cha kwanza cha mgonjwa wa Corona.

Kwa sasa ni kwamba hakuna haja ya kununua kwa wingi kemikali za kuosha mikono zinazoua viini kwa haraka au hata kununua bidhaa kwa wingi kwasababu ya hofu ya ugonjwa huu. **BBC**




Hatua muhimu za kuzingatia ili kujikinga na ugonjwa wa virusi vya Corona. **PICHA: MTANDAO**

# Mbabe wa kivita amaliza kifungo

**KINSHASA,** Congo

ALIYEKUWA kiongozi wa waasi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Thomas Lubanga, ambaye alikuwa mtu wa kwanza kukamatwa na kufungwa jela na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), ameachiliwa huru na mahakama ya Makla jijini Kinshasa baada ya kumaliza kifungo chake cha miaka 14.

Lubanga alipatikana na hatia kwa makosa ya ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwamo mauaji na ubakaji wa raia na kuwatumia watoto wakati akiongoza kundi la waasi la UPC kati ya mwaka 1997 hadi 2007 katika jimbo la Ituri.

Julai 2010, majaji waliisimamisha kesi ya Thomas Lubanga kuhusu makosa ya uhalifu wa kivita na kuamuru aachiliwe huru baada ya waendesha mashtaka kukataa kuwasilisha taarifa kwa upande wa utetezi. Lubanga alikana mara kadhaa kutumia watoto kama wanajeshi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuanzia mwaka 2002 hadi 2003.

Thomas Lubanga aliyekuwa kiongozi wa wanamgambo wa Union of Congolese Patriots-UPC aliongoza wanamgambo wa kabila la Hema kupigana dhidi ya watu wa kabila la Lendu.

Ghasia za kugombea ardhi ziligeuka na kuwa vita vya kikabila ambapo takriban watu 50,000 waliuawa na maelfu walibaki bila makazi. **RFI**

## Biden, Sanders wamkosoa Trump

**WASHINGTON,** Marekani

MAKAMU wa zamani wa Rais wa Marekani, Joe Biden na Seneta wa Jimbo la Vermont, Bernie Sanders jana wameshiriki katika mdahalo wa ana kwa ana kwa mara ya kwanza.

Biden na Sanders wanaowania kuchaguliwa katika kura za mchujo za kugombea urais kwa tiketi ya chama cha Democratic wamekutana katika mdahalo wa 11 ambao ulihamishwa kutoka Arizona, kutokana na hofu ya kuenea kwa virusi vya corona na ambao ulifanyika bila ya kuwa na watazamaji.

Baada ya kukutana katika ukumbi unakofanyika mdahalo huo mjini Washington, wagombea hao wawili walisalimiana kwa kugonganisha kiwiko. **DW**

# Waomba ajira zaidi kwa wakunga

**Na Elizabeth Zaya**

MUUNGANO wa Utepe Mweupe (Rwatz) umeiomba serikali kuajiri wakunga katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma ya afya, ili wasaidie katika kitengo cha huduma za uzazi.

Ombi hilo lilitolewa na Mratibu wa Muungano huo, Rosemary Mlay, katika maadhimisho ya siku ya Utepe mweupe ambayo kitaifa yalifanyika jijini Dar es Salaam.

Mlay alisema ni vema serikali ikaajili wakunga wa kutosha angalau kila zahanati wawe watano, kituo cha afya nane, hospitali ya wilaya 20 na kila hospitali ya mkoa 102.

"Wakunga hawa wasifanye idara nyingine zaidi ya ukunga na masuala yote yanayohusiana na mambo ya uzazi wa mpango, kliniki ya wajawazito kabla na baada ya kujifungua na kuhudumia watoto walio chini ya umri wa miaka mitano," alisema Mlay.

Aliongeza: "Pia tunaomba serikali za mitaa ziweke bajeti ya hawa wakunga na wasiwahamishe. Faida ya kutokuwahamisha ni pamoja na kuwasaidia kuendelea kutengeneza mazingira bora ya kufanya kazi hiyo, mkunga mwenye stadi za kazi wakati wote lazima ahakikishe kwamba kila kitu kinachohitajika kwenye uzazi kinakuwapo wakati wote."

Alisema pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kuboresha huduma ya uzazi, lakini bado kunahitajika kuendelea kuboresha mazingira ya kuwahakikishia uzazi salama wanawake wanaojifungua na kupambana na vifo visivyo vya lazima.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alisema serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha huduma za uzazi na kwamba itaendelea kuboresha zaidi ili kumaliza kabisa vifo vinavyokana na uzazi huo kwa kinamama na watoto.

Pia, aliwaomba wakina mama pamoja na wananchi wote kuachana na tabia ya kuwapatia fedha wahudumu wa afya ili wapewe huduma bora.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kushoto), akiangalia miundombinu ya barabara, iliyoharibika wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani juzi, akiwa katika ziara ya kukagua miundombinu mbalimbali mkoani humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Mkuu Majaliwa awataka wasichana kusoma kwa bidii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia wilayani Ruangwa wasome kwa bidii kwa sababu serikali imewaboreshea mazingira na kuwaepusha na vishawishi.

"Mawazo na akili yenu yote iwe katika kusoma tu, tunataka kuona mkiendelea kusoma hadi kidato cha tano na sita ili ndoto zenu za kufika vyuo vikuu zitimie."

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na walimu na wanafunzi alipotembelea na kukagua maendeleo ya shule hiyo mkoani Lindi.

Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia ni ya bweni na ilibadilishwa kutoka shule ya msingi Mnacho, ambayo ilianzishwa mwaka 1932 na Shirika la Wamisionari Wakatoliki chini ya Mwalimu Lucas Malia.

Waziri Mkuu ambaye alisoma katika Shule Msingi Mnacho kabla ya kubadilishwa, alisema mwaka 2017 alitembelea shule hiyo na kukuta majengo yamechakaa, ndipo alipotafuta wadau na kuyafanyia ukarabati.

"Nilikuta hata jengo ambalo nilisomea lilikuwa limechakaa, tulitafuta fedha na kukarabati ikawa mpya. Tuliamua kufanya mabadiliko kwa kuzingatia watoto waliokuwa wakisoma hapa walikuwa wanatoka kijiji cha Ng'au na kipindi cha mvua walishindwa kuja shule kutokana na mto kujaa maji."

Waziri Mkuu aliongeza kuwa baada ya kubadilisha shule hiyo na kuwa ya sekondari ya wasichana walijenga shule ya msingi katika kijiji cha Ng'au na kuwahamishia watoto waliokuwa wakisoma Shule ya Msingi Mnacho.

Amesema katika Wilaya ya Ruangwa hakukuwa na shule ya sekondari ya wasichana, hivyo amefarijika sana kuona watoto wa kike wakianza kusoma kidato cha kwanza kwenye shule hiyo ya bweni.

Waziri Mkuu alisema lengo ni kuhakikisha shule hiyo inakuwa na kidato cha tano na sita kwa sababu ina vyumba vya madarasa na mabweni ya kutosha. "Kuwapo kwa kidato cha tano na sita kutawaongezea ari ya kusoma wanafunzi wengine."

Wanafunzi wanaosoma kwenye shule hiyo waliishukuru serikali kwa kuanzisha shule hiyo kwa kuwa imewaepusha na vishawishi.

Wakizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzao, Sharifa Mbunga, Irene Mkuti, Ikra Jirani na Mwanayazi Omary walisema uwapo wa shule hiyo utaongeza ari ya kusoma kwa wanafunzi wa kike wilayani Ruangwa, hivyo wameahidi kusoma kwa bidii.

Kaimu Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Gladness Makongwa, alisema shule imedahili wanafunzi 75 wa kike waliopata ufaulu wa juu kutoka kata zote zilizo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

# Rita kusajili wanafunzi Sengerema

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

MKUU wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, amezindua kampeni ya kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa katika wilaya hiyo, huku akiwataka watendaji wawajibike ipasavyo kuhakikisha zoezi hilo linakamilika.

Pia amepongeza Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi na kuwafuata kule wanakoishi badala ya kuwasubiri ofisini.

Uzinduzi huo ulifanyika jana katika Shule ya Sekondari ya Sengerema ambapo pia yanaendeshwa mafunzo kwa waratibu elimu wa kata zote za wilaya hiyo, ambapo kila mmoja ataratibu kampeni hii katika eneo lake kwa kushirikiana na walimu wakuu.

Kipole alisema kwa muda mrefu wananchi wengi wameishi bila kuwa na utambulisho rasmi na ndiyo maana hivi sasa serikali imeweka msukumo wa kuhakikisha kila mwananchi anatambulika.

Aliongeza kuwa utambulisho ni suala la msingi na katika nchi zilizopiga hatua katika suala hili hata fursa za mikopo zimekuwa rahisi kutokana na kila mwananchi anatambulika.

Alisema kampeni hiyo itapunguza msongamano wa wananchi katika ofisi yake kila mara inapofika kipindi cha mwisho wa mwaka wanafunzi wanapokaribia kuanza kidato cha kwanza ambapo cheti cha kuzaliwa kinahitajika.

"Kampeni hii ni mkombozi kwa wananchi kwani itawapunguzia wananchi usumbufu waliokuwa wanaupata kwa kutumia gharama nyingi na muda mrefu kufika katika ofisi yake kwa ajili ya kusajiliwa na kutolea mfano wa eneo la Soswa katika Halmashauri ya Buchosa ambapo nauli ya mtu mmoja kuja na kurudi makao makuu ya Wilaya ni Sh. 28,000 na akiambatana na mtoto anayesajiliwa inakuwa mara mbili ya hiyo hivyo ni mzigo mkubwa kwa wananchi," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

## KUPOTEA KWA CHETI



115670202

**MAGONGO M. MAGONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0823-0115** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia THAAQAFA SEKONDARI mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAB/RB/4565/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115670702

**KRISENT DAUDI KRISENT anatangaza** kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3587-0139** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAGUGU SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIL/RB/232796/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUKAS KISHIMBE KITAPELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 762 DEG** aina ya **TOYOTA CRESTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi: **KAH/TR/RB/113/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN LUKIMBILO MWANGOMBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 883 BHS** aina ya Mitsubish Canter rangi ya Multicolour. Chassis namba **FE648G531006.** Engine namba **4D35G61209.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **SMT/RB/6718/18.**

115415802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KENNY FELIX SAMILLAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 925 DRV AINA YA SCANIA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/234188/2020.**

115670902

## KUPOTEA KWA VYETI



115670102

**MASUMBUKO BUNDALA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0131-0073** kilichotolewa Baraza la Mithihani mwaka 2005 katika Shule ya Sekondari Mazengo na cheti cha sita index namba **S0110-0612** kilichotolewa Baraza la Mithihani mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Ilboru. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MAJ/RB/15/2020**

## KUPOTEA KWA KADI

**Filomena S. Njau** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania,yenye usajili namba **MC 644 CAW** aina ya **TVS.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/GOG/RB/233772/2020**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# FERNANDES MCHEZAJI BORA WA FEBRUARI



**LONDON,** England

KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes, ametajwa kuwa mchezaji bora Februari kwenye Ligi Kuu ya England, ikiwa ameanza kucheza ligi hiyo Februari Mosi mwaka huu baada ya kusajiliwa Januari akitokea Sporting CP.

Fernandes haraka aliinyanyua United ambayo ilikuwa na matokea mbaya kuanzia Desemba na Januari na mchezo wake wa kwanza ulikuwa dhidi ya Wolves ambao ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Baada ya hapo akaiondoa timu kwenye mechi za ushindi mfululizo dhidi ya Chelsea na Watford mwanzoni mwa Februari.

Katika mechi zote hizo za ushindi, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu, akifunga kwa penalti.

Na Fernandes mwenye amebainisha kwamba, ameridhishwa na namna alivyoanza vizuri kuichezea United klabu ambayo ilikuwa ndoto yake tangu utoto.

"Tangu nilipokuwa mtoto ndoto yangu ilikuwa kuichezea Man Utd, na kucheza hapa kwenye uwanja wa Old Trafford ni ndoto kubwa katika maisha yangu ya soka," alisema Fernandes akinukuliwa na PremierLeague.com.

"Unapokuja kwenye klabu mpya mara zote unataka kufunga, bao la kwanza linakuwa la aina yake. Haijalishi namna gani umefunga, lakini goli lenye thamani kubwa katika maisha yako.

"Nina furaha na namna nilivyoanza, lakini kuanzia sasa nataka kuwa bora zaidi."

# Serie A kurudishwa Mei 3

**ROME,** Italia

SHIRIKISHO la soka la Italia limepanga kuirudisha Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Mei 3 mwaka huu, wakati rais wa chama hivyo akiwa ameomba kusogezwa mbele kwa mashindano ya Euro 2020.

Ligi zote za soka barani Ulaya zimesimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na Italia ndio nchi iliyoathirika zaidi barani humo pamoja na England, Ufaransa, Ujerumani na Hispania.

UEFA leo Jumanne watakutana kwenye mkutano wa dharura kwa ajili ya kujadiliana uwezekano wa kuizogeza mbele michuano ya Euro 2020, baada ya kusimamishwa kwa ligi na kuzipa nafasi ya kumalizia ratiba zao.

Na Rais wa Shirikisho la soka la Italia, FIGC, Gabriele Gravina – ametaka kuahirishwa kwa mashindano ya Euro 2020 ili kuwapa nafasi ya kumaliza mechi za Ligi Kuu.

"Tumewaomba UEFA wasogeze mbele mashindano ya Ulaya," alisema Gravina akinukuliwa na Sky Sports."





# Chelsea yamuadhibu Mount kwa uzembe wa kujikinga na corona

**LONDON,** England

CHELSEA inatarajia kumuadhibu kiungo Mason Mount kwa faini kali baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa 21 kuonekana akiwa hadharani baada ya kutakiwa kujitenga.

Wachezaji wa kikosi chote cha Chelsea wametakiwa kujifungia majumbani mwao baada ya mchezaji mwenzao, Callum Hudson-Odoi kupigwa na kugundulika na virusi vya corona, huku klabu hiyo ikisisitiza ushauri wote uliotolewa na serikali juu ya kujikinga na maambukizi hayo kufuatwa.

Hata hivyo, gazeti la The Mirror lilibainisha kwamba, Mount alikaidi agizo hilo na alionekana akitaniana na kiungo wa West Ham United, Declan Rice.

Rice hajawekwa kwenye karatini na hataadhibiwa na klabu yake, lakini Mount hakutakiwa kuwa nje kwa sababu alikutana na Hudson-Odoi mwenye virusi hivyo na hivyo anaweza kuvisambaza.

Msemaji wa klabu hiyo amesema 'watatakiwa kumkumbusha Mount majukumu yake', kwa faini kali na maneno makali kutoka kwa kocha wake, Frank Lampard.

Hudson-Odoi amethibitishwa kwamba, anajisikia vizuri baada ya kuwa mchezaji wa kwanza wa Ligi Kuu ya England kupatikana na virusi vya corona.

HABARI MICHEZO

# Rooney atoa somo kwa wachezaji vijana

**LONDON,** England

WAYNE Rooney amesema elimu zaidi na taarifa inahitajika kwa wachezaji soka vijana kwa ajili ya kujifunza namna ya kujiendesha wao wenyewe kwenye mitandao ya kijamii.

Kiungo huyo wa Derby County, Rooney ni mmoja wa nyota wenye wafuasi wengi kwenye mitandao ya kijamii, ambapo kwenye twitter wapo milioni 17.1 na kwenye Instragam ana wafuasi milioni 14.9 na facebook milioni 24.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amebainisha kwamba alijifunza namna ya kujilinda kwenye kurasa za mitandao ya kijamii wakati akiwa na umri wa miaka 18, lakini amesema kwa sasa ni muhimu kwa sababu ni suala linalosababisha uchizi kwa wachezaji vijana.

Rooney alisema kupitia gazeti la Sunday Times: "Changamoto kubwa inayowakabili wachezaji vijana kwa sasa ni mitandao ya kijamii.

"Mitandao ya kijamii ni mizuri kwa upande mmoja, lakini ni hatari kubwa zaidi kwa wachezaji vijana na wanatakiwa kufundishwa namna ya kuitumia.

"Baadhi ya ujumbe wanaouweka humo ni mzuri, lakini wanaweka wakazi ambao sio sawa na klabu zinatakiwa kuwasaidia wachezaji vijana katika hilo.

"Nilikuwa huko wakati nikiwa kijana na kuweka vitu vya tofauti tofauti kwenye Twitter. Nafikiri ni vizuri wachezaji kujifunze namna bora ya kutumia mitandao hiyo."

Dele Alli mwenye umri wa miaka 23, alipigwa faini na FA baada ya kuposti kwenye Snapchat picha akimzomea kijana wa Kiasia na kumtania kuhusu mlipuko wa virusi vya corona.

Pia kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva, aliadhibiwa kwa kuweka kwenye twitter picha ya mchezaji mwenzake, Benjamin Mendy pamoja na sura ya chokoleti ya Kihispania, Conguitos, ambayo ina rangi nyeusi ikiwa ni kama ubaguzi wa rangi, Septemba mwaka jana.






# VIRGIL AHOFIA MASHABIKI LIVERPOOL KUTOUONA UBINGWA

**LIVEPOOL,** England

VIRGIL van Dijk amesema atakuwa "amejiandaa kuwakilisha" kama mlipuko wa virusi vya corona utawazuia mashabiki wa Liverpool kuiangalia timu yao ikishinda taji la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Ligi Kuu ya England imesimamishwa hadi Aprili 4, huku Liverpool wanaongoza kileleni mwa msimamo kwa pointi 25.

Licha ya kujotulikana kwa hatima yake, au kama msimu utamalizika, Van Dijk amebainisha kupeleka taji kwa mashabiki wa Liverpool.

Ameliambia gazeti la Uholanzi:"Kama tutashinda kwenye uwanja usio na mashabiki na mashabiki hawakuwa pale, nitawawakilisha.

"Kwa kawaida, kama hakuna mashabiki kwenye uwanja wa Anfield, litakuwa pigo kubwa, hakuna anayetaka kucheza bila mashabiki.

"Ni wazi kwamba, kila shabiki anataka kuona timu yake wakati inatwaa ubingwa, hivyo mimi nitawawakilisha mashabiki."

# *Arteta: Najisikia vizuri kwa sasa*

**LONDON** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta "tayari anajisikia vizuri" baada ya kukutwa na virusi vya corona na ameishukuru Ligi Kuu ya England kwa kuahirisha mechi zake.

Klabu hiyo ya hapa London ilithibitisha Alhamisi kwamba, Arteta alikutana na kugusana na mtu mwenye virusi vya corona, na kulazimika kufungwa uwanja wao wa mazoezi wa Colney uliopo pale London.

Maofisa wa Ligi Kuu ya England walikutana kwa dharura Ijumaa na kuamua kusimamisha Ligi Kuu hadi Aprili 3.

Arteta aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter Ijumaa kutoa shukurani zake baada ya kupatikana na virusi vya corona.

"Shukrani kwa maneno yenu na sapoti," alisema. "Tayari najisikia vizuri. Tunakabiliwa na changamoto kubwa kwa sasa."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SHEARER ATAKA LIVER WASIPEWE UBINGWA EPL

●●● Wanahitaji pointi sita tu kubeba taji, lakini hawajazipata na kwa sababu hiyo...

**LONDON,** England

LIVERPOOL haiwezi kupewa taji la Ligi Kuu ya England kama msimu haujamalizika kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, kwa mujibu wa Alan Shearer.

**Tayari mjadala umeanza juu ya nini kitatokea kama Ligi Kuu ya England, ambayo imesimamishwa hadi Aprili 3, kama haitaendelea.**

Liverpool wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya England kwa pointi 25, huku Manchester City ikiwa ina mchezo mmoja mkononi na mechi tisa zikiwa zimebakia msimu kumalizika.

Lakini Shearer, mfungaji wa wakati wote wa Ligi Kuu ya England, amesema hakuna namna kwa Liverpool kupewa taji la Ligi Kuu kama msimu haujaisha.

"Kama msimu haujamalizika hakuna namna yoyote unaweza kuwa mshindi au kupoteza," ameandika Shearer kwenye gazeti la The Sun.

"Wakati mgumu na wa hatari kwa baadhi ya klabu, si zaidi ya Liverpool, ni matokeo yake ndio muhimu.

"Kama huwezi kushindana kwenye ratiba, hivyo huwezi kupewa taji kwa urahisi tu au kumfanya mtu yoyote ashuke daraja."

Liverpool wanatakiwa washinde mechi mbili tu za ligi na wataweza kutwaa taji la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Lakini Shearer amesema hata kama vijana hao wa Jurgen Klopp walikuwa wanapanga kutwaa taji hilo, hawawezi kupewa.

"Kwa Liverpool, itakuwa ni ngumu," aliendelea. "Lakini sioni namna ambayo itakuwa sawa kwao kupewa taji, licha ya ukweli kwamba hakuna atakayeweza kuwafikia.

"Wanahitaji pointi sita tu kubeba taji, lakini hawajazipata na kwa sababu hiyo haiwezekani wakapewa kirahisi hivyo. "Ingekuwa tofauti kama ligi ingesimamishwa wakati tayari wameshapata pointi hizo. Lakini hawajazipata na kwa uhakika litakuwa jambo la ajabu."

## ZISIKUPITE

### IGHALO KUPUNGUZIWA MSHIKO

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Nigeria, Odion Ighalo,30, ambaye yuko klabu hiyo kwa mkopo, anajiandaa kupunguziwa mshahara hadi pauni milioni sita kwa mwaka ili abakie klabuni hapo. ***(Daily Mail)***

### RONALDO KUFUNGWA JUVE

JUVENTUS wanajiandaa kumpa ofa Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, ili kuongeza mkataba wake na miamba hao wa Italia hadi mwaka 2024. ***(Tuttosport)***

### KANE KUZIPOTEZEA UTD, CITY

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na timu ya Taifa ya England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 26, anafikiria kukataa uhamisho wa kwenda Manchester United au Manchester City ili ajiunge na Juve. ***(Tuttosport)***

### BRUYNE, STERLING KUITESA CITY

KLABU ya Manchester City inatumia muda wa kusimamishwa kwa Ligi Kuu ya England kufanya mazungumzo ya kuongeza mkataba na kiungo, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 28, pamoja na winga wa England, Raheem Sterling mwenye miaka 25. ***(Sun)***

### LONGSTAFF LULU NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imeanza mazungumzo ya kumpa mkataba mpya, kiungo wa kimataifa wa England, Matty Longstaff mwenye umri wa miaka 19. ***(Star)***

### VAN DE BEEK SAFI UTD

KLABU ya Manchester United ina nafasi nzuri zaidi ya kumsajili kiungo wa Ajax, Donny van de Beek, huku Real Madrid wakipanga kumkosa mchezaji huyo wa kimatafa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 23. ***(Marca)***

### ARTETA KUIBOMOA WEST HAM

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anafikiria kumsajili beki wa West Ham United, Issa Diop , 23. Mfaransa huyo thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 60 pia anawaniwa na Manchester United. ***(Metro)***

### UEFA KUIVUTA NUSU FAINALI

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), linafikiri nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ile ya Europa kuchezwa kwa simu nne kwa ajili ya kurahisisha michuano hiyo ili kuendana na ratiba baada ya kusimamishwa kutokaa na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Telegraph)***

### LIVER BADO INAYE WIJNALDUM

LIVERPOOL imefikia pazuri katika mazungumzo ya kumpa mkataba mpya, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 29, ili raia huyo wa Uholanzi akae hapo Anfield hadi mwaka 2023. ***(Star)***

### MOUNT KUADHIBIWA CHELSEA

KIUNGO wa Chelsea, Mason Mount mwenye umri wa miaka 21, anaweza kukabiliwa na faini na klabu hiyo baada ya kupigwa picha akionekana akitaniwa na nyota wa West Ham, Declan Rice kwenye sehemu ya kupaki magari, wakali alitakiwa kuwa peke yake. ***(Mirror)***

### DOGO WA UTURUKI LULU ULAYA

TIMU za Barcelona, Manchester United na Real Madrid zipo kwenye mbio moja ya kumwania kiungo wa Fenerbahce na timu ya Taifa ya Uturuki chini ya umri wa miaka 17, Omer Beyaz, 16. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

## Ndanda yapania za Nangwanda tu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ndanda FC, Abdul Mingange, amesema wakati huu Ligi Kuu Bara ikielekea mwishoni, mapambano yao wanayaelekeza katika michezo yao ya nyumbani.

Ndanda ambayo imetoka kuchezea kichapo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Tanzania Prisons, kesho itaikaribisha Biashara United katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, iliyotoka kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mingange alisema kwa sasa wanapambana kushinda mechi zao za nyumbani ili kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo.

Alisema kwa mwelekeo wa ligi kipindi hiki cha lala salama, kila timu inapambana kushinda katika uwanja wa nyumbani.

"Biashara ni timu nzuri, hivi karibuni imepata matokeo mazuri, hivyo wanakuja nyumbani na sisi hatujawahi kupoteza kirahisi kwetu," alisema Mingange.

Alisema hawataibeza Biashara United na wamejipanga vizuri kuhakikisha wapinzani wao hao wanaacha alama zote tatu.

## Hererimana atoa siri KMC kupaa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Haruna Hererimana, amesema siri ya timu yake kushinda michezo yake minne mfululizo ni kutokana na kubadilisha mfumo mzima wa timu alioukuta pamoja na kutoa vitu ambavyo vilikuwa vinachangia kwa kiasi kikubwa kuididimiza klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana asubuhi, Hererimana alisema, anashukuru baada ya kukaa na uongozi wa klabu hiyo alishauri baadhi ya vitu vitolewe na baadhi viongezwe ili kuiimarisha klabu hiyo ambayo ameikuta ikiwa katika wakati mgumu kimatokeo.

"Nashukuru mpaka sasa timu yangu ilipofikia kwa sababu nilikuta kuna hali mbaya sana, lakini nashukuru vitu ambavyo nimevifanya vimeleta mabadiliko makubwa kuanzia kwenye benchi la ufundi mpaka kwa wachezaji," alisema Haruna.

Alisema ametumia nguvu nyingi mpaka kuifikisha KMC ilipo sasa, na anawashukuru mashabiki pamoja na wadau mbalimbali wa mchezo huo kwa sapoti kubwa waliyompa tangu aanze kuitumikia klabu hiyo kazi ambayo anadai ilikuwa si rahisi.

# MIRAJI ATOA MATUMAINI KUREJEA TENA SIMBA

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukaa chumba cha majeruhi kwa muda mrefu, hatimaye mshambuliaji wa klabu ya Simba, Miraji Athumani amesema "namshukuru Mungu kwa sasa hali yangu inaendelea vizuri licha ya kufanya mazoezi peke yangu".

**Akizungumza na Nipashe jana, Miraji alisema anaendelea vizuri na kuwataka mashabiki wake waendelee kumwombea atakaporejea dimbani aweze kuendeleza makali yake.**

"Nashukuru siku zinavyozidi kwenda hali yangu inazidi kuimarika tofauti na kipindi cha nyuma, kikubwa ni kuomba Mungu niweze kurudi kwenye hali yangu ya kawaida kama nilivyokuwa mwanzo naomba mashabiki wangu wazidi kuniombea," alisema Miraji ambaye hadi sasa bado ana bandeji ngumu kwenye kifundo cha mguu 'enka'.

Hata hivyo, alisema anafurahishwa na mwenendo wa klabu yake kwa kuendelea kushikilia usukani katika msimamo wa Ligi Kuu licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu wakati huu baadhi zikipanga kuepuka kushuka daraja.

"Nafurahi kuona timu yangu inazidi kuimarika na kuendelea kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu japo kuna baadhi ya timu Simba ikikutana nazo zinawakamia vilivyo, kikubwa ni ushirikiano uliopo kati ya wachezaji kwa wachezaji," alisema.

Alisema anaushukuru uongozi wa klabu hiyo kwa ushirikiano pamoja na moyo ambao wamekuwa wakimpa mara kwa mara katika kipindi chote ambacho hajafanikiwa kuitumia timu yake kutokana na kuwa majeruhi.

"Sina budi kuushukuru uongozi wangu pamoja na wachezaji wenzangu kwa ushirikiano pamoja na kunitia moyo mara kwa mara, jambo ambalo linanifanya nizidi kuimarika," alisema mchezaji huyo ambaye hadi anapata majeraha ya kifundo cha mguu alikuwa ameshacheka na nyavu mara sita kwenye Ligi Kuu.

TUNAJIFUA...



Wachezaji wa Pamba FC ya Mwanza, Alex Mwaisaka akimiliki mpira dhidi ya Nassoro Iddy, wakati wa mazoezi yaliyofanyika katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mechi zao za Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Maxime ahofia makali ya Namungo FC*

**Na Shufaa Lyimo**

KIWANGO kinachoonyeshwa na Namungo FC huku ikifanikiwa kuing'ang'ania Yanga katika Uwanja wa Majaliwa juzi, kimeitisha Klabu ya Kagera Sugar wakati huu timu hizo zikitarajiwa kukutana kesho katika mwendelezo wa Ligi Kuu.

Namungo iliyotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga juzi, itaikaribisha Kagera Sugar ambayo imetoka kuichapa Lipuli FC kwa bao 1-0 katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Samora, Iringa.

Akizungumza na Nipashe jana akiwa njiani kuelekea mkoani Ruangwa Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu mara nyingi wanapokutana na timu hiyo mechi huwa ngumu.

Maxime alisema licha ya kutokufanya vizuri katika michezo iliyopita hajakata tamaa na badala yake anaendelea kunoa wachezaji wake na tayari amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika kikosi chake.

"Mchezo utakuwa mgumu kutokana na aina ya timu tunayokutana nayo, makosa ambayo niliyabaini kwa wachezaji wangu nimeyafanyia kazi, naomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo ambayo tumeyapata katika michezo iliyopita, watambue kuwa mpira ndivyo ulivyo kuna kushinda na kushindwa," alisema.

Alisema alikaa na kuzungumza na wachezaji wake kutokana na makosa waliyoyafanya katika michezo iliyopita na kudai kila mchezaji amejua tatizo lake na kuahidi kutorudia kuyafanya tena katika mchezo wao ujao ambao ni kati ya mechi kali inayotarajiwa kuvutia mashabiki wengi kuitazama.

"Nilikaa na kuzungumza na wachezaji wangu kila mmoja nilimwambia tatizo lake wamenipa matumaini kwa sababu walinielewa na tangu nimezungumza nao kuna baadhi ya vitu ambavyo tayari nimeovina wameanza kubadilika," alisema.

Maxime alisema anakerwa na baadhi ya watu ambao timu inapokuwa haifanyi vizuri wanatoa maneno ya kuvunja moyo wachezaji kitu ambacho amedai kwenye mpira hakitakiwi kwa kuwa huchangia kushusha kiwango cha mchezaji husika.

Kagera Sugar ambayo imeshuka dimbani mara 29, ina pointi 41 katika nafasi ya nane, huku Namungo ikiwa nafasi ya nne na alama zake 50 baada ya mechi 28 kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo kinara ni Simba yenye pointi 71.

Michezo

Jumanne Machi 17, 2020

Nipashe




Shearer ataka Liver wasipewe ubingwa EPL UKURASA 30

TUNAJIWINDA...




Wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar e Salaam jana kujiandaa na fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN, zinazotarajiwa kufanyika nchini Cameroon kuanzia Aprili 4-25, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba SC kutangazia ubingwa Nangwanda

## ●●● Sven asema hakuna kulala, ataka gharika ya mabao kikosi kikirejea, huku...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU mechi zao za Ligi Kuu zikiwa zimesimamishwa kutokana na kuwakosa wachezaji saba waliopo katika kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' inayojiandaa na fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ni wazi sasa Simba imebakiza mechi tano tu za kushinda ili kutangazwa bingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

**Kitendo cha Yanga kutoka sare juzi ugenini dhidi ya Namungo FC, kinaifanya Simba yeye alama 71 baada ya mechi 28, sasa kuhitaji pointi 14 tu ili kufikisha 85 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Katika msimamo huo, Azam FC ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 54 baada ya mechi 28 huku ikifuatiwa na Yanga yenye alama 51 zilizotokana na kushuka dimbani mara 27, hiyo ikiwa na maana kama timu hizo zitashinda mechi zao zote zilizosalia, kila moja itafikisha pointi 84, lakini pia ikumbukwe bado hazijakutana zenyewe kwa zenyewe.

Hivyo, kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu, Simba ambayo imebakiza mechi 10 kabla ya msimu huu kufikia ukingoni, kama itahitaji kujihakikishia ubingwa huo mapema, inapaswa kushinda mechi zake tano zijazo ikianza na Ruvu Shooting katika Uwanja wa Taifa, kisha Mwadui FC (Taifa), Mbeya City (Sokoine), Tanzania Prisons (Sokoine) na kuhitimisha na Ndanda FC kwenye dimba la Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Ikifanikiwa kuibuka na ushindi katika mechi hizo, michezo inayofuata dhidi ya Namungo FC katika Uwanja wa Majaliwa, Mbao FC (Taifa), Alliance (Taifa), Coastal Union (Mkwakwani) na Polisi Tanzania kwenye dimba la Ushirika, itakuwa ikisaka tu rekodi ya kumaliza na pointi nyingi.

Na kuonyesha Simba imepania kumaliza biashara mapema, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck amesema hakuna kulala na kwamba wachezaji waliobaki kikosini wanaendelea kujifua.

Nyota wa Simba walioitwa katika kikosi cha Taifa Stars, ni Aishi Manula, Erasto Nyoni, Jonas Mkude, John Bocco, Hassan Dilunga, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Sven alimwambia mwandishi wetu: "Licha ya kuwa wengine wapo timu ya taifa, hakuna muda wa kupumzika kwa wachezaji waliobaki ni lazima wafanye mazoezi ili kuwa bora".

Akizungumzia ushindi uliopita wa mabao 8-0 dhidi ya Singida United, Sven alisema anahitaji kutoa darasa zaidi kwa safu yake ya ushambuliaji ili kutumia kila nafasi wanayoipata kwa kufunga kila wanapotengeneza nafasi ya kufanya hivyo.

"Unapopata nafasi ya kufunga unatakiwa kufunga mabao mengi bila kujali ambayo umeshafunga, tunahitaji pointi tatu na mabao mengi pia," alisema kocha huyo aliyerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems.

Simba ambayo pia inaongoza kwa kufunga mabao mengi (63) na kuruhusu machache (15) hadi sasa katika ligi hiyo, inaendelea na mazoezi katika viwanja vyao vya Mo Simba Arena vilivyopo Bunju, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

# TFF yajichimbia kujadili corona

**Na Saada Akida**

TAARIFA iliyotolewa rasmi jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ya kubainika mgonjwa mwenye maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), imelishtua Shirikisho la Soka nchini (TFF) na kuamua kujichimbia mapema kujadili mustakabli wa Ligi Kuu kuendelea ama la, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao alisema hawezi kuzungumza suala lolote kuhusu kusimama kwa ligi kwa sasa kwani vikao bado vinaendelea ili kujua hatua ya kuchukua.

"Kwa sasa ni vigumu kusema lolote, kwani bado Bodi ya Ligi inaendelea na vikao vya ndani," alisema Kidao.

Akitangaza jinsi mgojwa huyo alivyobainika nchini, Waziri Ummy alisema: "Machi 15 (Jumapili), tulipokea msafiri Mtanzania mwanamke (46), ambaye aliwasili nchini na ndege ya Rwanda Air akitokea Ubelgiji. Msafiri huyu aliondoka nchini Machi 3, mwaka huu na kati ya Machi 5 na 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena nchini humo na baada ya hapo kurejea Tanzania," alisema.

"Msafiri huyu alipita KIA akafanyiwa ukaguzi na kuonekana kutokuwa na homa. Baadaye alianza kujisikia vibaya akiwa hotelini na kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mt. Meru ambako alichukuliwa sampuli na kupelekwa Maabara ya Taifa ya Afya iliyoko jijini Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi na kuthibitisha kuwa ana maambukizo ya ugonjwa wa corona (COVID-19) na anaendelea vizuri," alisema.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya duniani (WHO), hadi sasa virusi vya corona vimeenea zaidi ya nchi 132 huku vikisababisha vifo 6,500.

9 770856 541002 >